

NJIA YA IBADA

Sehemu za kitabu cha Sala ya Asubuhi na Jioni, Litania na Ushirika Utakatifu, zisemwe au kuimbwa na watu, pamoja na sehemu za Katekismo na Zaburi nyingine na nyimbo.

BOOK OF WORSHIP

Parts of the Book of Common Prayer, the Litany and Holy Communion, to be said or sung by the people, together with parts of the Catechism and some Psalms and hymns.

NJIA YA IBADA

Swahili: Book of Worship

LONDON:

SOCIETY FOR PROMOTING
CHRISTIAN KNOWLEDGE

NJIA YA IBADA

DIBAJI

Kusudi la kitabu hiki ni kutoa kitabu rahisi kwa kutumia Wenyaji katika Sala zao za kanuni. Wengi hawawezi kununua Kitabu cha Sala kizima, na kwa hiyo hawawezi kuabudu vizuri. Kitabu hiki kitawasaidia sana kuabudu na akili zaidi na kusali vizuri.

“Anitoleae sifa mimi hunitukuza.”

INTRODUCTORY NOTE

The purpose of this book is to provide a book at low cost for the use of African congregations at the ordinary services of the Church. Many cannot afford the complete Book of Common Prayer and a Hymn Book. They are therefore not able to take their proper part in worship. This book should help them to a more sincere and intelligent worship.

“Whoso offereth me praise, glorifieth me”.

DURAI

Kaundi la kitabu hiki ni kuuza kitabu tabiri kwa
kumunia Wenyewe kitabu zote za kumunia Wenyewe
kawawazi kumunia Kitabu cha Sais kumunia na kaw-
awazi kawawazi kawabuni viziwi Kitabu hiki kitawa-
zaidia sana kitabuni na kitabu hiki ni kitabu viziwi
"Aniotele aha mimi huminduka"

INTRODUCTORY NOTE

The purpose of this book is to provide a book at low
cost for the use of African congregations at the ordinary
services of the Church. Many cannot afford the com-
plete book of Common Prayer and a Hymn book. They
are therefore not able to take their proper part in worship.
This book should help them to a more sincere and
intelligent worship.
"Wote otafika me pame, kiofika me"

NJIA YA IBADA

YALIYOMO

	PAGE
INTRODUCTORY NOTE	v
NJIA YA IBADA	1
LITANIA	9
USHIRIKA UTAKATIFU	15
MAFUNDISHO YA KANISA YANAYOWAPASA WATU WOTE KUYAJUA	21
ZABURI NYINGINE ZA DAUD	24
NYIMBO	51
INDEX	213

NJIA YA IBADA

¶ *Mwanzo wa Sala ya Asubuhi na Fioni Mhudumu asome mojawapo ya Aya za Maandiko Matakatifu. Kisha aseme maonyo ya Ibada. Baada ya maonyo, wote wapige magoti, waseme ungamo lifuatalo.*

UNGAMO

BABA Mwenyiezi na mwenye rehema ; Tumekosa kwa kutokufuata njia zako takatifu. Tumekuwa kama kondoo waliopotea. Tumefuata mno mawazo na tamaa zetu. Tumezihalifu sharia zako takatifu. Tumeyaacha yaliyotupasa kutenda. Tumeyatenda yasiyotupasa kutenda ; Wala uzima hatunao. Uturehemu Wewe Bwana, sisi maskini wenye dhambi. Uwaachilie, Mungu, wanaoungama dhambi zao. Uwarudishe wanaotubu ; Kwa ahadi zako ulizowaahidia wana Adamu kwa Kristo Yesu Bwana wetu. Na kwa ajili yake, Baba wa rehema, Utujalie tuyatende tangu leo mambo ya kitawa, ya haki, na ya kiasi. Jina lako takatifu litukuke. Amin.

¶ *Kasisi tu ndiye awezaye kusema Ghofira au Ondoleo la Dhambi, lakini kila Mhudumu ana ruhusa kusema sala hii :*

BWANA, twakusihii, uwakarimie watu wako wakuaminio samaha na amani, watakaswe na machukizo yote, wakutumikie kwa moyo usioshughulika ; kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amin.

WOTE WASEME SALA YA BWANA

BABA yetu, uliye mbinguni, Jina lako liwe takatifu. Ufalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe duniani, Kama yatimizwavyo mbinguni. Utupe leo riziki zetu. Utusamehe makosa yetu, Kama sisi tunavyowasamehe

waliotukosa. Usitutie majaribuni; Lakini utuokoe mavuni; Kwani ufalme, na nguvu na utukufu ni wako milele. Amin.

¶ *Kisha Mhudumu aseme :*

Bwana, ufunue midomo yetu.

Watu. Na vinyua vyetu vitanena sifa zako.

Mhudumu. Mungu, utuokoe kwa haraka.

Watu. Bwana, utusaidie hima.

¶ *Watu wakirwa wamesimama, Mhudumu aseme :*

Utukufu una Baba, na Mwana : na Roho Mtakatifu ;
Watu. Ulivyokuwa mwanzo : ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.

Mhudumu. Msifuni Bwana.

Watu. Jina la Bwana lisifiwe.

VENITE

NJONI, tumwimbie Bwana : tufanyie shangwe mwamba wa wokofu wetu.

Tuje mbele zake kwa shukrani : tumfanyie shangwe kwa zaburi.

Kwani Bwana ni Mungu mkuu : na Mfalme mkuu juu ya miungu wote.

Mkononi mwake zimo bonde za dunia : hata vilele vya milima ni vyake.

Bahari ni yake, ndiye aliyefanya : na mikono yake iliumba nchi kavu.

Njoni, tuabudu, tusujudu : tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba.

Kwani ndiye Mungu wetu : na sisi watu wa malisho yake, na kondoo za mkono wake.

Ingekuwa heri leo msikie sauti yake ! Msifanye migumu mioyo yenu : kama vile Meribah, kama siku ya Massah jangwani ;

Kama vile walivyoni jaribu baba zenu : wakanipima, wakayaona matendo yangu.

Miaka arubaini nalihuzunika nacho kizazi hiki nika-

sema : watu waliopotoka mioyo hawa, hawakujua njia zangu.

Nikaapa kwa hasira yangu : wasiingie rahani mwangu.

Utukufu una Baba, na Mwana : na Roho Mtakatifu ;

Ulivyokuwa mwanzo : ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.

¶ *Kisha zifuata Zaburi : karatasi 24.*

Kisha lisomwe Somo la kwanza (katika Agano la Kale).

Baadaye watu waseme au kuimba wimbo huu wakati wa Sala ya Asubuhi :

TE DEUM LAUDAMUS

WEWWE, Mungu, twaskusifu : wewe, Bwana, twakukiri. Wewe Baba wa milele : ulimwengu wote unakuabudu.

Wewe Malaika zote : nazo Mbingu na Nguvu zote, Nao Makerubi na Maserafi : wakuambia hawakomi, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu : Mungu Bwana wa majeshi.

Mbingu na nchi zimejaa : enzi ya utukufu wako.

Wakusifu wewe : jamii tukufu ya Mitume.

Wakusifu wewe : shirika lenye sifa la Manabii.

Wakusifu wewe : jeshi la Mashahidi waliovaa mavazi meupe.

Kanisa takatifu katika nchi zote : lakukiri wewe.

Baba mwenye enzi : isiyo na kiasi.

Mwana wako pekee : wa kweli, wa kuabudiwa.

Na Mfariji : Roho Mtakatifu.

Wewe Kristo : ndiwe Mfalme wa utukufu.

Wewe Mwana wa milele : wa Baba.

Wewe ulipotaka kujifanya mtu, ili umwokoe Mwana Adamu : hukuchukizwa na tumbo lake Bikira.

Wewe ulipouhinda uchungu wa mauti : uliwafunulia waaminio Ufalme wa Mbingu.

Wewe unakaa mkono wa kuume wa Mungu : katika utukufu wake Baba.

Tunasadiki : utakuja kuwa Mwamuzi.

Kwa hiyo, twakuomba uwasaidie watumwa wako : uliowakomboa kwa damu yako ya thamani.

Uwajalie pamoja na Watakatifu wako : utukufu wa milele.

Uwaokoe watu wako, Bwana : uubarikie urithi wako.

Uwatawale : uwainue hata makao ya milele.

Sisi kila siku : twakutukuza.

Twalisifu Jina lako : zamani hizi na za milele.

Ukubali, Bwana, kutulinda leo : tusipate dhambi.

Utuhemu, Bwana : utuhemu sisi.

Utuheme huruma, Bwana : kwani sisi twakutumaini wewe.

Nimekutumaini wewe, Bwana : nisipotee milele.

¶ *Wakati wa jioni waseme au kuimba Magnificat—Luka i. 46, ukurasa 7.*

Kisha lisomwe Somo la Pili (katika Agano Jipya).

Baadaye waimbe wimbo huu ufuatao :

JUBILATE. Zab. c.

MFANYIENI shangwe Bwana, dunia yote : mtumikieni Bwana kwa furaha, njoni mbele zake kwa kuimba.

Juani kwamba Bwana ndiye Mungu : ndiye aliye-tuumba, na sisi tu watu wake, na kondoo za malisho yake.

Ingieni milangoni mwake kwa kushukuru, nyuani mwake kwa kusifu : mshukuruni, lihimidini Jina lake.

Kwani Bwana ndiye mwema, rehema zake za milele : na uaminifu wake vizazi na vizazi.

Utukufu una Baba, na Mwana : na Roho Mtakatifu ;

Ulivyokuwa mwanzo, ulivyo sasa : utakavyokuwa milele. Amin.

¶ *Wakati wa jioni waseme au kuimba Nunc Dimittis—Luka ii. 29, ukurasa 8.*

¶ *Watu waiseme Imani ya Mitume.*

NAMWAMINI Mungu Baba Mwenyiezi, Muumba mbingu na nchi ;

Na Yesu Kristo Mwana wake pekee Bwana wetu,

Aliyechukuliwa mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Akazaliwa na Bikira Mariamu, Akateswa zamani za Pontio Pilato, Akasulibiwa, Akafa, Akazikwa, Akashuka pahali pa wafu ; Siku ya tatu akafufuka, Akapaa mbinguni, Anaketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyiezi ; Kutoka huko atakuja kuwahukumu watu wahai na wafu.

Namwamini Roho Mtakatifu ; Kanisa Takatifu, Katholiko ; Ushirika wa Watakatifu ; Ondoleo la dhambi ; Kiyama ya mwili, Na uzima wa milele. Amin.

¶ *Kisha Mhudumu aseme :*

Bwana akae nanyi.

Watu. Akae na roho yako.

Mhudumu. Tuombe.

Wote wapige magoti.

Bwana, utuhemu.

Watu. Kristo, utuhemu.

Mhudumu. Bwana, utuhemu.

Wote waseme pamoja :

BABA yetu, uliye mbinguni, Jina lako liwe takatifu. Bfalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe duniani, Kama yatimizwayo mbinguni. Utupe leo riziki zetu. Utusamehe makosa yetu, Kama sisi tunavyowasamehe waliotukosa. Usitutie majaribuni ; Lakini utuokoe maovuni. Amin.

Kisha Mhudumu asimame, aseme :

Bwana, utuonyeshe rehema yako.

Watu. Utupe wokofu wako.

Mhudumu. Bwana, umwokoe Mfalme.

Watu. Utusikie kwa rehema tukuombapo.

Mhudumu. Wahudumu wako uwavike haki.

Watu. Uwafurahishe wateule wako.

Mhudumu. Uwaokoe watu wako, Bwana.

Watu. Uubariki urithi wako.

Mhudumu. Utupe amani, Bwana, siku zetu.

Watu. Kwani hatuna mwingine wa kutupigania, ila wewe Mungu wetu.

Mhudumu. Mungu, utuumbie ndani mioyo safi.

Watu. Wala Roho yako Mtakatifu usituondolee.

¶ *Kisha zifuata Sala ya Siku, Sala ya Amani na Sala ya neema, na maombi mengine.*

Nyumbani na vijijini msimopatikana kitabu cha sala semeni sala ifuatayo badala ya Sala ya siku :

EBaba Mweyiezi, ndiwe uliyetuumba na kutukomboa Ekwa damu ya Mwana wako Mpenzi, ili tutangaze sifa zako. Utusaidie tukushuhudie kwa mawazo na maneno na matendo, ili tukutukuze na kuonyesha imani yetu kwa wengine, kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amin.

¶ *Maombi mengine.*

Wakati wa Sala za Jioni badala ya Sala ya Amani na Sala ya Neema, semeni Sala ya kuondoa Hofu na Sala ya Kuomba Msaada, na maombi mengine.

SALA YA MWISHO. II Wakor. xiii.

NEEMA ya Bwana wetu Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu, ukae nasi sote sasa na milele. Amin.

KUSHUKURU

Kushukuru kwa watu wengi pamoja.

MWENYIEZI Mungu, Baba wa rehema zote, sisi watumwa wako wanyonge twakushukuru kwa unyenyekevu na kwa moyo kwa wema wako wote na pendo lako kwetu sisi, na kwa watu wote. Twakutukuza kwa ajili ya kuumbwa kwetu, na kuhifadhika kwetu, na kwa baraka zote za maisha haya ; lakini zaidi ya yote, kwa pendo lako lisilopitika la kukombolewa ulimwengu na Bwana wetu Yesu Kristo ; kwa njia za neema, na tumaini la utukufu. Utupe, twakusihii, fahamu itupasayo ya rehema zako zote, mioyo yetu ikushukuru pasipo hila, nasi tuonyeshe sifa zako, si kwa midomo yetu tu, ila na kwa maisha yetu : tukijitia kabisa katika utumwa wako, tukienda mbele yako katika utakatifu na haki siku zetu zote ; kwa Yesu Kristo Bwana wetu, kwa huyo pamoja na wewe na Roho Mtakatifu iwe heshima yote na utukufu, maisha na milele. Amin.

¶ *Wakati wa Sala za Jioni watu waimbe uimbo huu baada ya Somo la Kwanza.*

MAGNIFICAT. Luka i.

MOYO wangu wamwadhimisha Bwana : roho yangu yamfurahia Mungu, Mwokozi wangu.

Kwani ameutazama : unyonge wa mjakazi wake.

Kwani hakika, tokea leo : vizazi vyote wataniita heri.

Kwani aliye hodari amenitendea makuu : na Jina lake ni takatifu.

Na rehema zake vizazi hata vizazi : kwao wanaomcha.

Ametenda nguvu kwa mkono wake : amewatawanya walio na kiburi katika mioyo yao.

Amewashusha wakuu katika viti : amewakweza wanyonge.

Wenye njaa amewashibisha mema : wenye mali amewaondoa mikono mitupu.

Kwa kukumbuka rehema amemsaidia Israeli mtumishi wake : kwa jinsi alivyowaambia baba zetu, Ibrahimu na uzao wake, hata milele.

Utukufu una Baba, na Mwana : na Roho Mtakatifu ;

Uliyoyokuwa mwanzo : ulivyo sasa, utukavyokuwa milele. Amin.

¶ *Tena waimbe wimbo huu baada ya Somo la Pili.*

NUNC DIMITTIS. *Luka ii. 29.*

SASA wamruhusu, Bwana, mtumwa wako kwa amani : skama ulivyosema.

Kwani macho yangu : yameuona wokofu wako.

Ulioweka tayari : machoni pa watu wote.

Nuru ya kuwaangaza mataifa : na kuwa utukufu wa watu wako Israeli.

Utukufu una Baba, na Mwana : na Roho Mtakatifu ;

Uliyoyokuwa mwanzo : ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.

LITANIA

MUNGU Baba, wa mbinguni : uturehemu maskini wenye dhambi.

Mungu Baba, wa mbinguni : uturehemu maskini wenye dhambi.

Mungu Mwana, Mkomboa ulimwengu : uturehemu maskini wenye dhambi.

Mungu Mwana, Mkomboa ulimwengu : uturehemu maskini wenye dhambi.

Mungu Roho Mtakatifu, utokae katika Baba na Mwana : uturehemu maskini wenye dhambi.

Mungu Roho Mtakatifu, utokae katika Baba na Mwana : uturehemu maskini wenye dhambi.

Utatu Mtakatifu, Mhimidiwa, Mtukufu, Nafsi tatu na Mungu mmoja : uturehemu maskini wenye dhambi.

Utatu Mtakatifu, Mhimidiwa, Mtukufu, Nafsi tatu na Mungu mmoja : uturehemu maskini wenye dhambi.

Usiyakumbuke, Bwana, makosa yetu ; wala makosa ya baba zetu ; wala usitupatilize kwa dhambi zetu ; utuachilie, Bwana mwema, waachilie watu wako, uliowakomboa kwa damu yako ya thamani, wala usituonee hasira milele,

Utuaachilie, Bwana mwema.

Na mabaya yote na madhara ; na dhambi, na hila na jeuri za Shetani ; na ghadhabu yako na laana la milele,

Utuoakoe, Bwana mwema.

Na upofu wote wa moyo ; na kiburi, majisifu, na nafiki ; na husuda, chuki, na uovu, na kutopendana kwote,

Utuoakoe, Bwana mwema.

Na uasharati na dhambi zingine zote za kufisha ; na madanganya yote ya dunia, ya mwili, na ya Shetani,

Utuoakoe, Bwana mwema.

Na umeme na tufani ; na tauni, maradhi, nzige na njaa ; na vita na uaji, na na mauti ya ghafula,

Utuoakoe, Bwana mwema.

Na maafikano ya fitina ya siri, na kuasi ; na elimu ya uwongo, uzushi, na kufarakana kwa dini ; na kuwa na moyo mgumu, na kulidharau Neno na amri zako.

Utuo koe, Bwana mwema.

Kwa siri ya Kufanyika mwili kwako kutakatifu ; kwa Kuzaliwa kwako kutakatifu, na Kutahiriwa ; kwa Kubatizwa kwako, Kufunga, na Kujaribiwa,

Utuo koe, Bwana mwema.

Kwa huzuni yako, na Hari ya damu ; kwa Msalaba wako na Kuteswa ; kwa Kufa kwako kwa thamani, na Kuzikwa ; kwa Kufufuka kwako kutukufu na Kupaa ; na kwa kuja kwake Roho Mtakatifu,

Utuo koe, Bwana mwema.

Wakati wote wa kutaabika kwetu ; wakati wote wa kufanikiwa ; saa ya kufa, na siku ya kuhukumiwa,

Utuo koe, Bwana mwema.

Sisi wenye dhambi twakusih utusikie, Bwana Mungu : upende kulitawala na kuliongoza Kanisa lako takatifu Katholiko, lishike njia njema ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

[Upende kumbariki mfalme wa inchi hii, na kuuongoa moyo wake aikubali kweli yako ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.]

Upende kuwaangaza Maaskofu wote, Makasisi, na Mashemasi, wajue na kufahamu kwa kweli Neno lako ; wakalieneze kwa mafundisho na kwa mwenendo wao ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwavika watu wakuu wa Serkali na wazee wote neema, hekima, na akili ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwabariki na kuwalinda makadhi, [maliwali, na maakida,] na watu wote wenye mamlaka ; ukiwajalia neema ya kutenda haki, na kuihakikia kweli ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwabariki na kuwalinda watu wako wote ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwapa mataifa yote umoja, amani, na urafiki ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kutujalia moyo wa kukupenda na kukucha, na kufuata kwa bidii amri zako ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwazidishia neema watu wako wote, ili kwa unyenyekevu walisikia Neno lako, walikubali kwa moyo safi, na kuzaa matunda ya Roho ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwaleta katika njia ya kweli Washenzi na Waislamu na wote waliopotea na kudanganyika ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwaimarisha wasimamao ; kuwafariji na kuwasaidia walio na moyo dhaifu ; kuwainua waangukao ; na hatima kumkanyaga Shetani chini ya miguu yetu ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwatunza, kuwasaidia, na kuwafariji wote walio katika hatari, shidda, na taabu ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwahifadhi wote wanaosafiri katika inchi au baharini, wanawake wote walio na utungu wa kuzaa, wagonjwa wote, na watoto wote wachanga, na kuwahurumia wafungwa wote ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwalinda na kuwaruzuku watoto wote wasio na baba, wanawake waliofiwa na waume zao, na wote wasio na msaada, na wanaooneka ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwarehemu watu wote ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kuwasamehe adui zetu, nao watufukuzao na watusingiziao, uwageuze mioyo ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kutupa na kutuhifadhia mazao ya inchi kwa jinsi yake, tupate kuyatumia wakati wake ;

Twakusih utusikie, Bwana mwema.

Upende kutujalia tutubu kwa kweli ; kutusamehe dhambi zetu zote, za ulegevu na ujinga, na utuvike

neema ya Roho yako Mtakatifu, tutengeneze mwenendo wetu kwa Neno lako takatifu ;

Twakusihhi utusikie, Bwana mwema.

Mwana wa Mungu : twakusihhi, utusikie.

Mwana wa Mungu : twakusihhi, utusikie.

Mwana Kondoo wa Mungu : uzichukuae dhambi za ulimwengu ;

Utupe amani yako.

Mwana Kondoo wa Mungu : uzichukuae dhambi za ulimwengu ;

Utuhemumu sisi.

Kristo, utusikie.

Kristo, utusikie.

Bwana, utuhemumu.

Bwana, utuhemumu.

Kristo, utuhemumu.

Kristo, utuhemumu.

Bwana, utuhemumu.

Bwana, utuhemumu.

¶ *Kiisha Mhudumu na watu pamoja nae waseme Sala ya Bwana.*

BABA yetu, uliye mbinguni, Jina lako liwe takatifu. Bwafalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe duniani, Kama yatimizwavyo mbinguni. Utupe leo riziki zetu. Utusamehe makosa yetu, Kama sisi tunavyowasamehe waliotukosa. Usitutie majaribuni ; Lakini utuokoe maovuni. Amin.

Mhudumu. Bwana, usitutendee kwa hesabu ya dhambi zetu.

Jibu. Wala usitulipe kwa kadiri ya maovu yetu.

Tuombe

MUNGU, Baba wa rehema, usiyedharau kilio chao waliopondeka moyo, wala haja zao walio na huzuni ; ukubali kwa rehema sala zetu tukuombazo katika taabu na misiba yetu yote itulemeapo ; utusikie kwa neema, ili

mabaya hayo, tutendewayo kwa hila na werevu wa Shetani au wa wana Adamu, yakome ; na kwa tunza la wema wako yaondolewe ; ili sisi watumwa wako, tusipozuiwa na mafukuzo, tukushukuru daima katika Kanisa lako takatifu ; kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

Bwana, uondoke, utusaidie, utuokoe kwa ajili ya Jina lako.

Mungu, tumesikia kwa masikio yetu, na baba zetu wametuambia mambo makuu, uliyoyatenda siku zao, na zamani za kale kabla yao.

Bwana, uondoke, utusaidie, utuokoe kwa ajili ya heshima yako.

Utukufu una Baba, na Mwana : na Roho Mtakatifu ; *Jibu.* Uliyokuwa mwanzo : ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.

Na adui zetu utulinde, Kristo.

Uyaangalie kwa wema mateso yetu.

Utazame kwa huruma huzuni ya mioyo yetu.

Usamehe kwa rehema dhambi za watu wako.

Kwa upendeleo na rehema usike sala zetu.

Mwana wa Daud, utuhemumu.

Sasa na daima upende kutusikia, Kristo.

Utusikie kwa wema, Kristo ; utusikie kwa wema, Bwana Kristo.

Mhudumu. Bwana, utuonyeshe rehema yako ;

Jibu. Kama sisi tunavyokuamini wewe.

Tuombe

BABA, twakusihhi kwa unyenyekevu, uziangalie kwa rehema dhaifu zetu ; na kwa ajili ya kutukuka Jina lako, utuepushie mbali mabaya hayo yote, tuliyoystahili kwa haki ; utujalie, katika taabu zote, tuamini na kutumainia kabisa rehema zako, na tukutumikie siku zote katika utakatifu na mwenendo safi, kwa heshima na utukufu wako ; kwa Msuluhisha na Mneni wetu mmoja, Yesu Kristo Bwana wetu. Amin.

Sala ya KRUSOSTOMO Mt.

MWENYIEZI Mungu, uliyetujalia neema wakati huu kushirikiana kutaka haja zetu mbele yako; umeahidi, ya kwamba watu wawili au watatu wakikutanika kwa Jina lako, utawapa haja zao; Fikiliza sasa, Bwana, haja na maombo ya watumwa wako kwa jinsi itakavyotufaa; ukitujalia tuijue kweli yako katika ulimwengu huu, na katika ulimwengu ujao uzima wa milele. Amin.

2 *Wakor.* xiii.

NEEMA ya Bwana wetu Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu, ukae nasi sote maisha na milele. Amin.

USHIRIKA UTAKATIFU

¶ *Kasisi na Askofu tu ndio wawezao kufanya Ibada ya Ushirika Utakatifu.*

Kasisi ataanza Ibada ya Ushirika Utakatifu kwa kusema Sala ya Bwana peke yake, pamoja na Sala ya usafi wa roho. Kisha Kasisi atasema Amri Kumi za Mungu. Baada ya kila amri, watu wajibu:

Bwana, uturehemu, tuelekeze mioyo tuishike amri hii.

AMRI KUMI

1. Usiwe na miungu wengine ila mimi.
2. Usijifanyizie sanamu ya kuchora, wala mfano wa kitu cho chote kilichoko juu mbinguni, wala chini duniani, wala majini chini ya nchi. Usivisujudu, usiviabudu: kwani mimi Bwana Mungu wako Mungu mwivu, nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne wanichukiao; nami nawarehemu elfu elfu wanipendao, na kushika amri zangu.
3. Usilitaje bure Jina la Bwana Mungu wako, kwani Bwana hatamtoa hatiani alitajaye Jina lake bure.
4. Ikumbuke sikuya Sabato, itakase. Siku sita fanya kazi, tenda mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana Mungu wako; Usitende kazi yo yote, wewe, wala mwanao, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala nyama zako, wala mgeni aliomo nyumbani mwako. Kwani kwa siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi, bahari na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba: kwa sababu hii Bwana akaibariki siku ya saba akaitakasa.
5. Waheshimu baba yako, na mama yako; siku zako zipate kuzidi katika nchi upewayo na Bwana Mungu wako.
6. Usiue.
7. Usizini.
8. Usiibe.
9. Usimshuhude jirani yako uwongo.

10. Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako, wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alichacho nacho jirani yako.

¶ *Jibu la mwisho :*

Bwana, uturehemu, uziandike, twakusihhi, amri hizi zote mioyoni mwetu.

¶ *Kisha ifuate Sala ya Mfalme na ya siku.*

Ndipo watu wakae wasikilize Waraka.

Baada ya Waraka hufuata Injili.

*Wakati wa kutangaza Injili, watu wasimame na kusema :
Utukufu uwe kwako, Ee Mungu.*

¶ *Ikiisha Injili, watu waseme :*

Shukrani iwe kwako, Ee Mungu, kwa Injili yako hii takatifu.

¶ *Ndipo wote waseme au kuimba Imani ya Nike.*

IMANI YA NIKE

NAMWAMINI Mungu mmoja Baba Mwenyiezi, Muumba mbingu na nchi, Na vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana :

Na Bwana mmoja Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu, Amezaliwa na Baba kabla ya zamani zote, Yu Mungu anatoka katika Mungu, Yu Nuru anatoka katika Nuru, Yu Mungu kweli anatoka katika Mungu kweli, Amezaliwa, hakuumbwa, Mwenye asili moja na Baba, Kwa yeye huyu vitu vyote vyaliumbwa : Aliyeshuka kutoka mbinguni kwa ajili yetu wana Adamu, na kwa wokofu wetu, Akatwaa mwili kwa uweza wa Roho Mtakatifu katika Bikira Mariamu, Akawa mwana Adamu, Akasulibiwa kwa ajili yetu, zamani za Pontio Pilato. Aliteswa akazikwa, Siku ya tatu akafufuka kama yanavyo Maandiko Matakatifu, Akapaa mbinguni, Anaketi mkono wa kuume wa Baba. Naye atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu watu wahai na wafu. Na milki yake haina mwisho.

Namwamini Roho Mtakatifu, Bwana, Mtoa uzima, Atokaye katika Baba na Mwana, Anayebudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, Aliyenena kwa vinywa vya Manabii. Naamini Kanisa moja, Takatifu, Katholiko, na Apostoliko. Nakiri Ubatizo Umoja wa kuondolea dhambi. Natazamia Kiyama ya wafu, na uzima wa ulimwengu ujao. Amin.

MATANGAZO

HOTUBA

SADAKA

¶ *Kasisi aweke Mkate na Divai mezani, kisha aseme :*

Tuliombe Kanisa la Kristo pia lifanyalo vita hapa duniani.

¶ *Kuwakaribisha Washiriki.*

Waalikwe wote walio tayari, wenye toba na upendano na maisha ya kumpendeza Mungu, wakipokee chakula cha Bwana.

UNGAMO

MWENYIEZI Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Muumba vitu vyote, Mhukumu watu wote, Twaungama na kujutia dhambi na uovu wetu, Tuliotenda kwa ubaya mno siku hizi zote. Tumewaza, tumenena, tumetenda mambo ya kukuchukiza wewe, Mwenyiezi Mungu. Hata itakuwika haki kutukasirikia na kutughadhabikia. Tumejuta kwa majuto makuu. Tume-yasikitikia sana haya makosa yetu. Kuyakumbuka tu kunatuhuzunisha ; Ni kama mzigo usiochukulika. Uturehemu, Uturehemu, Baba wa rehema ; Kwa ajili ya Mwana wako Bwana wetu Yesu Kristo, Utusamehe yote yaliyopita ; Utujalie tangu leo tukutumikie, Tukupende katika upya wa maisha, Kwa heshima na utukufu wa Jina lako ; kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amin.

Kasisi (au Askofu akiwapo) aseme GHOFIRA.

MANENO YA FARAJA.

¶ *Kisha Kasisi aseme :*

Inueni mioyo.

Watu. Twaiinua kwa Bwana.

Kasisi. Na tumshukuru Bwana Mungu wetu.

Watu. Ina haki, tena ni wajib.

¶ *Kisha Kasisi aikabili Meza ya Bwana, aseme :*

NDIO wajib wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru Bwana, Baba Mtakatifu, Mungu Mwenyiczi wa milele. Kwa hiyo sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika wakuu, na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu; tukikusifu daima tukisema,

Wote Waseme

MTAKATIFU, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa Sabaoth, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako: Utukufu u kwako, Bwana uliye juu. Amin.

Kasisi aseme SALA YA UNYONGE

HATUTHUBUTU kuikaribia Meza yako, Bwana mwenye Rehema, tukiitumainia haki yetu sisi, ila rehema zako nyingi zilizo kuu. Hatustahili hata kuokota makombo chini ya Meza yako. Wewe ndiwe Bwana yeye yule, sifa zako ni kuwa na rehema siku zote: Basi utujalie, Bwana mwema, tule nyama ya Mwana wako mpendwa Yesu Kristo, na kunywa damu yake, kwa jinsi miili yetu yenye dhambi isafike kwa mwili wake, na roho zetu ziosheke kwa damu yake ya thamani, tukae daima ndani yake, na yeye ndani yetu. Amin.

SALA YA KUFANYA WAKF MKATE NA DIVAI

¶ *Kasisi aseme peke yake.*

MWENYIEZI Mungu, Baba yetu wa mbinguni, kwa Mwema na huruma zako ulitupa Mwana wako pekee Yesu Kristo afe msalabani kwa ukombozi wetu nae

alitoa Msalabani sadaka ya nafsi yake mara moja tu, iwe dhabihu, na sadaka, na kafara, timilifu, kamili, ya kutosha, kwa dhambi za ulimwengu wote: alituamuru, na katika Injili yake takatifu alituusia tufulize daima kumbukumbu la kufa kwake kwa thamani, hata atakaporudi; Utusikie, Baba wa rehema, twakuomba kwa unyenyekevu: na kwa kupokea viumbe hivi vyako, Mkate na Divai, kwa agizo takatifu la Mwana wako Yesu Kristo Mwokozi wetu, tukikumbuka kufa na kuteswa kwake, utujalie tuushiriki Mwili na Damu yake mbarikiwa: * Yeye usiku ule ule alitolewa alitwaa Mkate; na akiisha kushukuru † akaumega, akawapa wanafunzi wake, akisema, Twani, mle, ‡ Huu ndio Mwili wangu ulitolewa kwa ajili yenu: Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula § akatwaa Kikombe; na akiisha kushukuru, akawapa, akisema, Nyweeni nyote hiki; kwani || hii ndiyo Damu yangu ya Agano Jipya, imwagikayo kwa ajili yenu, na kwa watu wengi, kwa ondoleo la dhambi: Fanyeni hii, kila mtakapokunywa, kwa ukumbusho wangu. Amin.

¶ *Kwanza Kasisi apokee Ushirika mwenyewe, kisha Maaskofu na Makasisi na Mashemasi, kisha na watu.*

Akimshirikisha mtu Mkate aseme :

MWILI wa Bwana wetu Yesu Kristo, ulitolewa kwa Majili yako, ukulinde mwili na roho hata uzima wa milele. Pokea, ule huu, ukikumbuka kuwa Kristo alikufa kwa ajili yako, na wewe umle yeye moyoni kwa imani na shukrani.

¶ *Akimshirikisha mtu Kikombe, aseme :*

DAMU ya Bwana wetu Yesu Kristo, iliyomwagika kwa ajili yako, ikulinde mwili na roho hata uzima wa

* Hapa Kasisi atwae sahani mikononi mwake.

† Hapa amega Mkate.

‡ Hapa aweke mkono wake juu ya kila sahani.

§ Hapa atwae kikombe mikononi mwake.

|| Hapa aweke mkono wake juu ya kila chombo chenye Divai ya kufanyika Ukufu.

milele. Unywe hii ukikumbuka kuwa Damu yake Kristo ilimwagika kwa ajili yako, ushukuru.

Wote waseme SALA YA BWANA.

Kasisi aseme Sala ya Kunshukuru Mungu.

¶ *Wote waseme au kuimba.*

UTUKUFU una Mungu juu, katika nchi amani, kwa watu nia njema. Twakusifu, twakuhimidi, twakuabudu, twakutukuza, twakushukuru, kwa ajili ya utukufu wako mkuu, Bwana Mungu, Mfalme wa mbinguni, Mungu Baba Mwenyiezi.

Bwana, Mwana pekee, Yesu Kristo; Bwana Mungu, Mwana Kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba, uchukuae dhambi za ulimwengu, uturehemu. Uchukuae dhambi za ulimwengu, ukubali kuomba kwetu. Uketiye mkono wa kuume wa Mungu Baba, uturehemu.

Kwani ndiwe uliye peke yako Mtakatifu; ndiwe peke yako Bwana; ndiwe peke yako uliye juu, Yesu Kristo, pamoja na Roho Mtakatifu, katika utukufu wake Mungu Baba. Amin.

BARAKA

MAFUNDISHO YA KANISA YANAYO-WAPASA WATU WOTE KUYAJUA

SEHEMU ZA KATEKISIMO

AHADI TATU ZA UBATIZO

LA kwanza, kwamba nitamkataa Shetani na kazi zake zote, mapendezo na mambo yasiyofaa ya dunia hii mbaya, na tamaa mbaya zote za mwili. La pili, kwamba nitaziamini sharti zote za Imani ya Kikristo. Na la tatu, kwamba nitayashika mapenzi na amri takatifu za Mungu, na kuzifuata siku zote za maisha yangu.

MAFUNDISHO YA IMANI

KWANZA, nafundishwa kumwamini Mungu Baba, aliyeniumba mimi, na ulimwengu wote.

La pili, kumwamini Mungu Mwana, aliyenikomboa mimi, na wana Adamu wote.

La tatu, kumwamini Mungu Roho Mtakatifu, anitakasae mimi, na watu wateule wa Mungu wote.

MAFUNDISHO YA AMRI KUMI

NAFUNDISHWA mambo mawili: yanipasayo kwa Mungu, na yanipasayo kwa Jirani yangu.

Swali. Imekupasaje kwa Mungu?

Jibu. Imenipasa kwa Mungu, kumwamini, kumcha, na kumpenda, kwa moyo wangu wote, kwa akili zangu zote, kwa roho yangu yote, na kwa nguvu zangu zote; kumwabudu, kumshukuru, kumtumainia kabisa, kumwomba, kuliheshimu Jina lake takatifu na Neno lake, na kumtumikia vema siku zote za maisha yangu.

Swali. Imekupasaje kwa Jirani yako?

Jibu. Imenipasa kwa Jirani yangu, kumpenda kama nafsi yangu, na kuwatendea watu wote, kama nitakavyo wao wanitendee mimi: Kuwapenda, kuwaheshimu,

kuwasaidia baba na mama yangu: Kumheshimu na kumtii Mfalme, na wakuu wote walio chini yake: Kujitiisha kwa wakubwa wangu, waalimu wangu, mapadri na bwana zangu: Kunyenyekaa mbele zao wote walio wakubwa kuliko mimi: Kujiangalia nisimdhuru mtu kwa neno wala kwa tendo: Kuwa adili na mwenye haki katika shughuli zangu zote: Kutokuwa na kinyongo wala machukio moyoni mwangu: Kuizua mikononyangu isiibe kitu cho chote, ulimi wangu usitukane, wala usiseme uwongo, wala usisingizie: Kujiangalia mwili wangu niwe na kiasi, nisiwe mlevi, wala asharati: Nisitamani wala kutaka mali ya watu; lakini kujifunza na kufanya kwa bidii kazi ya kunipatia riziki zangu, na kutenda yanipasayo katika hali, Mungu atakayopenda kuniitia.

MAFUNDISHO YA SAKRAMENTI

Swali. Kuna Sakramenti ngapi alizoamuru Kristo katika Kanisa lake?

Jibu. Mbili tu, zilizo faradhi kwa wokofu wa watu wote, nazo ni Ubatizo, na Chakula cha Bwana.

Swali. Neno hili Sakramenti maana yake nini?

Jibu. Sakramenti ni dalili ya nje, na inayoonekana kwa macho, ya neema ya ndani na ya rohoni tunayopewa, imeamriwa na Kristo mwenyewe, kuwa njia ya kupokelea neema hiyo, na kuwa arabuni ya kutuyakinisha.

Swali. Kuna sehemu ngapi katika Sakramenti?

Jibu. Mbili; dalili ya nje na inayoonekana, na neema ya ndani na ya rohoni.

Swali. Dalili ya nje na inayoonekana kwa macho katika Ubatizo ni nini?

Jibu. Ni maji; mtu abatizwayo kwayo *Kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.*

Swali. Neema ya ndani na ya rohoni ni nini?

Jibu. Kufa kwa mambo ya dhambi, na kuzaliwa mara ya pili katika haki; Kwani tukiwa kwa asili tumezaliwa dhambini, na watoto wa ghadhabu, kwa Ubatizo tumezaliwa watoto wa neema.

Swali. Watu watakaobatizwa wamepasiwa nini?

Jibu. Toba, ili waache dhambi; na Imani, ili wazi-amini sana ahadi za Mungu walizopewa katika Sakramenti hii.

Swali. Kwani, basi, hubatizwa watoto wachanga, nao wakiwa hawawezi kutenda haya kwa kuwa wadogo?

Jibu. Kwa sababu wanaahidi mambo haya yote mawili kwa vinywa vya Wadamini wao; na wakipata kuwa watu wazima imewapasa wenyewe waifikilize ahadi hiyo.

Swali. Kwa kusudi gani Sakramenti ya Chakula cha Bwana imeamriwa?

Jibu. Kuwa kumbukumbu la siku zote la dhambi ya kufa kwake Kristo, na la mambo mema tunayopokea kwa kumbukumbu hilo.

Swali. Nini sehemu ya nje au dalili ya nje katika Chakula cha Bwana?

Jibu. Mkate na Divai, alivyoamuru Bwana vipokewe.

Swali. Nini sehemu ya ndani, au kitu kinachoashiriwa?

Jibu. Mwili na Damu ya Kristo zinazotwaliwa na kupokewa kwa kweli na pasipo shaka na waamini katika Chakula cha Bwana.

Swali. Mambo gani mema tupatayo kwa Mwili na Damu ya Kristo?

Jibu. Kwa Mwili na Damu ya Kristo twapata nguvu ya kuburudishwa roho zetu, kama vile miili yetu inavyopata nguva na kuburudishwa kwa mkate na divai.

Swali. Wale wajiao Chakula cha Bwana wamepasiwa nini?

Jibu. Kujihoji, kama kweli wametubia dhambi zao za zamani, na kukusudia sana kuishi maisha mapya; na kama wanaziamini sana rehema za Mungu zilizo katika Kristo, na kukumbuka kwa shukrani kufa kwake; na kama wana upendano na watu wote.

ZABURI NYINGINE ZA DAUD

ZABURI YA KWANZA

- 1 Yu heri mtu asiyekwenda katika shauri la wasi o haki :
Wala hakusimama katika njia yao wakosaji, wala hakukaa barazani mwao wenye mizaha.
- 2 Lakini hupendezwa na sharia ya Bwana :
Na sharia yake huitafakari mchana na usiku.
- 3 Bassi amekuwa kama mti uliopandwa kando ya mito :
Uzaao matunda kwa majira yake.
- 4 Majani yake hayanyauki :
Na kila atendalo hulifanikisha.
- 5 Wasio haki mbali :
Wao kama makapi yanayopeperushwa na upepo.
- 6 Kwa hiyo wasio haki hawatasimama hukumuni :
Wala wakosaji katika kusanyiko lao wenye haki.
- 7 Kwa kuwa Bwana anajua njia ya wenye haki :
Na njia yao wasio haki itaharibika.

ZABURI YA NANE

- 1 BWANA, Bwana wetu, Jina lako li tukufu ajabu mno katika dunia yote :
Wewe umeweka utukufu wako juu ya mbingu.
- 2 Vinywani mwa watoto na wanyonyao umeimarisha nguvu, kwa sababu ya adui zako :
Umkomeshe mwenye chuki na mipa kisasi.
- 3 Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako :
Mwezi na nyota, ulizozitengeneza.
- 4 Mtu ni kitu gani, umkumbuke :
Mwana Adamu, umjue ?
- 5 Umempunguza punde kidogo kuliko Mungu :
Wamtia taji ya utukufu na heshima.
- 6 Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako :

- Umevitia vitu vyote chini ya miguu yake.
- 7 Kondoo na ng'ombe, zote pia :
Na nyama za mwituni.
- 8 Ndege za angani, na samaki za baharini :
Killa kipitacho njia za baharini.
- 9 Bwana, Bwana wetu :
Jina lako li tukufu ajabu mno katika dunia yote.

ZABURI YA KUMI NA TANO

- 1 BWANA, nani atakaekaa katika masikani yako :
Nani atakaeketi katika kilima cha utakatifu wako ?
- 2 Ndiye aendae kwa ukamilifu, na kutenda haki :
Na kusema kweli moyoni mwake.
- 3 Asiyesingizia kwa ulimi wake ; wala kumtenda mabaya mwenziwe :
Wala kumshutumu jirani yake.
- 4 Machoni pake mwovu hudharauliwa ; lakini awahe-shimu wamchao Bwana :
Anaepa wala habadili ajapopata hasara.
- 5 Hakuweka fedha yake apate faida, wala hatwai rushwa amwangamize asiye hatia :
Atendae haya, hataondoshwa milele.

ZABURI YA KUMI NA KENDA

- 1 MBINGU zahubiri utukufu wa Mungu :
Anga yatangaza kazi za mikono yake.
- 2 Mchana husemezana na mchana :
Usiku hutoa maarifa kwa usiku.
- 3 Hakuna usemi wala lugha :
Sauti yao haisikilikani.
- 4 Kamba yao imeenea katika dunia pia, na maneno yao mpaka miisho ya ulimwengu :
Ameliwekea jua hema katika hizo.
- 5 Nalo kama bwana arusi akitoka chumbani mwake :
Lafurahi kama shujaa akienda mbio katika njia yake.

- 6 Kutoka kwake, katika mwisho wa mbingu, na kuzunguka kwake hatta miisho yake :
Wala hakuna kitu kinachofichikana na hari yake.
- 7 Sharia ya Bwana kamilifu, yaiburudisha roho :
Ushahidi wa Bwana thabiti, humwelemisha mjinga.
- 8 Amri za Bwana sawa, zaufurahisha moyo :
Agizo la Bwana safi, huyatia macho nuru.
- 9 Kicho cha Bwana kitakatifu, kinadumu milele :
Hukumu za Bwana za kweli, zina haki kabisa.
- 10 Ni za kutamanika kuliko dhahabu, kuliko dhahabu safi nyingi :
Nazo tamu kuliko asali, na kamba ya asali.
- 11 Tena mtumwa wako huonywa nazo :
Kwa kuzishika hupata thawabu nyingi.
- 12 Nani awezae kuyatambua makosa yake :
Unisafishe na mambo ya siri.
- 13 Umzuie mtumwa wako na mambo ya kiburi :
Yasinitawale, ndipo nitakuwa kamili, nitasafishwa na kosa lililo kubwa.
- 14 Maneno ya kinywa changu na kutafakari kwa moyo wangu kuwe na kibali mbele yako :
Bwana, mwamba wangu na mwokozi wangu.

ZABURI YA ISHIRINI NA TATU

- 1 BWANA ni mchungwa wangu :
Sitapunguka kitu.
- 2 Katika majani yameayo hunilaza :
Kando ya maji yaliyotulia hunipeleka.
- 3 Huniburudisha roho :
Huniongoza katika mapito ya haki kwa ajili ya Jina lake.
- 4 Hata nikipita katika bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya ; kwani wewe upo pamoja nami :
Fimbo yako na gongo lako ndivyo vinifarijivyo.
- 5 Waniandikia meza mbele ya watesi wangu :
Umenipaka mafuta kichwani ; kikombe changu kinafurika.

- 6 Hakika wema na rehema zitanifuata siku zote za maisha yangu :
Nami nitakaa nyumbani mwa Bwana siku nyingi.

ZABURI YA ISHIRINI NA NNE

- 1 INCHI na vyote pia vilivyomo mali ya Bwana :
Ulimwengu na wote wakao ndani yake.
- 2 Kwani ndiye aliyeweka juu ya bahari :
Na juu ya maji aliifanya thabiti.
- 3 Nani atakaepanda mlimani kwa Bwana :
Nani atakaesimama mahali pake patakatifu ?
- 4 Aliye na mikono safi, na moyo mweupe, asiyechukuliwa roho kwa ubatili :
Wala hakuapa kwa hila.
- 5 Atapokea baraka kwa Bwana :
Na haki kwa Mungu wa wokofu wake.
- 6 Kizazi hiki ndicho chao wantafutao :
Wakutafutao uso, Mungu wa Yakobo.
- 7 Inueni vichwa, enyi milango ; inukeni, enyi milango ya milele :
Na Mfalme wa utukufu ataingia.
- 8 Nani Mfalme huyu wa utukufu :
Bwana mwenye nguvu, hodari, Bwana hodari kwa mapigano.
- 9 Inueni vichwa, enyi milango ; naam, inueni, enyi milango ya milele :
Na Mfalme wa utukufu ataingia.
- 10 Nani aliye Mfalme huyu wa utukufu :
Bwana wa majeshi, ndiye mfalme wa utukufu.

ZABURI YA ISHIRINI NA SABA

- 1 BWANA ni nuru yangu na wokofu wangu : nimwogope nani :
Bwana ni ngome ya maisha yangu ; nimhofu nani ?
- 2 Watenda mabaya waliponikaribia wanile nyama :
Watesi wangu na adui zangu mimi, walijikwaa wakaanguka.

- 3 Ijapo jeshi lijipange kupigana nami, moyo wangu hautaogopa :
Ijapo vita itokee juu yangu, hata hivyo nitatumaini.
- 4 Neno moja nimelitaka kwa Bwana, ndilo nitakalotafuta :
Nikae nyumbani mwa Bwana siku zote za maisha yangu, niutazame uzuri wa Bwana, na kulitafakari hekalu lake.
- 5 Kwani atanisetiri hemani mwake siku ya ubaya :
Atanificha ndani ya hema yake, ataniinua juu ya mwamba.
- 6 Na sasa kichwa changu kitainuka juu ya adui zangu wanaonizunguka :
Nitatoa dhabihu za shangwe; hemani mwake nitamwimba, nitamsifu Bwana.
- 7 Usikie, Bwana, nipaazapo sauti yangu :
Unirehemu, uniitike.
- 8 Uliposema, nitafuteni uso; moyo wangu ulikuambia :
Uso wako, Bwana, nitautafuta.
- 9 Usinifiche uso wako; usimwondoshe mtumwa wako kwa hasira :
Umekuwa msaada wangu; usinitupe, wala kuniacha, Mungu wa wokofu wangu.
- 10 Babangu na mamangu wameniacha :
Bwana ndiye atakaenikaribisha.
- 11 Unifundishe njia yako, Bwana :
Uniongoze mahali paliponyoka, kwa sababu yao wanivizio.
- 12 Usinitie katika nia ya adui zangu :
Kwani mashahidi ya uwongo wameondoka wani-shtaki, nao wanaotoa jeuri kama pumuzi.
- 13 Ningalizimia kama nisingetumaini kuona wema wa Bwana :
Katika inchi ya wahayi.
- 14 Umngojee Bwana :
Uwe hodari, upige moyo konde, umngojee Bwana.

ZABURI YA ISHIRINI NA KENDA

- 1 MPENI Bwana, wenye mavazi matakatifu :
Mpeni Bwana utukufu na nguvu.
- 2 Mpeni Bwana utukufu wa jina lake :
Mwabuduni Bwana kwa uzuri mtakatifu.
- 3 Sauti ya Bwana juu ya maji :
Mungu mtukufu apiga radi, Bwana yu juu ya maji mengi.
- 4 Sauti ya Bwana ina nguvu :
Sauti ya Bwana ina enzi.
- 5 Sauti ya Bwana huivunja mierezi :
Bwana huivunjavunja mierezi ya Lebanon.
- 6 Huirusharusha kama ndama ya ng'ombe :
Lebanon na Sirion kama mwana nyati.
- 7 Sauti ya Bwana :
Huzipasua ndimi za moto.
- 8 Sauti ya Bwana hulitetemesha jangwa :
Bwana hulitetemesha jangwa la Kadeshi.
- 9 Sauti ya Bwana huwazalisha ayala, hufyeka misitu
Na hekaluni mwake kila aliomo hunena, Utukufu.
- 10 Bwana alikaa juu ya gharika :
Bwana anakaa akimiliki milele.
- 11 Bwana atawapa watu wake nguvu :
Bwana atawabariki watu wake kwa amani.

ZABURI YA THELATHINI NA MBILI

- 1 Yu heri aliyesamehewa makosa :
Aliyesetiriwa dhambi.
- 2 Yu heri mwana Adamu, Bwana asiyemhesabia hatia :
Rohoni mwake hamna hila.
- 3 Niliponyamaa mifupa yangu ilichakaa :
Kwa kuugua mchana kuchwa.
- 4 Kwani mchana na usiku mkono wako ulikuwa mzito kwangu :
Jasho langu likageuka kuwa kama hari wakati wa kaskazi.

- 5 Nalikufunulia dhambi yangu, wala sikuficha hatia yangu :
Nalisema, nitakiri makosa yangu kwa Bwana :
ukasamehe hatia ya dhambi yangu.
- 6 Kwa hiyo kila mtu mwema akuombe wakati unapatikana :
Hakika maji mengi yafurikapo hayatamfikia.
- 7 Ndiwe mahali pangu pa kujificha ; utanihifadhi :
Utanizungusha nyinbo za wokofu.
- 8 Nitakufundisha, nitakuonyesha njia utakayoiondea :
Nitakupa shauri, jicho langu likikutazama.
- 9 Msiwe kama frasi au nyumbu, wasio na akili :
Matandiko yao lijamu na hatamu kwa kuwazuia,
au hawatakuja kwako.
- 10 Mtu mwovu ana huzuni nyingi.
Amwaminiye Bwana, rehema zitamzunguka.
- 11 Mfurahieni Bwana mkashangilie, watu wa haki :
Pigeni vigelegele vya furaha, ninyi nyote wenye moyo
wa adili.

ZABURI YA THELATHINI NA NNE

- 1 NITAMTUKUZA Bwana wakati wote :
Sifa zake kinywani mwangu daima.
- 2 Roho yangu itajisifia Bwana :
Wenye upole watasikia, watafurahi.
- 3 Mtukuzeni Bwana pamoja nami :
Tuadhimishe jina lake sote.
- 4 Nalimtafuta Bwana akanijibu :
Akaniponya katika hofu zangu zote.
- 5 Walimtazama wakatiwa nuru :
Wala nyuso zao hazitaona haya.
- 6 Maskini huyu alilia, Bwana akasikia :
Akamwoko na taabu zake zote.
- 7 Malaika wa Bwana huwalinda wamwogopao :
Huwaopoa.
- 8 Onjeni mwone ya kuwa Bwana ni mwema :
Yu heri mtu anaemtumainia.

- 9 Mwogopeni Bwana, watakatifu wake :
Kwani wamwogopao hawahitaji kitu.
- 10 Wana simba huzidiwa, huona njaa :
Wamtafuta Bwana hawahitaji kitu cho chote kilicho
chema.
- 11 Njoni, wana, mnisikilize :
Nitawafundisheni kicho cha Bwana.
- 12 Mtu yupi atakae uzima :
Apendae siku nyingi, aone mema ?
- 13 Uzuie ulimi wako na mabaya :
Na midomo yako isinene hila.
- 14 Ujitenge na mabaya, ukatende mema :
Utafute amani, ukaifuata.
- 15 Macho ya Bwana juu yao wenye haki :
Na masikio yake kwa kilio chao.
- 16 Uso wa Bwana juu yao watendao mabaya :
Aondoe kumbukumbu lao duniani.
- 17 Walilia, Bwana akasikia :
Akawaponya katika taabu zao zote.
- 18 Bwana yu karibu yao wenye moyo uliovunjika :
Wenye roho iliyopondeka huwaokoa.
- 19 Mateso yake mwenye haki mengi :
Bwana humponya katika yote.
- 20 Humhifadhi mifupa yake yote :
Usivunjike hata mmoja.
- 21 Ubaya utamwua mwovu :
Wamchukiao mwenye haki watahukumiwa.
- 22 Bwana hukombo roho za watumwa wake :
Wala hakuna mtu amwaminiye ataka hukumiwa.

ZABURI YA ARUBAINI NA SITA

- 1 MUNGU ni kimbilio na nguvu zetu :
Msaada ulio karibu sana wakati wa shida.
- 2 Ijapo inchi igeuke hatutaogopa :
Ijapo milima iteteme moyoni mwa bahari.
- 3 Ijapo maji yake yavume na kuchafuka :
Ijapo milima ipepesuke kwa kiburi chake.

- 4 Pana mto, maji yake yaufurahisha mji wa Mungu :
Mahali patakatifu pa masikani zake Aliye Juu.
- 5 Mungu yu katikati yake ; hautaondoshwa :
Mungu atausaidia asubuhi na mapema.
- 6 Mataifa yalighadhabika, falme zikataharuki :
Alitoa sauti, inchi ikayeyuka.
- 7 Bwana wa majeshi yuko kwetu :
Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.
- 8 Njoni, tazameni matendo ya Bwana :
Ukiwa alioufanya kati ya inchi.
- 9 Akomesha vita hatta mwisho wa inchi :
Auvunja upinde, aukata mkuki, ayateketeza magari
katika moto.
- 10 Nyamaeni, jueni ya kuwa mimi ni Mungu :
Nitatukuka katika mataifa, nitatukuka kati ya inchi.
- 11 Bwana wa majeshi yuko kwetu :
Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.

ZABURI YA ARUBAINI NA SABA

- 1 WATU wote, pigeni makofi :
Mpigieni kelele Mungu kwa sauti ya shangwe.
- 2 Kwani Bwana Aliye Juu mwenye kuogofya :
Mfalme mkuu juu ya dunia yote.
- 3 Atawatiisha watu chini yetu :
Na mataifa chini ya miguu yetu.
- 4 Atatuchagua urithi wetu :
Fahari ya Yakobo, aliyempenda.
- 5 Mungu amepaa kwa kelele za shangwe :
Bwana kwa sauti ya panda.
- 6 Mwimbieni Mungu, imbeni :
Mwimbieni mfalme wetu, imbeni.
- 7 Kwani Mungu ndiye mfalme wa dunia yote :
Imbeni kwa akili.
- 8 Mungu awamiliki mataifa :
Mungu amekaa kitini mwa utakatifu wake.
- 9 Wakuu wa watu wamekusanyika wawe watu wa
Mungu wake Ibrahimu :
Kwani ngao za dunia ni zake Mungu : ametukuka sana.

ZABURI YA ARUBAINI NA NANE

- 1 BWANA ni mkuu, mwenye kusifiwa sana :
Mjini mwa Mungu wetu, mlimani mwa utakatifu
wake.
- 2 Umeinuliwa kwa uzuri, furaha ya dunia yote pia :
Mlima Sayuni, pande za kaskazini, mji wa Mfalme
mkuu.
- 3 Mungu majumbani mwake :
Amejijulisha kuwa ngome.
- 4 Kwani, tazama, wafalme walikusanyika :
Wakapita pamoja.
- 5 Wakaona, wakashangaa :
Wakafadhaika, wakaenda zao kwa haraka.
- 6 Wakashikwa palepale na tetemeko :
Utungu kama wa mwanamke azaae.
- 7 Kwa pepo za mashariki :
Wavunja jahazi za Tarashishi.
- 8 Kama tulivyosikia, ndivyo tulivyoona :
Mjini mwa Bwana wa majeshi, mjini mwa
Mungu wetu : Mungu ataufanya imara milele.
- 9 Tumeutafakari wema wako, Mungu :
Kati ya hekalu lako.
- 10 Kama lilivyo jina lako, Mungu, ndivyo na sifa zako
hata pembe za dunia :
Mkono wako wa kuume umejaa haki.
- 11 Mlima Sayuni ufurahi :
Binti za Yuda washangilie, kwa sababu ya hukumu
zako.
- 12 Tembeeni katika Sayuni, uzungukeni :
Hesabuni minara yake.
- 13 Tieni moyoni boma yake, yatafakari majumba
yake :
Mpate kuwaambia kizazi cha baada.
- 14 Kwani Mungu huyu ndiye Mungu wetu milele na
milele :
Atatuchunga yeye hata kufa.

ZABURI YA HAMSINI NA MOJA

- 1 UNIREHEMU, Mungu, kwa jinsi ulivyo mwema :
Rehema zako zilivyo kuu, ufute makosa yangu.
- 2 Unioshe na hatiya yangu :
Unitakase dhambi zangu.
- 3 Kwani nayajua makosa yangu mimi mwenyewe :
Na dhambi yangu iko mbele yangu daima.
- 4 Nimekutendea dhambi wewe, wewe peke yako, na
kutenda yaliyo mabaya machoni pako :
Uwe na haki unenapo, uwe safi utoapo hukumu.
- 5 Mimi naliumbwa hatiani :
Dhambini mama yangu alinichukua mimba.
- 6 Nawe wapendezwa na kweli ya ndani :
Sirini utanijulisha hekima.
- 7 Unisafishe kwa husopo, nami nitakuwa safi :
Unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko thuluji.
- 8 Unisikize kufurahi na shangwe :
Mifupa uliyoiponda istarehe.
- 9 Ufiche uso wako, usitazame dhambi zangu :
Ufute hatia zangu zote.
- 10 Uniumbie moyo safi, Mungu :
Ufanye ndani yangu roho thabiti.
- 11 Usiniondoe usoni pako :
Usiniondolee Roho yako takatifu.
- 12 Unirudishie furaha ya wokofu wako :
Unitegemeze kwa Roho yako bora.
- 13 Nitawafundisha wakosao njia zako :
Na wenye dhambi watakurudia.
- 14 Uniponye na kumwaga damu, Mungu, Mungu wa
wokofu wangu :
Na ulimi wangu utaimba haki yako.
- 15 Bwana, ufunue midomo yangu :
Na kinywa changu kitatangaza sifa zako.
- 16 Kwani hupendi dhabihu ; ningeitoa :
Wala hupendezwi na kafara.
- 17 Dhabihu za Mungu, ndio roho iliyovunjika :
Moyo uliovunjika, uliopondeka, Mungu, huta-
udharau.

- 18 Uitendee mema Sayuni :
Uzijenge kuta za Yerusalemi.
- 19 Ndipo utakapopenda sadaka za haki, dhabihu, na
kafara :
Ndipo watatoa ng'ombe madhbahuni pako.

ZABURI YA SITINI NA TATU

- 1 MUNGU, ndiwe Mungu wangu ; nitakutafuta
mapema :
Roho yangu yaona kiu kwako, nyama yangu yaku-
tamani, kwenye inchi kavu na kame isiyo maji.
- 2 Hivyo ndivyo nilivyokuona katika patakatifu :
Nitazame nguvu zako na utukufu wako.
- 3 Kwani huruma zako bora kuliko uzima :
Midomo yangu itakusifu.
- 4 Bassi, nitakubariki nikiwa hayi :
Kwa jina lako nitainua mikono yangu.
- 5 Roho yangu itashiba kama kwa mafuta na unono :
Kinywa changu kitakusifu kwa midomo ya furaha ;
- 6 Nikikukumbuka kitandani mwangu :
Nikikutafakari wakati wa makesha ya usiku.
- 7 Kwani wewe ndiwe uliyekuwa msaada wangu :
Na uvulini mwa mbawa zako nitafurahi.
- 8 Roho yangu inaambatana nawe :
Mkono wako wa kuume wanitegemeza.
- 9 Nao wanitafutao roho ili waiharibu :
Wataingia pande za chini za inchi.
- 10 Watatiwa katika nguvu za upanga :
Watakuwa sehemu ya mbwa za mwitu.
- 11 Nae mfalme atamfurahia Mungu :
Killa amwapiae atashangilia, kwani kinywa chao
wasemao uwongo kitafumbwa.

ZABURI YA THEMANINI NA NNE

- 1 MASIKANI zako zapendeza mno :
Bwana wa majeshi.
- 2 Roho yangu yazitamani, yazionea shauku nyua za
Bwana :

- Moyo wangu na kiwiliwili changu vyampigia kelele
Mungu aliye hayi.
- 3 Ndege amepata nyumba, na mbayuwayu kitagio
cha kuwekea makinda yake :
Madhbahu zako, Bwana wa majeshi, Mfalme wangu
na Mungu wangu.
- 4 Wa heri wakaao nyumbani mwako :
Watakuwa wakikusifu daima.
- 5 Wa heri watu wenye nguvu kwako :
Na njia za Sayuni mioyoni mwao.
- 6 Wakipita kati ya bonde la Vilio, hulifanya chem-
chemi :
Naam, mvua ya vuli hulijaza baraka.
- 7 Huendelea toka nguvu hata nguvu :
Huonekana Sayuni mbele ya Mungu kila mmoja
wao.
- 8 Bwana Mungu wa majeshi, unisikie niombapo :
Usikilize, Mungu wa Yakobo.
- 9 Uangalie, Mungu, ngao yetu :
Umtazame uso masiha yako.
- 10 Kwani siku moja nyuani mwako yapita siku elfu :
Ningechagua kuwa bawabu katika nyumba ya
Mungu wangu, kuliko kukaa kitako hemani mwa
uovu.
- 11 Kwani Bwana Mungu ni jua na ngao, Bwana atatoa
neema na utukufu :
Hatawanyima neno jema waendao kwa ukamilifu.
- 12 Bwana wa majeshi :
Yu heri mtu anaekutumaini.

ZABURI YA TISAINI

- 1 BWANA, wewe ndiwe makao yetu :
Kizazi kwa kizazi.
- 2 Kabla ya kuzaliwa milima, au kuumbwa ulimwengu :
Tangu milele hata milele, ndiwe Mungu.
- 3 Wamrejeza mtu hata mavumbini :
Wasema, Rudini, wana Adamu.

- 4 Kwani miaka elfu machoni pako kama jana ikiisha :
Kama kesha la usiku.
- 5 Wawagharikisha, wamekuwa kama usingizi :
Assubuhi kama majani yaotayo :
- 6 Assubuhi yaota, yachanua :
Jioni yakatwa, yakauka.
- 7 Kwani tumekonda kwa hasira yako.
Twafadhaika kwa ghadhabu yako.
- 8 Umeziweka hatia zetu mbele yako :
Siri zetu katika mwanga wa uso wako.
- 9 Maana siku zetu zote zimetoweka kwa uchungu wako :
Tumekwisha miaka yetu kama hadithi.
- 10 Siku za miaka yetu ni miaka sabaini, au aliye na
nguvu miaka themanini :
Lakini kiburi chao taabu na udhia tu, maana chapita
upes, nasi tumekwenda zetu.
- 11 Nani ajuae uwezo wa hasira yako :
Na ghadhabu zako kwa hofu ikupasayo ?
- 12 Utujulishe tuzihesabu hivi siku zetu :
Tupate kuwa na moyo wa hekima.
- 13 Urudi, Bwana, hata lini :
Uwahurumie watumwa wako.
- 14 Utushibishe asubuhi kwa rehema zako :
Nasi tutashangilia, na kufurahi siku zetu zote.
- 15 Utufariji kadiri ya siku ulizotutesa :
Miaka tuliyoona mabaya.
- 16 Matendo yako yaonekane kwa watumwa wako :
Na enzi yako kwa wana wao.
- 17 Na neema ya Bwana Mungu wetu iwe kwetu :
Kazi ya mikono yetu utufanikishie ; tena kazi ya
mikono yetu uifanikishe.

ZABURI YA TISAINI NA MOJA

- 1 AKAAE mahali pa siri pake Aliye Juu :
Atakaa uvulini mwake Mwenyiezi.
- 2 Nitamnena Bwana, Yeye ndiye kimbilio langu na
ngome yangu :
Mungu wangu ninaemtumainia.

- 3 Kwani atakuponya na tego la mwindaji :
Na tauni ya uharibifu.
- 4 Kwa manyoya yake atakufunika, chini ya mbawa
zake utaona hamaya :
Kweli yake ni ngao na kigao.
- 5 Hutaogopa kwa hofu za usiku :
Wala mshale uendao mchana.
- 6 Wala tauni ipitayo gizani :
Wala uweli ufishao adhdhuuri.
- 7 Elfu wataanguka ubavuni pako, na elfu kumi mkono
wako wa kuume :
Hautakufikia wewe.
- 8 Ila kwa macho yako utatazama :
Utaiona ijara ya waovu.
- 9 Kwani ndiwe, Bwana, uliye tumaini langu :
Aliye juu umemfanya kuwa makao yako ;
- 10 Mabaya hayatakupata :
Wala tauni haitakaribia hema yako.
- 11 Kwani atakuagizia malaika zake :
Wakulinde katika njia zako zote.
- 12 Watakuchukua juu mikononi :
Usijikwae mguu jiwani.
- 13 Juu ya simba na nyoka utakwenda :
Utawakanyaga mwana simba na joka.
- 14 Kwa kuwa amenipendelea, nitamwoko :
Nitamweka juu, kwa kuwa amenijua jina.
- 15 Ataniita, nami, nitamwitikia :
Nitakuwapo nae kwenye taabu ; nitamwoko,
nitamtukuza.
- 16 Kwa siku nyingi nitamshibisha :
Nitamwonyesha wokofu wangu.

ZABURI YA TISAINI NA TATU

- 1 BWANA anamiliki ; amevaa enzi ; amevaa Bwana,
amevaa nguvu kama mshipi :
Nao ulimwengu umewekwa usitikisike.
- 2 Kiti chake kimewekwa tangu zamani :
Wewe ndiwe wa milele.

- 3 Mito imepaaza, Bwana, mito imepaaza sauti zao :
Mito imepaaza uvumi wao.
- 4 Kuliko sauti za maji mengi, kuliko mawimbi makuu
ya bahari :
Bwana aliye juu ndiye mkuu.
- 5 Shuhuda zako amini sana, utakatifu ni pambo la
nyumba yako :
Bwana, milele na milele.

ZABURI YA TISAINI NA SITA

- 1 MWIMBIENI Bwana uimbo mpya :
Mwimbieni Bwana, inchi yote.
- 2 Mwimbieni Bwana, litukuzeni jina lake :
Uhubirini wokofu wake kila siku.
- 3 Utangazeni utukufu wake kwa mataifa :
Maajabu yake kwa watu wote.
- 4 Kwani Bwana ni mkuu mwenye kusifiwa sana :
Mwenye kuogopwa yeye kuliko miungu yote.
- 5 Kwani miungu yote ya watu si kitu :
Lakini Bwana aliyezifanya mbingu.
- 6 Heshima na enzi zipo mbele yake :
Nguvu na uzuri zimo ndani ya patakatifu pake.
- 7 Mpeni Bwana, jamaa za watu :
Mpeni Bwana utukufu na nguvu.
- 8 Mpeni Bwana utukufu wa jina lake :
Leteni sakaka, ingieni nyuani mwake.
- 9 Mwabuduni Bwana kwa uzuri wa utakatifu :
Tetemekeni mbele yake, dunia yote.
- 10 Semeni na mataifa, Bwana anamiliki :
Ulimwengu umewekwa, usitikisike, atawahukumu
watu kwa haki.
- 11 Mbingu zifurahi, inchi ishangilie :
Bahari ivume na vyote vilivyomo.
- 12 Shamba lipige shangwe, na vyote vilivyomo :
Ndipo na miti yote ya mwituni itaimba furaha.
- 13 Mbele zake Bwana, kwani anakuja ; kwani anakuja
aihukumu inchi :
Atauhukumu ulimwengu kwa haki, na watu kwa
uaminifu wake.

ZABURI YA TISAINI NA NANE

- 1 MWIMBIENI Bwana uimbo mpya, kwani ametenda miujiza :
Mkono wake mtakatifu, mkono wake wa kuume umempatia wokofu.
- 2 Bwana amehubiri wokofu wake :
Amewadhahirishia mataifa haki yake.
- 3 Amezikumbuka rehema zake na uaminifu wake kwa Waisraeli :
Pembe zote za inchi zimeuona wokofu wa Mungu wetu.
- 4 Mshangilieni Bwana, dunia yote :
Imbeni, furahini, shukuruni.
- 5 Mshukuruni Bwana kwa kinubi :
Kwa kinubi mkiimba zaburi.
- 6 Kwa panda na sauti ya baragumu :
Shangilieni mbele za Bwana, mfalme.
- 7 Bahari ivume na vyote vilivyomo :
Ulimwengu nao wakaao.
- 8 Mito ipige makofi :
Milima ipalize sauti za furaha.
- 9 Mbele za Bwana, kwani anakuja aihukumu inchi :
Atauhukumu ulimwengu kwa haki, na watu ilivyo sawa.

ZABURI YA MIA NA TATU

- 1 UMTUKUZE Bwana, roho yangu :
Na vyote vilivyomo mwangu, lisifuni jina lake takatifu.
- 2 Umtukuze Bwana, roho yangu :
Wala usizisahau fadhili zake zote.
- 3 Anaesamehe hatia zako zote :
Aponyae udhaifu wako wote ;
- 4 Akomboae maisha yako katika uharibifu :
Akutiae taji ya rehema na huruma.
- 5 Akushibishae kinywa chako kwa mema :
Ujana wako unarudi kuwa kama tai.

- 6 Bwana ndiye afanyae mambo ya haki :
Na hukumu kwa watu wote wanaoonewa.
- 7 Alimjulisha Musa njia zake :
Wana wa Israeli matendo yake.
- 8 Bwana ndiye mwenye huruma na neema :
Asiyeona hasira upesi, na mwingi wa rehema.
- 9 Hatateta na sisi siku zote :
Wala hatashika hasira yake milele.
- 10 Hakututendea kwa dhambi zetu :
Wala hakutulipa kwa hatia zetu.
- 11 Kwa maana mbingu kadiri zilivyo juu ya inchi :
Vivyo na rehema zake zi nyingi kwao wamwogopao.
- 12 Mashariki yalivyo mbali ya Magharibi :
Vivyo na dhambi zetu ameziweka mbali yetu.
- 13 Baba awahurumiavyo watoto wake :
Ndivyo Bwana anavyohurumia wamwogopao.
- 14 Kwa kuwa atujua umbo letu :
Akikumbuka tulivyo mavumbi tu.
- 15 Mwana Adamu siku zake zi kama majani :
Kama ua la shambani ndivyo asitawivyo.
- 16 Kwani upepo wapita juu yake nalo latoweka :
Na mahali pake hapalijui tena.
- 17 Na rehema za Bwana zi kwao wamchao tangu milele hata milele :
Na haki yake kwa wana wa wana ;
- 18 Kwa watu wayashikao maagano yake :
Wazikumbukao amri zake ili wazitende.
- 19 Bwana ameweka kiti chake mbinguni :
Enzi yake yatawala juu ya vyote.
- 20 Mtukuzeni Bwana, malaika zake, wenye nguvu nyingi, mtendao neno lake :
Msikilizao sauti ya neno lake.
- 21 Mtukuzeni Bwana majeshi yake yote :
Wahudumu wake, wafanyao mapenzi yake.
- 22 Mtukuzeni Bwana, matendo yake yote, mahali pote pa milki yake :
Umtukuze Bwana roho yangu.

ZABURI YA MIA NA EDASHARA

- 1 MSIFUNI Bwana. Nitamshukuru Bwana kwa moyo wangu wote :
Katika baraza ya wenye adili na katika makutano.
- 2 Matendo ya Bwana ni makuu :
Yanatafutwa na watu wote wayapendao.
- 3 Kazi yake fahari na uzuri :
Na haki yake yakaa daima.
- 4 Amefanya kumbukumbu la miujiza yake :
Bwana yu mwenye rehema na neema.
- 5 Amewapa chakula wamwogopao :
Atayakumbuka maagano yake milele.
- 6 Amewajulisha watu wake uwezo wa matendo yake :
Kwa kuwapa urithi wa mataifa.
- 7 Kazi za mikono yake kweli na hukumu :
Maagizo yake yote amini.
- 8 Yamefanywa imara daima na milele :
Yametendwa kwa kweli na adili.
- 9 Amewapelekea watu wake ukombozi ; ameamuru maagano yake milele :
Jina lake ni takatifu, lenye hofu.
- 10 Kumcha Bwana, mwanzo wa hekima :
Wenye akili ndio wayatendao haya ; sifa zake zakaa daima.

ZABURI YA MIA NA THENASHARA

- 1 MSIFUNI Bwana :
Yu heri mtu amwogopae Bwana, ayapendae sana maagizo yake.
- 2 Wazao wake watakuwa hodari duniani :
Kizazi cha wenye adili kitabarikiwa.
- 3 Utajiri na mali nyumbani mwake :
Haki yake yakaa daima.
- 4 Nuru huchomoza gizani kwa watu wenye adili :
Ndiye mwenye neema, na rehema, na haki.
- 5 Yu heri atendae kwa neema na kukopesha :
Athubutisha neno lake hukumuni.

- 6 Kwani hataondoshwa milele :
Mtu wa haki atakumbukwa daima.
- 7 Hataogopa kwa habari mbaya :
Moyo wake u thabiti, ukimwamini BWANA.
- 8 Moyo wake u imara, hataona hofu :
Mpaka atimize shauku yake kwa adui zake.
- 9 Amegawanya, amewapa fukara, haki yake yakaa daima :
Enzi yake itainuka kwa utukufu.
- 10 Mtu mbaya ataona, atasikitika ; atasaga meno, atayeyuka :
Tamaa ya wabaya itapotea.

ZABURI YA MIA NA TISATASHARA

- 1 WA heri walio kamili kwa mwendo wao :
Waendao katika sharia ya Bwana.
 - 2 Wa heri washikao shuhuda zake :
Wamtafutao kwa mioyo yao yote.
 - 3 Wala hawatendi mapotofu :
Waenda katika njia zake.
 - 4 Umeyaamuru mausia yako :
Tuyashike sana.
 - 5 Njia zangu zithubutike :
Nizishike amri zako !
 - 6 Ndipo sitaona haya :
Nikiyaangalia maagizo yako yote.
 - 7 Nitakushukuru kwa moyo wa adili :
Nikijifunza hukumu zako za haki.
 - 8 Nitazishika amri zako :
Usiniache kabisa.
-
- 9 Kijana aisafisheje njia yake :
Kwa kuangalia, akifuata neno lako.
 - 10 Kwa moyo wangu wote nimekutafuta :
Nisipotee katika maagizo yako.

- 11 Moyoni mwangu nimeiweka amri yako :
Nisikufanyie dhambi.
- 12 Umetukuzwa, Bwana :
Unifundishe amri zako.
- 13 Kwa midomo yangu nimezihubiri :
Hukumu zote za kinywa chako.
- 14 Nimefurahia njia ya shuhuda zako :
Kama ingekuwa jamii ya mali.
- 15 Nitayatafakari mausia yako :
Nitaziangalia njia zako.
- 16 Nitajifurahisha kwa amri zako :
Sitalisahau neno lako.
- 33 Unijulishe, Bwana, njia ya amri zako :
Nami nitaishika hata mwisho.
- 34 Unipe akili, nami nitaishika sharia yako :
Nitaiangalia kwa moyo wote.
- 35 Unienendeshe katika mapito ya maagizo yako :
Kwani ndiyo yanifurahishayo.
- 36 Uelekeze moyo wangu kwa shuhuda zako :
Wala si kwa choyo.
- 37 Unigeuze macho nisyatazame yasiyofaa :
Unifufue katika njia yako.
- 38 Umthubutishie mtumwa wako usia lako :
Linalohusu kicho chako.
- 39 Uniondolee mbali laumu niogopayo :
Kwani hukumu zako njema.
- 40 Tazama, nimeyatamani mausia yako :
Unifufue kwa haki yako.
-
- 105 Neno lako ni taa kwa miguu yangu :
Na mwanga nipitapo.
- 106 Nimeapa na kukusudia sana :
Nizishike hukumu za haki yako.
- 107 Nimeteswa mno :
Unifufue, Bwana, kwa neno lako.
- 108 Ukubali Bwana, nakuomba, sadaka za kinywa
changu :
Unifundishe hukumu zako.

- 109 Roho yangu daima mikononi mwangu :
Nami siisahau sharia yako.
- 110 Waovu wameniwekea mtego :
Nami sikuyahalifu mausia yako.
- 111 Shuhuda zako nimezitwaa kuwa urithi wa milele :
Kwani ndiyo furaha ya moyo wangu.
- 112 Nimeelekeza moyo wangu nizitende amri zako :
Daima hata milele.
-
- 137 Wewe ndiwe mwenye haki, Bwana :
Na hukumu zako za adili.
- 138 Kwa haki umeagiza shuhuda zako :
Na kwa uaminifu mwingi.
- 139 Jitihadi yangu imeniangamiza :
Kwa sababu watesi wangu wameyasahau maneno
yako.
- 140 Usia lako limesafika sana :
Mtumwa wako alipenda.
- 141 Mimi mdogo wala sina heshima :
Siyasahau mausia yako.
- 142 Haki yako haki ya milele :
Na sharia yako kweli.
- 143 Shida na taabu zimenipata :
Maagizo yako ni furaha zangu.
- 144 Shuhuda zako za haki milele :
Unipe akili, nami nitaishi.

ZABURI YA MIA NA ISHIRINI NA MOJA

- 1 NITAINUA macho yangu milimani :
Msaada wangu utatoka wapi ?
- 2 Msaada wangu kwa Bwana :
Aliyezifanya mbingu na inchi.
- 3 Hatauacha mguu wako uteleze :
Hatalala akulindae.
- 4 Angalia, hatasinzia wala hatalala :
Amlindae Israeli.
- 5 Bwana mlinzi wako :
Bwana uvuli wa mkono wako wa kuume.

- 6 Jua halitakupiga mchana :
Wala mwezi usiku.
- 7 Bwana atakulinda na mabaya yote :
Atakulinda roho.
- 8 Bwana atakulinda utokapo na uingiapo :
Tangu sasa hata milele.

ZABURI YA MIA NA ISHIRINI NA MBILI

- 1 NALIFURAHUWA waliponiambia :
Twende nyumbani kwa Bwana.
- 2 Miguu yetu inasimama :
Milangoni mwako, Yerusalemi.
- 3 Yerusalemi, uliojengwa :
Kama mji ulioshikamana.
- 4 Huko ndiko wapandako makabila, makabila ya
Israeli :
Amri kwa Israeli, walishukuru jina la Bwana.
- 5 Kwani humo vimewekwa viti vya hukumu :
Viti vya nyumba ya Daud.
- 6 Iombeeni amani Yerusalemi :
Watafanikiwa wakupendao.
- 7 Amani iwe kutani mwako :
Kufanikiwa majumbani mwako.
- 8 Kwa ajili ya ndugu zangu na wenzangu :
Nitasema sasa, Amani kwako.
- 9 Kwa ajili ya nyumba ya Bwana Mungu wetu :
Nitakutakia mema.

ZABURI YA MIA NA ISHIRINI NA NANE

- 1 YU heri kila amwogopae Bwana :
Aendae kwa njia zake.
- 2 Kwani utazila kazi za mikono yako :
U heri, tena kwema kwako.
- 3 Mkewo kama mzabibu uzaao, ndani ya nyumba
yako :
Wanawo kama miche ya mzeituni, wakizunguka
meza yako.

- 4 Tazama ndivyo atakavyobarikiwa mtu :
Amwogopae Bwana.
- 5 Nawe atakubariki toka Sayuni :
Utayaona mema ya Yerusalemi siku zote za maisha
yako.
- 6 Hata utawaona wana wa wanao :
Amani kwa Israeli.

ZABURI YA MIA NA THELATHINI

- 1 TOKA vilindini :
Nimekulilia, Bwana.
- 2 Bwana, usikie sauti yangu :
Masikio yako yasikilize sauti ya dua zangu.
- 3 Kama ungehesabu hatia, Bwana :
Nani angesimama, Bwana ?
- 4 Lakini kwako samaha :
Ili uogopwe.
- 5 Namngoja Bwana, roho yangu inangoja :
Na neno lake nalitumainia.
- 6 Roho yangu yamtazamia Bwana kuliko walinzi
watazamiavyo :
Wakiitazamia asubuhi.
- 7 Israeli, umtumaini Bwana :
Kwa maana Bwana anazo rehema, anao na ukombozi
mwingi.
- 8 Nae atamkomboa Israeli :
Katika hatia zake zote.

ZABURI YA MIA NA THELATHINI NA TATU

- 1 JINSI ilivyo vema na kupendeza :
Ndugu wakae pamoja, wakipatana !
- 2 Ni kama mafuta, mazuri kichwani, yaliyoshuka
mpaka ndevuni :
Ndevu za Haruni ; yaliyoshuka mpaka upindo wa
mavazi yake.
- 3 Ni kama umande wa Hermani, ushukao juu ya milima
ya Sayuni :
Kwani ndipo Bwana alipoiamuru baraka, naam,
uzima hatta milele.

ZABURI YA MIA NA ARUBAINI NA TANO

- 1 NITAKUTUKUZA, Mungu wangu, mfalme :
Nitalihimidi jina lako milele na milele.
- 2 Killa siku nitakutukuza :
Nitalisifu jina lako milele na milele.
- 3 Bwana ni mkuu, mwenye kusifiwa sana :
Na ukuu wake hautafutikani.
- 4 Kizazi kwa kizazi kitayasifu matendo yako :
Kitayaeneza matendo yako makuu.
- 5 Nitautafakari uzuri wa utukufu wa enzi yako :
Na mambo yako ya ajabu.
- 6 Watu wayaadhimisha matendo yako ya hofu :
Nitauhubiri ukuu wako.
- 7 Watatangaza kumbukumbu la wema wako mwingi :
Wataimba haki yako.
- 8 Bwana mwenye rehema na mwingi wa huruma :
Si mwepesi wa hasira na mwingi wa rehema.
- 9 Bwana yu mwema kwa wote :
Na huruma zake juu ya kazi zake zote.
- 10 Kazi zako zote zitakushukuru, Bwana :
Na watakatifu wako wakutukuza.
- 11 Waunena utukufu wa ufalme wako :
Na kuzihadithia nguvu zako :
- 12 Wajulishe wana Adamu mambo yake makubwa :
Na utukufu wa uzuri wa ufalme wake.
- 13 Ufalme wako ufalme wa zamani zote :
Na mamlaka yako ya vizazi vyote.
- 14 Bwana huwategemeza wote waangukao :
Huwainua wote wainamiao.
- 15 Macho yao wote yakutazama wewe :
Nawe huwapa chakula chao majira yake.
- 16 Wafunua mkono wako :
Kila kilicho hayi wakishibisha upendeleo wako.
- 17 Bwana mwenye haki katika njia zake zote :
Na mwenye rehema katika kazi zake zote.
- 18 Bwana yu karibu nao wote wamwitao :
Wote wamwitao kwa kweli.

- 19 Atawafanyia uradhi wamwogopao :
Atawasikia tena waliapo, atawaokoa.
- 20 Bwana huwahifadhi wote wampendao :
Waovu wote atawaharibu.
- 21 Kinywa changu kitanena sifa za Bwana :
Wote wenye mwili walitukuze jina lake takatifu
milele na milele.

ZABURI YA MIA NA ARUBAINI NA SITA

- 1 MSIFUNI Bwana :
Roho yangu, umsifu Bwana.
- 2 Nitamsifu Bwana kadiri niishivyo :
Nitamsifu Mungu wangu nikiwa hayi.
- 3 Usiwatumainie wakuu :
Wala mwana Adamu, asiyeweza kuokoa.
- 4 Pumzi yake yatoka, arudia inchi yake :
Siku hiyo mashauri yake yapotea.
- 5 Yu heri aliye na Mungu wa Yakobo kuwa msaada
wake :
Anaemtumaini Bwana Mungu wake.
- 6 Aliyezifanya mbingu na inchi :
Bahari na vyote vilivyomo ; ashikae kweli milele.
- 7 Huwatendea hukumu walioonewa ; huwapa chakula
wenye njaa :

ZABURI MIA NA ARUBAINI NA NANE

- 1 HALELUYAH. Msifuni Bwana, mbinguni :
Msifuni toka juu.
- 2 Msifuni, malaika zote :
Msifuni, majeshi yake yote.
- 3 Msifuni, jua na mwezi :
Msifuni, nyota zote za mwanga.
- 4 Msifuni, mbingu za mbingu :
Na maji mlioko juu ya mbingu.
- 5 Yalisifu jina la Bwana :
Kwani aliamuru yakaumbwa.

- 6 Ameyaweka kwa maisha na milele :
Akatoa amri, nayo haipiti.
- 7 Msifuni Bwana, katika inchi :
Nyamgumi na vilindi vyote ;
- 8 Moto na mvua ya mawe, thuluji na mvuke :
Pepo za tufani, zilitendazo neno lake ;
- 9 Milima na vilima vyote :
Miti yenye matunda na mierezi yote ;
- 10 Nyama na ng'ombe zote :
Zitambaazo na ndege zenye mbawa ;
- 11 Wafalme wa dunia na watu wote :
Wakuu na makadhi wa dunia wote ;
- 12 Vijana waume na wana wali :
Wazee na watoto ;
- 13 Walisifu jina la Bwana ; kwani jina lake peke yake
limetukuka :
Enzi yake juu ya inchi na mbingu.
- 14 Nae ameinua nguvu za watu wake ; sifa za wataka-
tifu wake wote :
Za wana wa Israeli, watu walio karibu nae.
Halleluyah.

ZABURI YA MIA NA HAMSINI

- 1 HALELUYAH. Msifuni Mungu katika patakatifu
pake :
Msifuni katika nafasi ya uweza wake.
- 2 Msifuni kwa matendo yake makuu :
Msifuni kwa ukuu wake mwingi.
- 3 Msifuni kwa sauti ya baragumu :
Msifuni kwa kinanda na kinubi.
- 4 Msifuni kwa ngoma na kucheza :
Msifuni kwa kinanda chenye nyuzi na zomari.
- 5 Msifuni kwa matoazi yenye sauti kuu :
Msifuni kwa matoazi yavumayo sana.
- 6 Kila mwenye pumzi amsifu Bwana :
Halleluyah.

NYIMBO

DIBAJI

Nyimbo katika kitabu hiki zimetungwa kwa namna mbali ya desturi ya zamani.

Hasa mistari iliyo mingi ina silabi moja zaidi. K.m., wimbo ule, " Mwamba wangu wa kale " uliimbwa hivi :
Mwā-mba wā-ngu wā ka-lé."

Silabi zenye alama juu zilitamkwa kwa nguvu zaidi ya silabi nyingine. Lakini watu husema ká-le, siyo ka-lé, kwa hiyo tumeona vema kubadili nyimbo zote za namna hii, kwa kuongeza silabi moja ili tutamke katika kuimba kama tunavyotamka katika kusema. Kwa hiyo tumeandika wimbo ule hivi : " Mwā-mba ú-li-ó-pa-sú-ka." Hapo -su- ndiyo silabi ya mwisho katika kuimba, na -ka- itatamkwa kwa sauti ndogo isiyosikika sana. Tume-fanya vivyo katika nyimbo nyingi.

Tena nyimbo nyingine, au mistari mingine katika nyimbo, havina haja ya silabi moja saidi ya noti za tuni. K.m. 475 mistari ya 3 na 4.

Tumsifu tuwezavyo.

Aliye Mfulme wetu.

Mstari wa kwanza una silabi zake saba, za halali zote. Wa pili una saba vile vile, ila ya saba imeongezeka, si ya halali. Imewekwa ili kusaidia tuni, tena itamkwe kwa sauti ndogo.

Pengine tuni za Kiingereza na maneno ya Kiswahili havikubaliani hata kidogo, hata tulishindwa kufuata mfano ulio juu. K.m. 440 :

Yeye anichungaye 'mi
Ni mfalme wa upendo,
Sitapungukiwa kitu
Ningali nipo naye.

yaani silabi moja zaidi kwa mistari wa 2 na wa 4 tu. Tungalifuata desturi za kwanza, tungaliandika wimbo huu hivi :

Yeye anichungaye mimi

Ni mfalme wa upendo,
Sitapungukiwa kitu kweli.

Ningali nipo naye.

yaani silabi moja zaidi kwa kila mstari. Lakini katika mstari wa kwanza na wa tatu, tumeandika silabi za halali, maana katika kuimba hakuna kituo hata kidogo baada ya *mi* na baada ya *kitu*. Kweli tungeweza kuandika hivi :

Yeye anichungaye mi, ni mfalme wa upendo,

Sitapungukiwa kitu ningali nipo naye.

yaani mistari miwili tu.

Hasa tumetaka maneno kama haya : Mdhamini, akampa, mbinguni, mbali, mfalme, yaandikwe kwa silabi chache hivi : Mdha-mi-ni, 3, sivyo m-dha-mi-ni, 4 ; Mbi-ngu-ni, 3, sivyo m-bi-ngu-ni, 4, n.k. Pengine tume-shindwa kufanya hivi, k.m. Wimbo 453, shairi la mwisho tumeandika M-chu-nga-ji, badala ya Mchu-nga-ji.

Maneno kama mtu, mji, yaliyo mafupi, tumeandika silabi mbili hivi : m-tu, m-ji. Taz. wimbo 434 " Njoni faragha mpumzike kwangu ". Maneno haya : Mji-tengeni, msishirikiane, lazima tutamke hivi : m-ji-te-nge-ni, m-si-shi-ri-ki-a-ne, n.k., maana *m* inahusu *myi*. Nukta mbili juu ya herufi fulani yaonyesha kwamba lazima kuitamka kama silabi moja, yaani peke yake.

Vile vile mwimbaji aangalie maneno kama saa, neema, sauti, n.k., maana pengine, tukitaka silabi 3 twaimba ne-e-ma, na tukitaka silabi 2 twaimba nee-ma. Tukitaka silabi ziwe tatu maneno yataandikwa hasa hivi : neema, sauti, kukaä, n.k.

Twamshukuru Bwana Bishop wa Unguja aliyetupa ruhusa kutumia nyimbo nyinginezo katika kitabu cha U.M.C.A. Tena yafaa Waalimu watumie kitabu cha tuni cha U.M.C.A., maana humo zimeandikwa tuni zitakazohusu sana maneno ya nyimbo zilizomo katika kitabu hiki.

Nambari zilizofungwa hivi ndizo nambari katika kitabu cha C.M.S. Nairobi.

NYIMBO

NYIMBO ZA ASUBUHI

1 "Holy, Holy, Holy, Lord God Almighty." (1)

1 **M**TAKATIFU Wewe Mungu Mwenyezi
Kila tuamkapo tufike kuabudu ;
Mtakatifu Wewe wa huruma nyingi
Uhimidiwe Mungu wa Utatu.

2 Mtakatifu Wewe wakuaminio
Wakusujudia Wewe daima huko ;
Malaika wote wakuinamia
Uliye, tena utakayekuwa.

3 Mtakatifu Wewe watu wenye dhambi
Hawawezi kuona utukufu wako
Wewe peke yako Mtakatifu kweli
Upendo mwingi na uwezo mkuu.

4 Mtakatifu Wewe Mungu Mwenyezi
Uliyoviumba vyote vinakusifu
Mtakatifu Wewe wa huruma nyingi
U Mungu mmoja katika Utatu.

2 "New every morning is the love." (5)

H.C. 5. [L.M.]

1 **T**waona kila asubuhi,
Mapenzi yake Bwana wetu
Ametulinda saa za giza,
Tumeamka na afya njema.

- 2 Tunapoomba kila siku,
Rehema zake tunapewa,
Hatari zinatupitia
Tukimtumainia Yeye.
- 3 Tukimhimidi Mungu leo
Katika mwendo wa halisi,
Atatupatia hazina
Ya kutosha dhabihu zetu.
- 4 Kila kazi, kila kitendo
Kitatufaa kwa uhudumu
Tukijinyima duniani
Tutapata 'sogea Mungu.
- 5 Rafiki zetu wa zamani,
Tunawapenda kwa amani
Nayo mashaka yetu yote
Yatashindwa na pendo lake.
- 6 Bwana utufanye tayari
Kwako mbinguni tustarehe
Yesu utubariki leo
Na siku zetu zote hivyo.

3 "Forth in Thy Name, O Lord, I go." (11)

H.C. 16. [L.M.]

- 1 **K**WA Jina lako naondoka
Nifanye kazi yangu leo,
Nikuheshimu Mungu wangu
Kwa yote nitakayofanya.
- 2 Kazi ile uliyonipa
Nitaifanya kwa furaha,
Nifanye uyaamuruyo,
Nikutolee vyangu vyote.

- 3 Nataka uwe nami hivi
Uangalie zangu zote
Niyatendayo, niendapo
Nikuone u mbele yangu.
- 4 Unifungie nira yako
Nikeshe na kuomba sana
Nitazamie ya mbinguni,
Hata utakaporejea.
- 5 Nifanye kazi kwa bidii,
Kadiri ulivyowezesha,
Nikufuate kwa furaha
Hata nifike kwako juu.

NYIMBO ZA JIONI

4 "Father, again in Jesus' name we meet." (16)

H.C. 99. [108.]

- 1 **E**Machoni pako kwa jina la Mwana ;
Saüti zetu twakuinulia,
Tunaomba tukikusujudia.
- 2 Twakushukuru kwa ulinzi wako,
Matendo yako tungeyatangaza
Je ! siku zetu hazijai wema ?
Tena waepukisha dhara mbali.
- 3 Hatustahili pendo kama hilo,
Tumeziacha mbali njia zako.
Sasa twataka rudi, twasikia
Ukituita nyumbani kwako.
- 4 Kwa jina hilo la uwezo wote
Kwa pendo lipitalo pendo lote,
Kwa damu Yesu aliyoimwaga,
Fungua lango ili tuingie.

5 "One sweetly solemn thought." (22)

S.S. AND S. 987. H.C. 35. [6S.]

1 **F**IKIRA moja bora,
Imo moyoni mwangu,
Nimekukaribia
Kuliko ya zamani.

2 Karibu na majumba
Ya Baba yangu juu,
Karibu na enzio,
Karibu na Mwenyewe.

3 Karibu na wakati
Wa mapumziko yangu,
Na nitakapotua
Mizigo ya dunia.

4 Karibu pata taji,
Niliyoahidiwa ;
Yesu unifikishe
Salama kwako juu.

6 "The sun is sinking fast." (23)

H.C. 26. [6.4.6.6.]

1 **J**UA lakwisha shuka
Giza karibu ;
Na tutoe sadaka
Wajibu wa jioni.

2 Alivyonena Yesu,
Mwenye msalaba,
"Baba natoa roho
Iende kwako sasa."

3 Hivi na sisi sote
Watoto wako,
Twakuwekea roho
Ewe Mwokozi wetu.

4 Hivyo napenda ishi
Kwa nguvu zake,
Akiwa ndani yangu,
Aniongoze vema.

5 Na tusikusudie
Mapenzi yetu ;
Ila yake ambaye
Ametufia sisi.

7 "Now the day is over." (24)

H.C. 469. [6S.5.]

1 **S**ASA kumekuchwa
Siku imekwisha,
Punde hivi mbingu
Zitatiwa giza.

2 Nyota zimetoka
Na zinamulika,
Viumbe vyake Mungu
Vinaanza tua.

3 Yesu wapumzishe
Waliolemewa,
Ili wastarehe
Wakikuhimidi.

4 "Tolee watoto
Ndoto zako njema,
Linda wasafiri
Duniani pote.

- 5 Ufariji wote
Wanaougua,
Zuia wabaya
Na uovu wao.
- 6 Malaika wako
Utupelekee
Vitandani kwetu
Ili watutunze.
- 7 Tutakapoamka
Hivyo tutatoka
Kwa usafi kweli
Tukutumikie.

8 "Saviour, breathe an evening blessing." (25)

C. AND F. 373. [8s. 7s.]

- 1 **M**WOKOZI utuletee
Baraka yako jioni;
Dhambi zetu twazikiri,
Utusamehe zote.
- 2 Dhambi zikituzunguka
Pote tumo hatarini,
Malaika wa mbinguni
Wafike watutunze.
- 3 Giza haituogofyi
Ungali uko karibu,
Ndiwe unayetukeshwa
Pote tunapolala.
- 4 Kifo kikighafilika
Tungali usingizini,
Tuamke kwako mbinguni
Hapo tukae nawe.

"Sun of my soul."

(26)

H.C. 21. [L.M.]

- 1 **J**UA la roho Ee Mwokozi
Ukiwapo sihofu giza;
Hivyo dhambi hazitaweza
Kukuficha machoni pangu.
- 2 Nituzwapo na usingizi
Macho yakipumzika leo,
Mawazo yangu ya mwishoni
"Nikae kifuani mwako."
- 3 Ukae nami mchana wote
Pasipo wewe sina uhai
Ukae nami usiku wote
Pasipo wewe siwezi kufa.
- 4 Kama mwana amepotea
Na yako ameyadharau
Utumike moyoni leo
Tena asilale dhambini.
- 5 Wagonjwa wote wauguze
Uwape masikini neema,
Uwafariji waliao
Ili watue kweli kwako.
- 6 Na tutakapoamka tena
Tuwe pamoja tuendapo,
Tukae daima pendoni
Hata tufike kwako juu.

"The day is past and over."

(27)

H.C. 28. [P.M.]

- 1 **K**UMEKUCHWA, na mimi
Nakushukuru Bwana,

Naomba saa za giza
Zisilete hatia.
Ewe Yesu unilinde
Uniponye usiku huu.

2 Furaha zake mchana
Zimekwisha kupita,
Naomba saa za giza
Zisiwe na chukizo,
Unimulikie giza
Uaniponye usiku huu.

3 Na kazi zikiisha
Nitakutazamia,
Niombe unitunze
Katika maumivu.
Ee Yesu ukeshe kwangu
Uanilinde usiku huu.

4 Utunze roho yangu
Kwani wee Mungu tu,
Ndiwe uzijuaye
Hatari zangu zote.
Ewe Yesu Mpendwa wangu
Madhara uniondolee.

11

“ Abide with me.”

(28)

H.C. 20. [IOS.]

1 **U**KAE nami kwani kunakuchwa,
Nakuhitaji giza linazidi ;
Waniachapo marafiki zangu
Mwenye huruma nyingi uwe nami.

2 Maisha yetu muda mfupi sana
Furaha zake zinapita mbio ;
Uharibifu uko pande zote,
Uliye wa milele uwe nami.

3 Usije kwangu mwenye kuogofya,
Na nguvu kuu za kutiisha watu,
Ila na pendo na huruma kubwa ;
Njoo kwangu Bwana Yesu Mwokozi.

4 Nakuhitaji wewe kila saa
Ili nishinde nikijaribiwa ;
Hakuna atakayeniongoza,
Kwa hiyo siku zote uwe nami.

5 Adui zote sitawaogopa
Taabu, machozi wala maumivu.
Mauti na kaburi sitahofu
Mwokozi ungali upo na mimi.

6 'Kae karibu nitakapokufa
Ondoa hofu, niongoze kwako.
Huko mbinguni kunapambazuka
Kwani naona mbele wewe tu.

12

“ O Saviour, bless us ere we go.”

(32)

H.C. 31. [8s.] [Tune “ Stella ” preferable.]

1 **M**WOKOZI utubarikie
Kabla hatujatawanyika
Utie moyoni maneno
Ya kuchochea sisi sana ;
Pote mchana, tena usiku,
Ee Yesu uwe mwanga wetu.

2 Katika saa za siku hii
Tumeyatenda mambo mbali.
Hatukushinda mara nyingi
Ila tulianguka sana, n.k.

3 Kwa watu wote twakusihii,
Wenye huzuni na maskini,
Tena waliofanya dhambi
Uhurumie watu wote, n.k.

- 4 Mwokozi utubarikie,
Kwa maana sasa kumekuchwa
Roho awe pamoja nasi
Nao wote tuwapendao, n.k.

13

"Glory to Thee my God."

(33)

H.C. 19 [L.M.]

- 1 **N**INAKUSIFU Mungu wangu,
Kwa mibaraka yote kwangu ;
Ewe Mfalme uliye mkuu
Usiku huu unihifadhi.
- 2 Unisamehe Bwana Yesu,
Kwa dhambi nilizozitenda ;
Ili nilale amanini
Nawe na wote duniani.
- 3 Unifundishe Bwana wangu
Nikae pasipo hatia ;
Ndivyo sitaogopa kufa
Kwani nitafufuka kwako.
- 4 Roho yangu na itulie
Katika usingizi bora ;
Hivyo na nguvu nitaamka
Na kukutumikia vema.
- 5 Na usingizi ukikosa,
Nifikirishe za mbinguni ;
Fukuza ndoto zote mbaya
Wala kitu kisinidhuru.
- 6 Mungu wangu ubarikiwe,
Na viumbe vyote duniani ;
Na vyote vilivyoko juu
Tumpe Yeye sifa kuu.

14

"At even e'er the sun was set."

(35)

H.C. 25. [L.M.]

- 1 **L**ILIPOSHUKA jua, Yesu,
Wagonjwa waliletwa kwako
Walikuja wenye huzuni,
Waliondoka kwa furaha.
- 2 Vivyo tunavyofika kwako
Tumelemewa kama hao,
Twajua kwamba upo hapa,
Ingawa macho hayaoni.
- 3 Ewe Mwokozi ufukuze
Madhara yatusumbuayo ;
Wengine hawajakupenda,
Upendo wa wengine haba.
- 4 Wengine wameona kwamba
Shughuli za dunia bure ;
Lakini hawawezi acha,
Maana wamo utumwani.
- 5 Hakuna mwenye raha kweli,
Kwani hakuna bila dhambi.
Hata sisi tukupendao
Tunajiona hatiani.
- 6 Nawe Yesu u binadamu,
Majaribu unafahamu.
Unatuchungulia ndani
Uone tungeyasetiri.
- 7 Ukitugusa kama wale,
Madhara yetu yatatoka,
Basi uguse watu wote
Na kutuponya sisi sote.

15 "Saviour, again to Thy dear name." (36)

H.C. 99. [IOS.] Tune "Ellers."

- 1 **T**ENA Mwokozi tunakutukuza
Kabla ya kurudi kwetu nyumbani,
Halafu ndipo tutasujudia
Turuhusiwe twende amanini.
- 2 Tupe amani kwa usiku huu,
Geuza giza yetu iwe nuru,
Utuhifadhi katika hatari,
Kwako nuru na giza ni mamoja.
- 3 Tulipoamka tulianza omba,
Twataka kuishi kwa namna hiyo ;
Tulinde baada ya ibada hii
Tusije tukatenda lenye dhambi.
- 4 Tupe amani siku zetu zote,
Ndipo mabaya yote hutoweka ;
Wakati wa mwisho ukituita
Tuletwe amanini kwako juu.

WAKATI WA KUJA

16 "A little while our Lord shall come." (40)

S.S. AND S. 910. [IIS. IOS.]

- 1 **N**ATAKA amani isiyoiisha,
Amani iondoayo mashaka ;
Nataka imani ijulishayo
Nitaurithi ufalme wa juu.
- 2 Kitambo tu nikeshe kwa saburi
Na hila za Shetani kupigana ;
Kitambo tu kupanda mbegu zake,
Na kuleta mavuno kwake Yesu.

- 3 Kitambo tu kunywa huko na huko
Yasiyozima kiu yangu kamwe,
Kitambo tu nitakunywa mbinguni
Maji ya uzima kwa Bwana Yesu.
- 4 Kitambo tu ziwake taã zangu ;
Kitambo tu kutazamia Yesu,
Kitambo tu tutaondoka sisi
Bwana arusi twende tumilaki.

17 "Hark the glad sound the Saviour comes."

H.C. 64. [C.M.]

- 1 **F**urahini maana Mwokozi,
Tuliyeahidiwa,
Toka mbinguni anashuka,
Tumwekee tayari.
- 2 Anakuja kuwafungua
Wafungwa wa Shetani,
Atapasua pingu zote
Atatuweka huru.
- 3 Atafukuza mbele yake
Uovu wa Shetani,
Wagonjwa wote ataponya,
Vipofu wataona.
- 4 Wote wanaohuzunika
Atafariji kweli,
Atawaletea maskini,
Utajiri wa juu.
- 5 Kwa hiyo sote tuondoke,
Tukamhimidi Yesu,
Yeye ni Mfalme wa wafalme
Anashukia kwetu.

18 "Lo, He comes with clouds descending." (41)

H.C. 73 AND 366. [8s. 7s.]

- 1 **M**AWINGUNI anashuka,
Aliyeuawa kale ;
Wengi wengi wako naye
Wakimsifu sana sana,
Aleluya Bwana Yesu
Anarudi duniani.
- 2 Kila jicho litamwona
Enzi yake amevaa ;
Wale waliomshutumua
Wakamkaza msalabani ;
Wakilia wakilia
Watamwona siku hiyo.
- 3 Mikononi zimo kovu
Majeraha ya msalaba,
Tena hizo zatubidi
Tumtukuze tuwezavyo,
Kwa furaha kubwa sana
Sisi tunamwanguka.
- 4 Na wokofu ule bora
Tulioutazamia,
Utaonekana, nasi
Tutakwenda tukutane,
Aleluya Bwana Yesu
Siku yako imefika.
- 5 Naam wakuabudu wote
Juu ya kiti kitukufu,
Twa Mwokozi enzi yako,
Twa ufalme kwani wako,
Njoo upesi Bwana Yesu,
Shuka ukatutawale.

19 "Work for the day is coming." (42)

C. AND F. 329. [7s. 6s.]

- 1 **F**ANYENI kazi vema,
Inakaribu siku,
Walioingojea
Wakubwa wa zamani ;
Siku ambayo Yesu,
Aliyeteswa chini,
Atatukia tena
Daima kutawala.
- 2 Fanyeni kazi bora,
Anatukaribia
Kwa wateule wake
Awachukue juu.
Katika siku hiyo
Shetani atashindwa,
Na nguvu zake zote
Hazitadhuru tena.
- 3 Fanyeni kazi njema,
Inakaribu giza,
Ukiisha usiku
Utamulika nuru.
Huzuni zetu zote
Zitageuka shangwe,
Watafurahi wote
Wakimhimidi Yesu.
- 4 Jitahidini wote,
Nanyi msisinzie,
Maana wasaa mfupi
Kabla ya kuchwa jua.
Mngemaliza zote
Ili kuwa tayari,
Jitahidini sana
Mwokozi yu karibu.

“Ye servants of the Lord.” (58)

H.C. 68. [S.M.]

- I **M**NAOTUMIKIA
Mwokozi wenu vema
Mwe waaminifu sana,
Kukeshwa na kutii.
- 2 Jifungeni viuno,
Alivyosema Yesu,
Msiye mkaghafalika
Taã zenu ziwake.
- 3 Alisema, “Kesheni,”
Neno nalo lafaa ;
Na mara akionekana,
Tuende tumlaki.
- 4 Yu heri mtu yule
Aliye mwaminifu
Sifa za Yesu atapewa,
Atatawazwa naye.
- 5 Tena atamketisha,
Mahali pa heshima ;
Hivyo atawakweza wote
Walioamtazamia.

KUZALIWA KWA YESU

21 “The first Nowell the angel did say.” (58)

- I **Z**AMANI shangwe kuu ililetwa chini
Kwa wachunga kondoo katika makonde
Bethlehemu wakawa walinzi wa zamu
Wakaona usiku ajabu ya nuru
- Salaam ! salaam ! salaam ! salaam !
Amezaliwa Yesu Mwokozi.

- 2 Wakaona mbinguni mwangaza wa nyota
Ing 'aayo kwa mbali na masharikini
Wakaenda upesi walivyoambiwa
Bethlehemu wamwone Mwokozi horini, n.k.
- 3 Mashariki walitoka wageni watatu
Majusi waliotafuta Mfalme,
Wakifuata nyota waliyoiona
Wasipate kukosa wanayemtafuta, n.k.
- 4 Kiongozi ni nyota iliyowaleta
Hata mji wa Daudi alimozaliwa,
Ikakaa mara moja isiendeleo,
Pale pale nyumbani alimo Mwokozi, n.k.
- 5 Majusi walipoingia nyumbani
Walipiga magoti kwa heshima kuu,
Mara hiyo walizifungua hazina,
Manemane, uvumba, dhahabu, watoa n.k.
- 6 Sisi sote Wakristo na tumsujudie,
Tumhimidi Mwokozi aliyeviumba
Vitu vyote mbinguni, dunia na sisi,
Naye ametufia na kutukombo, n.k.

22 “O come, all ye faithful.” (59)

H.C. [P.M.]

- I **N**JONI kwa furaha, Enyi waamini,
Njoni tufike hima Bethlehemu ;
Tumsujudie Mfalme wa mbinguni,
Njoöni tumwabudu,
Njoöni tumwabudu,
Njoöni tumwabudu, Yesu Kristo.
- 2 Mungu wa kweli, Mwanga wa dunia
Amekubali kuzaliwa chini,
Mungu halisi, Mwana si kiumbe, n.k.

- 3 Shangilieni, malaika leo,
Nanyi mnaokaa kwa Mungu juu ;
Mhimidini Mtawala wote, n.k.
- 4 Twakusalimu uliezaliwa
Yesu upewe utukufu mwingi,
Neno la Baba, Mwenye utu wetu, n.k.

23 " It came upon the midnight clear." (60)

H.C. 90. [D.C.M.]

- I **Z**AMANI wimbo mzuri huu,
Wimbo tokea mbingu,
Na malaika uliletwa
Kwa wachunga kondoo ;
" Imani kwao walimwengu,
Kutoka Mungu juu
Aliye mwenye neema kuu,"
Kwa kiyo sikieni.
- 2 Hata sasa kutoka mbingu
Hufika duniani,
Na wimbo wao ule ule,
Huimba kote kote,
Wengine wengi ni kiziwi,
Shughuli zao nyingi
Na wimbo haukomi,
Kwa hiyo sikieni.
- 3 Ati nyie mnaosumbuka
Mmelemewa sana ;
Na nyinyi mnao kungoja,
Hamwezi udhaifu ;
Elekeeni juu mbinguni,
Maneno ya amani,
Waliyoimba malaika,
Wanayaimba tena.

- 4 Kwa kweli siku zinapita
Walizotazamia
Wazee wale manabii,
Wakizibashiria,
Zi karibu wadia sasa,
Na watu wake wote
Watamkubali wakiimba,
" Mfalme wa amani."

24 " Thou didst leave Thy throne and
Thy heavenly crown." (65)

H.C. 89. S.S. AND S. 237. [P.M.]

- I **U**LIACHA kiti cha enzi chako
Uliponishukia chini ;
Hakukuwako nafasi Bethlehemu,
Ulipokuja duniani.
- Ingia moyoni mwangu,
Imo humo nafasi kwako.
- 2 Mbweha wote wanayo mapango yao
Tena ndege zina viota ;
Bali wewe ulilala chini tu,
Majangwani mwa Galile, n.k.
- 3 Malaika walikwimbia sana
Watangaze Ufalme wako,
Ilakini ulijinyenyekeza
Ukazaliwa kama sisi, n.k.
- 4 Ulifika unalo neno hai
Liwezalo kutufungua,
Ila walikutweza na kukuua
Msalabani kwa Kalvari, n.k.

- 5 Na utakaporudi hapa chini,
Utarudi u Mshindaji,
Tutakufurahia tukisikia
Unatuita sisi kwako, n.k.

25 “Hark, the herald angels sing.” (66)

H.C. 87. [D. 75.]

- 1 **S**IKIENI! Malaika
Wanamsifu Bwana Yesu
Amekuja 'patanisha
Wakosaji naye Mungu.
Mataifa, ondokeni!
Na tumsifu Mungu wetu,
Vitu vyote vinaimba,
Kwetu Yesu azaliwa.

Sikieni! Malaika
Wanamsifu Bwana Yesu.

- 2 Ndiye Mungu wa milele,
Mbinguni anasifiwa
Siku hizi amekuja
Azaliwe na Bikira;
Na Ungu umefichwa
Mwilini mwa mwanadamu,
Yesu yu Emanueli,
Ampenda kaã nasi, n.k.
- 3 Ndiye Mfalme wa Amani,
Tena yu wa haki kweli;
Huletea watu wote
Nuru na uzima mpya.
Aliacha utukufu,
Akafika duniani
Ili tuokoke sisi
Tuzaliwe kimbinguni, n.k.

- 4 Njoo! Uliyetamaniwa,
Njoo! ukae nasi leo,
Njoo! Mzao wa mwanamke
Seta kichwa cha Shetani;
Futa mfano wa Adamu
Na badala yake, tupe
Sura yako kamilifu,
Sura yako ya kimoyo, n.k.

26 “While shepherds watched their flocks.” (67)

H.C. 83 AND 113. [C.M.]

- 1 **W**ACHUNGA walipowatunza
Kondoo zao kondeni
Malaika aliwajia
Wakaogopa sana.
- 2 “Msiogope,” akasema,
“Maana, habari njema,
Ndio, ninawaleteeni,
Na watu wote pia.
- 3 Katika mji wa Daudi,
Na kwa ukoõ wake
Yesu leo amezaliwa
Na hivi mtamjua.
- 4 Yeye utamkuta amevikwa
Mavazi ya kitoto
Horini kule amewekwa
Ingawa Mwana Mungu.”
- 5 Malaika alipokwisha
Majeshi toka juu
Waliondoka wakaimba,
Wimbo wa shangwe huu;

6 “Kwa Mungu uwe utukufu,
Duniani amani,
Upendo uwe kwao wote
Leo na siku zote.”

27

“Christians, awake, salute the
happy morn.” (68)

H.C. 84. [6. IOS.]

1 **A**MKENI ndugu mlio Wakristo
Yesu alizaliwa siku hii ;
Na tumwabudu kwa upendo mkuu,
Walivyoimba malaika juu ;
Habari zao za furaha kuu
Za kuzaliwa kwake Yesu Kristo.

2 Usiku wachungaji walikesha
Wakaambiwa naye malaika,
“Msiogope, ninawaletea
Habari njema za Mwokozi wenu ;
Ahadi Baba ameitimiza,
Amezaliwa Kristo Yesu leo.”

3 Alipokwisha sema, walitoka
Majeshi ya mbinguni wakiimba ;
Wakimtukuza atokaye juu
Atuokoe kwa huruma kuu,
“Na utukufu una Mungu juu,
Amani kwao walioridhiwa.”

4 Wachunga walienda Bethlehemu
Waone Mungu aliyoitenda,
Wakawakuta Mwana na wazazi
Bandani mwenye ng'ombe wamekaa
Wakatokea watangaze pote
Ajabu ya upendo wake Mungu.

5 Hivyo ndivyo na sisi tueneze
Ulimwenguni maneno ya Yesu,
Habari zote tangu siku hiyo
Hata alipokufa Kalvari.
Tena tuutwike msalaba weru
Na tumwandame siku zote hapa.

6 Na tukimfuata kwa uaminifu
Tutastahili kwenda kwake juu,
Hapo ndipo tutamtukuza sana
Aliyeshuka akomboe sisi.
Fahari yake yote tutaona,
Nasi tutafahamu pendo lake.

MWAKA MPYA

28

“All, all for Thee, dear Saviour,
may this watchword.” (69)

H.C. 524. [IIS. IOS.]

1 **N**ATAKA sana mwaka huu wote
Mwokozi wangu niwe wako tu,
Mawazo yangu na matendo yote
Yashiriki kukutukuza wewe.

2 Nataka sana unitwae mimi
Ondoa lolote lisilofaa,
Natoa nafsi yangu kwako Yesu
Unitendee utakavyopenda.

3 Nakutolea moyo nikupende
Kuliko nilivyofanya zamani,
Nitende yapasayo kwa furaha,
Lizidi pendo langu kila siku.

- 4 Nakutolea makusudi yangu
Maana kaidi sana roho yangu ;
Ina kiburi nisiitawale,
Nitapendezwa ukiiongoza.
- 5 Ee Bwana, Roho yako awe mwangu,
Unitumie niwapelekee
Walio gizani, wasiojua
Habari zile za wokofu wako.

29 " My times are in Thy hand." (70)

H.C. 103 AND 245. [S.M.]

- 1 **Z**A mbele sizijui
Nakukabidhi wewe
Uzima, roho, na rafiki,
Vyote naacha kwako.
- 2 Za mbele sizijui
Yatakavyokuwaje ;
Nipe mabaya au mema,
Napenda utakayo.
- 3 Za mbele sizijui,
Lakini siogopi ;
Baba anayonitolea
Lazima yanifae.
- 4 Za mbele sizijui,
Yesu Mwokozi wangu
Na wewe niliyekutesa
Ni kiongozi wangu.
- 5 Za mbele sizijui,
Nakutumaini ;
Kiisha kufa nitapenda,
Kukaa kwako milele.

30 " O God of Bethel, by whose hand." (71)

H.C. 104 AND 279. [C.M.]

- 1 **E**Uliyechungu watu
Tokea siku za Yakobo
Hata siku ya leo,
- 2 Nadhiri na maombi yetu,
Twaleta mbele yako,
Ewe Mungu wa Baba zetu
Utusikie sisi.
- 3 Popote tukiwa na shaka,
Utuongoze vema,
"Tupe riziki zetu leo
Na nguo za kufaa.
- 4 Utulinde nyakati zote,
Popote tukaapo
Hata tufikie salama
Kwa nchi yetu juu.
- 5 Baraka hizo twaziomba
Tukijinyenyekeza,
Utupe siku zote neema
Maana U Mungu wetu.

EPIFANIA

31 " Come, Thou long-expected Jesus." (75)

H.C. 109. [8s. 7s.]

- 1 **N**JOO Yesu umengojewa
Kwa miaka mingi sana,
Ulifika kuondoa
Hatia ya watu wako.

2 Faraja ya Israeli,
Tumaini la dunia,
Watamaniwa na wote,
Furaha ya kila moyo.

3 Umekuja kuokoa
Hatimae kutawala,
Ufalme wako ulete,
Utumilki na neema.

4 Kwa Roho yako daima
Utawale mioyoni
Na uwezo wako bora
Tupandishe kwako juu.

32 "Hail, Thou source of every blessing." (76)

H.C. 120. [D. 8s. 7.]

1 **B**ABA Mfalme wanadamu
Sisi tulio wageni
Watu tu wa mataifa,
Twaruhusiwa kufika
Mbele yako bila hofu ;
Sasa twakusujudia
Tukisifu neema yako
Kwa imani tu thabiti.

2 Kale haikuwa hivi,
Bali sasa twakaribu ;
Tumekombolewa nawe,
Tumepatanishwa pia.
Neno hilo lilifumbwa
Kwao watu wa zamani,
Sisi tumefunuliwa
Za rehema zako kuu.

3 Basi Ee Yesu Mwokozi
Ulakiye watu wote,
Tu mataifa twaleta
Tunu zetu mbele yako ;
Hasa tunakutolea
Roho, mwili, na akili ;
Tungestahili kurithi
Utukufu wa mbinguni.

33

"As with gladness men of old." (77)

H.C. 106. [Six 7s.]

1 **K**WA shangwe wale Majusi
Waliona nyota yako,
Mara wakaifuata
Huko iwaongozako,
Sisi nasi kwa imani
Bwana tuongozwe kwako.

2 Wakaenda kwa furaha
Kumtafuta kwenye hori
Bwana wa viumbe vyote,
Wakamsujudia huko ;
Sisi nasi tutafute
Kiti chako cha neema.

3 Wakazitolea tunu
Mahali pa umaskini,
Sisi nasi kwa furaha,
Wenye moyo safi sana
Tutolee nafsi zetu,
Ni sadaka kwako Bwana.

4 Yesu mwema utulinde
Tusikose njia zako,
Baada ya maisha haya

Utulete kwako juu,
Kusikokuwa na haja
Tuongolewe na nyota.

- 5 Kwa nchi ile ya nuru
Hatutahitaji jua,
Maana wewe nuru yake
Isiyokuchwa daima ;
Hapo ndipo tutaimba
Sifa zako kwa milele.

34 " O Thou who by a star didst guide." (78)

H.C. 105 AND 113. [C.M.]

- 1 **U**LIWAONGOZA na nyota
Majusi wa zamani
Hata walifika mahali
Yesu alipolazwa.
- 2 Huwaongozi watu wako
Na nyota siku hizi,
Lakini Roho Mtakatifu
Ataonyesha njia.
- 3 Hatukujui sana bado,
Lakini hili kweli,
" Watakuona wale tu
Wenye mioyo safi."
- 4 Mwokozi tupe sote neema
Mioyo isafike,
Ili tupate kukuona
Tukujue ulivyo.

35 " Brightest and best of the sons of morning." (79)

H.C. 107. [I.I.S. 105.]

- 1 **N**YOTA ya mapambazuko ing'aayo,
Tupe msaada utumulikie,
Tulete mpaka walipoimlaza
Mwana wa Mungu, Ye Mwokozi wetu.
- 2 Hakuzaliwa mwenye nyumba nzuri
Ila katika banda ya ng'ombe ;
Na hapo akilala, malaika
Wanasujudia Mfalme wa wote.
- 3 Na sisi je ! tutamtolea nini
Ili kuonyesha upendo wetu ?
Je ! fedha zile zote za dunia
Lulu, dhahabu, vito vya thamani ?
- 4 Vipawa au tunu kama hivyo
Havina kwa Yesu faida kuu ;
Anavyotaka zaidi ya vyote,
Ndivyo ibada ya kweli ya moyo.
- 5 Nyota ya mapambazuko ing'aayo
Tupe msaada utumulikie ;
Tulete mpaka walipoimlaza
Mwana wa Mungu, Ye Mwokozi wetu.

36 " Jesus shall reign where'er the sun." (81)

A.M. 220. H.C. 16. [L.M.]

- 1 **Y**ESU atatawala pote
Panapopita jua lake ;
Ufalme wake utadumu
Hautakuwa na kikomo.

- 2 Watasujudu watu wote,
Ili kumtawaza mfalme
Duniani mwote daima
Tabia yake isifiwe.
- 3 Kwa lugha zote mbali mbali,
Kwa nchi zote duniani,
Adhama zake kubwa sana
Kwa shangwe zitaimbwa pote.
- 4 Baraka ziko aendako,
Wafungwa na hufunguliwa,
Waliochoka hustarehe,
Hushiba wale wenye njaa.
- 5 Kila kiumbe kikatoe
Heshima zihusuzo mfalme,
Na malaika waimbapo,
Dunia ijibu "Amina."

37 "Thy kingdom come, O God." (84)

H.C. 354 AND 258. [S.M.]

- 1 **U**FALME wako uje,
Ewe Mwenyiezi Mungu,
Zuia waharabu
Ukakomeshe dhambi.
- 2 Amani iko wapi?
Usafi na upendo?
Machuki bado upo,
Vitaondoka lini?
- 3 Na siku ziko wapi
Uishapo ugomvi?
Na majeuuri yote
Yataondoka lini?

- 4 Twaomba sana Bwana,
Ondoka na uwezo,
Uje uwafariji
Wakutazamiao.
- 5 Watu hulidharau
Jinalo takatifu,
Aibu inazidi,
Upendo hupungua.
- 6 Katika nchi nyingi
Wokofu hawajui,
Utoke Bwana Yesu
Na kuwaleta hao.

38 "Ye servants of God, your Master
proclaim." (85)

H.C. 123. [IOS. IIS.]

- 1 **E**NYI watumishi wa Mungu mkuu,
Tangazeni kote Jina lake Yesu,
Yeye yu mshindaji wa yule Shetani,
Na ufalme wake ni mtukufu sana.
- 2 Mungu hutawala huko mbinguni
Naye ni karibu, atatuokoa
Husifiwa sana kwa uwezo wake
Ametuletea wokofu kwa Yesu.
- 3 Sifuni Mungu kitini mwa enzi,
Ondokeni nyie, heshimuni Mwana,
Malaika hutangaza sifa juu
Za Yesu Mwokozi wanayemwabudu.
- 4 Na sisi pia, tupige magoti
Tuimsifu Yesu ilivyo ya haki;
Yapasa apewe utukufu wote,
Shukrani, baraka, heshima na pendo.

39 "Revive Thy work, O Lord." (87)

H.C. 167. [S.M.]

1 UWAAMSHE Wakristo,
Ee Mungu mwenye enzi,
Usemu na sauti kuu,
Ili tusikilize.

2 Uamshe kazi yako,
Kwani inafifa
Na itakufa sasa hivi
Usipoipuliza.

3 Utuamshe Wakristo,
Roho zikutamani,
Na tutafute mkate tu
Unaotoka juu.

4 Uamshe kazi yako,
Watu wakutukuze,
Na kwa nguvu za Roho yako,
Uwashe mioyo yetu.

5 Uamshe kazi yako,
Utunyweshee mvua,
Ili izidi kusitawi,
Na wewe usifiwe.

40 "Rescue the perishing." (88)

S.S. AND S. 814. [P.M.]

1 UWAOKOE wale
Wanaokufa,
Kabla hawajapotea kabisa ;
Uwalilie wale
Wanaotanga,

Uwaambie za Yesu Mwokozi.
Uwalilie wale,
Wanaokufa,
Yesu wa huruma ataokoa.

2 Ingawa watu hao
Wamemdharau,
Yesu mwepesi kuwaachilia ;
Kwa hiyo uwasihi
Tena wavute,
Atawasamehe wakiamini, n.k.

3 Mioyoni mwa watu,
Umo upendo,
Ambao Shetani anaupinga,
Na wakifadhiliwa,
Na kusihiwa,
Upendo huo utaamka tena, n.k.

4 Uwaokoe watu
Ndiyo faradhi ;
Yesu atatuwezesha tufanye ;
Toka walipotanga,
Uwarudishe,
Uwaambie Yesu amekufa, n.k.

41 "For My sake and the Gospel's go." (89)

G.B. 612. [8s. 7s.]

1 ENENDENI kwa ajili yangu,
Mkahubiri Injili,
Wajumbe walijibu, "Naam,
Nawe tu utukuzwe."
Habari zote hueneza
Kifo na ufufuo,
Na hasa damu ya thamani,
Itupatanishavo.

- 2 Sikilizeni watu wote
Jinsi zieneavyo,
Habari za wokofu huu,
Mpaka kila taifa.
Na waamini hupigana,
Waushinde uovu,
Na siku yake Bwana Yesu
Yazidi karibia.
- 3 Sauti ya watakatifu
Huzidi kusikiwa,
Na wale waliofariki
Wanashiriki nao,
Zimefuliwa nguo zao,
Na damu ya Mwokozi ;
Ndio waliostahimili,
Kwa hiyo wastahili.
- 4 Yesu naye akaribia,
Yeye Mjumbe wa Mwisho,
Ametawazwa faharini,
Maana yu Mfalme kweli.
Ee Yesu, Wee uzima wangu,
Nuru, tena upendo,
Ufalme wote wako tu
Sasa na kwa milele.

42 "Thou whose Almighty Word." (91)

H.C. 131. [6s. 4s.]

I ULIPOSEMA Bwana
Dunia ilumbwa,
Nuru ikawa ;
Sasa twawaombea
Wale wasiojua,
Na nuru imulike,
Moyoni mwao.

- 2 Wewe uliyefika
Uwalettee watu
Afya ya ndani,
Uwaponye wagonjwa,
Na vipofu waone,
Utupe sisi sote
Nuru moyoni.
- 3 Roho ya pendo, kweli
Uletaye uzima,
Tenda upesi ;
Pita mahali pote,
Hasa pale pa giza
Uwape watu wote
Nuru moyoni.
- 4 Mungu abarikiwe,
Kwani Mwenye hekima
Pendo, uwezo,
Hivyo havipimiki,
Vyasaidia sisi,
Basi iwe kwa wote,
Nuru moyoni.

KWARESIMA

43 "I need Thee, precious Jesus." (98)

H.C. 397 AND 126. [7s. 6s.]

I NAKUHITAJI Yesu,
Maana ni mwenye dhambi ;
Roho ina hatia
Na moyo umekufa ;
Nakuhitaji sana,
Kwa kukukimbilia,
Na damu ya thamani
Yaosha dhambi yangu.

- 2 Nakuhitaji Yesu,
Kwani mimi maskini
Mgeni tena Msafiri,
Na mali sina hapa.
Nataka unipende,
Tena kunifaraji ;
Uniongoze chini
Nisije nikatanga.
- 3 Nakuhitaji Yesu,
Rafiki kama wewe,
Rafiki Msaidizi,
Mwenye kutunza mimi ;
Nataka mtima wako,
Maäna sitaweza
Chukua peke yangu
Huzuni na taäbu.
- 4 Nakuhitaji Yesu,
Nyakati zangu zote
Uniongoze vema,
Nisipotoke leo.
Nataka Roho yako
Anifundishe mimi,
Nijue moyo wangu,
Nizidi kukuona.
- 5 Nakuhitaji Yesu,
Nataka kukuona
Katika utukufu,
Kitini pa fahari ;
Tuliokombolewa,
Tutafurahi sana
Kukaza macho yetu
Katika wewe tu.

44 " Oh, the bitter shame and sorrow." (99)

H.C. 333. [8.7.]

I **N**AKUMBUKA kwa aibu
Siku zile za zamani,
Nilipodharau Yesu
Sikumtaka, nikajibu,
" Mimi tu, sipendi Wee."

2 Alinitafuta sana,
Nikamwona msalabani,
'Kamsikia akiomba
" Baba wasamehe hao,"
Likaanza pendo mwangu.

3 Kila siku niliona
Jinsi alivyonienda,
Na huruma zake nyingi,
'Kanivuta, nikasema,
" Nitakupenda zaidi."

4 Nikazidi kufahamu
Wingi wa upendo wake,
Nikaacha kujipenda,
Moyo wangu ukajibu
" Nakupenda Wewe tu."

45 " Lord, I hear of showers of blessing." (100)

S.S. AND S. 485. [8s. 7s. 3.]

I **B**WANA nasikia kwamba
Unawabariki wengi ;
Mibaraka kama mvua
Inanyeshwa juu yao :
Mimi je ?
Uninyweshee na mimi.

- 2 Usipite Bwana Mwema,
Kweli mimi mwenyi dhambi ;
Haki uniache mimi,
Ila unihurumie.
Mimi je ?
Unihurumie na mimi.
- 3 Usipite Ee Mwokozi,
Ningeambatana nawe,
Nina hamu uniite
Uitavyo watu wale.
Mimi je ?
Uniite kama wale.
- 4 Usipite Roho Mwema,
Wawezeshe wadhaifu ;
Watokea kwake Yesu
Uzinipe nguvu zake ;
Mimi je ?
Uwezeshe mimi pia.
- 5 Nimekuwa hatiani,
Tangu siku za zamani ;
Nimeshikwa na dunia,
Nisamehe, niokoe.
Mimi je ?
Univute mimi kwako.
- 6 Pendo lake Mungu kubwa,
Damu yake Bwana Yesu,
Neema isiyopitika ;
Hivyo vyote vinivute.
Mimi je ?
Utanisamehe mimi.
- 7 Usipite, ila lete
Masamaha yako kwangu ;
Unawahuisha wengi,

- Nipe mibaraka pia ;
Mimi je ?
Nakuomba ubariki.
- 46 "Just as I am without one plea." (101)
A.M. 255. [8s. 6.]
- 1 **K**AMA nilivyo, nipokee
Nitakutegemea wewe,
Sababu waniita tu
Mwokozi wangu naja.
- 2 Nilivyo mimi, ni mpotevu,
Nahofu nikisitasita,
Vita ndani si nje tu ;
Mwokozi wangu naja.
- 3 Nilivyo, maskini, kipofu,
Nataka sana uniponye ;
Rohoni si mwilini tu
Mwokozi wangu naja.
- 4 Nilivyo, utanipokea,
Kukaribisha, kusamehe,
Kwani umeahidi tu
Mwokozi wangu naja.
- 5 Nilivyo, pendo lako kuu
Limeondoa mazuiio,
Nataka kuwa wako tu ;
Mwokozi wangu naja.
- 6 Nilivyo, pendo lanivuta,
Nizifahamu zako zote
Mbinguni siyo chini tu,
Mwokozi wangu naja.

"As pants the hart for cooling
streams." (104)

H.C. 149. [C.M.]

- 1 **A**NAVYOYATAMANI maji
Msafiri majangwani,
Ndivyo roho yangu Bwana,
Hutaka neema yako.
- 2 Nitauona uso lini,
Ee Mungu Mfalme wangu ?
Maana roho ina shauku
Kukutazama kweli.
- 3 Basi usikate tamaa,
Utumaini tu.
Na utapata kuziimba
Sifa za Mungu wako.
- 4 Kwa Baba, Mwana, na kwa Roho,
Tumwabuduye sisi,
Iwe daima utukufu
Kutoka watu wote.

"O Thou from whom all goodness
flows." (105)

H.C. 154 AND 239. [C.M.]

- 1 **H**UTOKA kwako wema wote,
Kwa hiyo nakuomba
Katika shida zangu zote,
Unisikie Bwana.
- 2 Na dhambi ikinilemea
Yesu unisamehe,
Na kunipa amani yako,
Unikumbuke Bwana.

- 3 Na nikijaribiwa sana,
Nataka kuanguka,
Nipe nguvu kunitoshea,
Unikumbuke Bwana.
- 4 Na watu wakinilaumu
Nataka kasirika,
Nitañshinda yule mwovu,
Kwa msaada wako Bwana.
- 5 Na saa ya kufa ikifika,
Sitaogopa neno
Ukiwa karibu na mimi ;
Unikumbuke Bwana.

"Rock of Ages cleft for me." (106)

H.C. 151 [Six 7s.]

- 1 **M**WAMBA uliipasuka,
Ndani yako nijifiche ;
Maji yale, damu ile,
Vilivyotoka mbavuni,
Iwe dawa ya rohani,
Viniushe dhambi zangu.
- 2 Kazi za mikono yangu,
Haziwezi 'nikomboo,
Hata nikilia sana
Na kutenda kazi nyingi,
Sitaweza 'jiokoa ;
Ila Wewe peke yako.
- 3 Mikononi sina kitu,
Nashika msalaba tu ;
Mimi uchi univike,
Sina nguvu niwezeshe,
Mimi mchafu unioshe,
Au kweli nitakufa.

- 4 Siku zangu zikiisha,
Ni tayari toa roho,
Nitakapokwenda juu
Nikuone hukumuni,
Mwamba uliopasuka,
Ndani yako nijifiche.

50

“ I lay my sins on Jesus.” (107)

C. AND F. 446. H.C. 96. [D. 7s. 6s.]

- I **N**AWEKA dhambi zangu
Kwake Mwokozi wangu,
Huzichukua zote
Na kuniweka huru,
Namwekea hatia,
Madoa aondoe,
Na nitatakasika,
Na kuwa safi sana.
- 2 Naweka haja zangu
Juu yake, yu karimu ;
Huniponya ugonjwa
Na kukomboa roho.
Huzuni naziweka,
Mizigo na mashaka ;
Huvipunguza vyote
Akishiriki nami.
- 3 Naegemea kwake,
Kwani roho ni nzito,
Mkono wa kuume
Utanisimamisha.
Napenda jina lake,
Emanueli, Kristo,
Nalo laburudisha
Wanaochoka sana.

- 4 Nataka kufanana
Na Yesu Mungu Mwana,
Nikiwa mpole sana
Nikiwapenda wote.
Nataka kuwa naye,
Nimsifu kweli kweli ;
Kama wanavyoimba
Wajumbe wake juu.

WALIO NJE KUITWA NA KUKARIBISHWA
NDANI

- 51 “ Whosoever heareth, shout, shout (125)
the sound.”

S.S. AND S. 389. [P.M.]

- I “ **Y**EYE apendaye ” Haya tangazeni,
Enezeni mbali duniani mwote,
Hayo ya furaha kwao watu wote,
Aje, “ Yeye apendaye.”
- “ Yeye apendaye, yeye apendaye,”
Enezeni hayo duniani mwote ;
Baba wa upendo anaita watu,
“ Yeye apendaye ” aje.
- 2 “ Yeye apendaye,” Tena apendapo,
Na mlango ni wazi ili aingie ;
Yesu ndiye njia, kweli ya pekee,
Aje, “ Yeye apendaye,” n.k.
- 3 “ Yeye apendaye,” Ni ahadi kweli,
“ Apendaye,” litadumu kwa milele ;
Apendaye ana utu wake Yesu,
Aje “ Yeye apendaye,” n.k.

52 "Knocking, knocking, who is there?" (129)

S.S. AND S. 422. [P.M.]

1 **H**odi! Hodi! yuko nani?
 Yuko mtu penye mlango
 Yu msafiri wa kifalme,
 Mtu wa ajabu sana,
 Hutamfungulia mlango
 Mtu huyo, roho yangu?

2 Hodi! Hodi! yuko nani?
 Yuko mtu penye mlango?
 Ni vigumu kufungua,
 Maana umeshikwa sana;
 Vyamea vijiti vingi,
 Mpaka mlango ni penyewe.

3 Hodi! Hodi! yuko nani?
 Yuko mtu penye mlango
 Majeraha mikononi,
 Kichwani iko miiba,
 Macho yajaa huruma,
 Yu Mwokozi anangoja.

53 "Jesus is tenderly calling to-day." (131)

S.S. AND S. 396. [P.M.]

1 **Y**ESU aita kwa upole leo,
 Uje upesi, uje upesi;
 Kwa nini wewe wazidi kutanga
 Ukipoteapotea.
 Uje upesi, uje upesi,
 Yesu aita, aita kwa upendo leo.

2 Yesu aita wanaolemewa
 Uje upesi, uje upesi;
 Lete mizigo kuiweka kwake,
 Hatakufukuza kamwe, n.k.

3 Yesu angoja, je utamfikia?
 Yeye tayari, yeye tayari;
 Atasamehe, njoo umisujudu;
 Usikawe ila njoo, n.k.

4 Yesu aita, sikia sauti,
 Leo sikia, leo sikia;
 Aaminiye Jina lake tu,
 Atafurahi milele, n.k.

54 "The Gospel bells are ringing." (134)

S.S. AND S. 356 [P.M.]

1 **I**NJILI yake Yesu
 Yaenea duniani,
 Ni habari za wokofu,
 Kwangu mi, na kwako we,
 Ni, "Mungu alipenda
 Walimwengu wale wote,
 Alitoa Mwana wake
 Awafie msalabani."
 Neno hilo, neno hilo,
 Laenea duniani,
 Neno hilo, neno hilo,
 La wokofu kwao wote.

2 Injili yatulaki
 Karamuni kwake Yesu,
 Kwa hiyo usidharau
 Maana neema yake kuu;
 Ni mkate wa Uzima,
 Mwenye njaa aje na kula,
 Na zikiwa dhambi nyingi
 Zitaondolewa zote, n.k.

3 Injili yatuonya
Siku zote bila kosa,
Kwamba ye akawiye
Atakufa bila shaka ;
Kwa hiyo ondokeni,
Msikawe duniani,
Tena msirudi nyuma
Au mtaangamia, n.k.

4 Injili ina shangwe
Kwani yaletea watu
Neno la wokofu bora
Ulimo Yesu tu.
Habari za furaha,
Nawaleteeni ninyi,
Siku hii amezaliwa
Kristo, Mfalme, na Mwokozi, n.k.

55 "There is life for a look at the Crucified One." (136)

S.S. AND S. 123. [P.M.]

1 **A**TAKAYEMTAZAMA Yesu Msalabani,
Kweli ataupata uzima ;
Kwa hiyo, Mhalifu ukitaka pona
Mwangalie Yesu Msalabani.

Basi nyie tazameni,
Kweli mtaokoka mkikaza macho
Kwa Mwokozi amesulibiwa.

2 Mbona alitolewa Ye kwa namna hii
Isipokuwa atuokoe ?
Au kwa nini kumwaga maisha damuni
Ila kulipa deni ya dhambi ? n.k.

3 Tukilia machozi ya toba ni bure,
Damu Yake tu, itaokoa,
Utaweza kuweka kwake hatia,
Mara Yeye ataiondoa, n.k.

4 Basi usiogope karibia Yesu,
Maana Mungu Mwenyewe hunena ;
Halibaki lo lote tulitende sisi,
Amemaliza yote kabisa, n.k.

5 Basi, twaa mara moja mkononi mwa Yesu,
Akupacho, uzima bora huu ;
Tena jua ya kwamba huwezi potea
Kwa sababu ya kazi ya Yesu, n.k.

56 "There is a fountain filled with blood." (145)

C.F. 491. H.C. 289. [C.M.]

1 **I**LITOKEA sana damu
Mwilini mwake Yesu
Na damu hiyo yasafisha,
Mawaa ya dhambi zote.

2 Na yule mwizi msalabani
Alisafishwa nayo ;
Na dhambi zangu mimi pia
Zimesafishwa nayo.

3 Ee Yesu, wewe mpendwa wetu,
Na damu ina nguvu
Iwakomboe watu wote
Wasipotee tena.

4 Tokea siku ya zamani
Nilipoona damu
Kuimba nimetaka tu,
Nisifu pendo lake.

5 Na nitakapopita juu
Dunia nimeacha,
Nitakusifu Ee Mwokozi.
“Wokovu huo mkuu.”

6 Najua umeniwekea,
Ingawa sistahili,
Dhawabu nitakayopata,
Kwa damu yake Yesu.

7 Dhawabu hiyo namna gani?
Ni neno hili tu,
Nimsifu daima Mwokozi
Na nguvu zangu zote.

57 “Come to the Saviour make no delay.” (148)

S.S. AND S. 1165. [P.M.]

1 **T**WENDE kwa Yesu tusikawie,
Mwenye Msahafu aonyesha njia,
Leo akaa miongoni mwetu
Akituita, “Njoni.”

Tutafurahia siku ile,
Mioyo yetu ikitakasika
Na sisi tutakutana naye,
Mbinguni kwetu juu.

2 “Acheni wana,” Alivyosema,
Kwa hiyo sote tuwe na shangwe,
Tumchague Ye Mfalme wetu,
Tusikawie twende, n.k.

3 Kweli Yesu yupo hapa leo,
Msikieni tena kumtii;
Sauti yake bado yasema
“Njoni wanangu, njoni,” n.k.

58 “God loved the world of sinners lost.” (149)

S.S. AND S. 17. [P.M.]

1 **M**ungu alipenda waasi
Na wapotevu wote,
Wokofu wa thamani kuu
Hutoa bure tu.

Kwa upendo wake mkuu,
Upendo kwangu mimi,
Mwokozi wangu alishuka,
Akafa Kalvarini.

2 Nadai sasa kwa imani,
Mwokozi awe wangu,
Naona kwake ukombozi
Katika dhambi zangu, n.k.

3 Upendo umetupatia,
Uhuru bora huu,
Na kwa imani yetu tu
Hatia itafutwa, n.k.

4 Waamini watafurahi
Katika ulimwengu,
Uzima bora wa mbinguni,
Watauonja hapo, n.k.

5 Shetani sasa hataweza
Poteza waamini;
Kwa nguvu zake Bwana Yesu
Kushinda, tutashinda, n.k.

MAISHA YA BWANA YESU

59 "She only touched the hem of His garment." (153)

S.S. AND S. 55. [P.M.]

1 **A**LIGUSA upindo wa kanzu
La Bwana Yesu tu ;
Alikuwa amezungukiwa
Na watu, kundi kuu.

Nawe utakuwa huru
Ukiugusa tu ;
Uwezo wake kuokoa
Uzima utakupa.

2 Alimfikia akiogopa,
Alijua ya kwamba
Uwezo wake utatoshea
Aponywe udhaifu, n.k.

3 Aligeuka akamwambia,
"Mwanangu usihofu,
Imani yako imekuponya,
Uende salamini," n.k.

60 "Jesus my Saviour, to Bethlehem came." (156)

S.S. AND S. 40. [P.M.]

1 **Y**ESU Mwokozi alifika chini,
Akizaliwa, maskini, horini,
Kweli ajabu, Yeye asifiwe,
Alitafuta mimi.

Alitafuta mimi, alitafuta mimi,

Kweli ajabu, Yeye asifiwe
Alitafuta mimi.

2 Yesu Mwokozi huko Kalvarini
Fidia yangu alinilipia,
Kweli ajabu, aliifanyaje ?
Akinifia mimi.
Akinifia mimi, akinifia mimi, n.k.

3 Yesu Mwokozi kama ya zamani,
Nilipokuwa nikitanga mbali
Alinisihi kwa upole sana
Akiniita mimi.
Akiniita mimi, akiniita mimi, n.k.

4 Yesu Mwokozi atashuka tena,
Ndivyo alivyotuahidi sisi ;
Na nitamwona akirudi hapa
Anichukue mimi.
Anichukue mimi, anichukue mimi, n.k.

MATESO YAKE

61 "Ride on ! ride on ! in majesty." (157)

H.C. 181. [L.M.]

1 **L**EO Yesu U Mfalme mkuu,
Sababu wote wakusifu ;
Wanakutandikia nguo
Upate kutembea humo.

2 Upite, Yesu Mfalme leo,
Ingawa unakwenda kufa
U Mfalme, kwani umeanza
Kushinda mauti na dhambi.

3 Upite Yesu Mfalme leo,
Wanatazama malaika ;
Wanastaajabu kuona
Jinsi unavyokwenda kufa.

- 4 Upite, Yesu Mfalme leo,
Shindano la mwisho karibu,
Na Baba ameketi juu
Aweza kutazama tu.
- 5 Upite Yesu, Mfalme leo,
Ingawa unakwenda kufa ;
Na ukiisha sulibiwa
Tawala, Mfalme kwa milele.

62 "Man of Sorrows, what a name." (160)

S.S. AND S. 102. [P.M.]

- 1 "W A simanzi," Jina gani !
Kwa Mwana wa Mungu Mkuu ;
Alikuwa kukomboa,
Asifiwe Bwana Yesu.
- 2 Alikubali dhahaka,
Na hukumu yangu mimi,
Ili nisiadhibiwe,
Asifiwe Bwana Yesu.
- 3 Tu wabaya hatuwezi,
Yeye ni Mungu Mtukufu ;
Amepatanisha sisi,
Asifiwe Bwana Yesu.
- 4 Alikufa msalabani,
Akalia, " Imekwisha,"
Sasa hutukuzwa juu,
Asifiwe Bwana Yesu.
- 5 Atakapokuja tena,
Kuchukua wateule,
Ndipo tutazidi imba,
Asifiwe Bwana Yesu.

63 "Glory be to Jesus." (163)

H.C. 197. [6s. 5s.]

1 Y ESU asifiwe,
Alitumwagia
Damu yake yote
Huko msalabani.

2 Damu hii yaleta
Neema na uzima,
Na huruma zake
Za ajabu sana.

3 Mto huu wa Damu
Utukuzwe sana,
Umewakomboa
Wanadamu wote.

4 Damu ya Habeli,
Iitaka haki ;
Damu yake Yesu
Masamaha yetu.

5 Na inyunyizwapo
Mioyoni mwetu,
Mwovu hukimbia
Ametiwa hofu.

6 Sisi tukiimba
Hapa duniani,
Sifa waitaka,
Malaika juu.

7 Pazeni sauti
Katika kuimba,
Tuiadhimishe
Damu ya thamani

64 "There is a green hill far away." (165)

483. [C.M.]

- 1 **K**IKO kilima huko mbali
Nje ya Mji mkuu,
Aliposulibiwa Yesu
Kwa wanadamu wote.
- 2 Hatutaweza kufahamu
Jinsi alivyomwa,
Ila twajua aliteswa,
Kwa dhambi zetu sisi.
- 3 Tusamehewe, alikufa,
Tufanywe watu wema,
Tupate kufika mbinguni ;
Sababu yake kufa.
- 4 Mwingine hakuweza tosha
Kulipa dia yetu,
Mlango wa mbingu Yesu tu
Aliweza kufungua.
- 5 Yeye ametupenda sana
Kwa hiyo tumpende ;
Tutumaini damu yake
Tutende kazi zake.

65 "O perfect life of love." (166)

G.B. 275. H.C. II. [S.M.]

- 1 **M**AISHA yake Yesu
Ni maisha ya pendo,
Aliposhuka toka mbingu
Alitimiza yote.

2 Hakuliacha neno
La mapenzi ya Baba,
Huzuni, kazi, moja moja
Alitimiza zote.

3 Uchungu tuonao
Nawe umeuona,
Zisumbuazo binadamu
Anazijua zote.

4 Mwilini mwake Yesu
Asiyekosa kamwe,
Makosa yetu yaliwekwa
Ili tuokolewe.

5 Amenipenda sana
Kwani alinifia ;
Kwa hiyo nitamtegemea,
Nikimwamini yeye.

6 Wakati wa hitaji,
Wakati wa hukumu,
Nitaitumaini damu
Na wema wake Yesu.

7 Moyoni mwangu Bwana
Utende kazi yako,
Upendo wangu ufanane
Na wako mkamilifu.

66 "When I survey the wondrous cross." (169)

H.C. 186. [L.M.]

- 1 **N**IANGALIPO msalaba
Aliofia Mfalme wetu,
Anasa na kiburi changu
Navidharau na kuviacha.

- 2 Hasha Yesu nisijivune,
Ila katika kufa kwako ;
Nakutolea Bwana Yesu
Vinavyonipendeza vyote.
- 3 Kichwani, mikononi pia,
Yachuruzika damu yake,
Hapana taji kama hii,
Upendo huu hauna mfano.
- 4 Na vitu vyote kama vyangu,
Kidogo bure kutolewa ;
Pendo kama hili laḍai
Uzima, roho, vyangu vyote.

67

“ Beneath the cross of Jesus.” (171)

S.S. AND S. 139. [P.M.]

- 1 **P**A Msalaba wa Yesu,
Hapo ningesimama,
Kivuli ni cha mwamba
Kwa waliolemewa,
Likichomoza na jua
Ni nyumba jangwani
Pa kutua mizigo yetu,
Pazuri pa pumzika.
- 2 Hapo ni pema sana,
Tena ngome imara,
Hapo naona haki,
Na pendo lake pia.
Na kama Yakobo mzee
Alivyoona ngazi,
Naona msalaba njia
Iendayo mbinguni.
- 3 Ng' ambo yake Msalaba
Ila si mbali sana ;
Kivuli naona pia
Kivuli cha kaburi ;

Na katikati msalaba,
Nao ni mfano kwangu,
Ni mlinzi kukinga njia
Ifikayo mauti.

- 4 Kwa msalaba wa Yesu
Hata sasa naona,
Sura ya aliyekufa
Ili nisipotee.
Nachomwa moyoni mwangu
Kwa maajabu haya :
Shani la pendo lake kuu
Na uhafifu wangu.

- 5 Kwa hiyo nachagua
Kukaa penye msalaba ;
Na Mwanga wake Yesu tu
Uwe kwa jua langu ;
Anasa za dunia hii
Sitatamani tena,
Mimi nina aibu tu,
Na yeye utukufu.

68 “ Sweet the moments rich in blessing.” (172)

S.S. AND S. 24. [8s. 7s.]

- 1 **N**INABARIKIWA sana,
Kwa kukaa penye msalaba,
Afya, uzima, napata
Tokea Mwokozi humo.
- 2 Nitaketi hapo sasa
Penye damu ya huruma ;
Na nitadai amani
Aliyolipa Mwokozi.

- 3 Kweli hapo pa baraka,
Nataka sujudu pake ;
Na katika macho yake
Kuona rehema kuu.
- 4 Moyo umejaa upendo
Na huzuni nyingi sana,
Kwani dhambi zangu ndizo
Zilizoimsulibisha.
- 5 Nimwamini na kumpenda,
Nimshukuru siku zote,
Nizitafakari zake,
Mimi nifanane naye.

UFUFUO WAKE

69 "Christ the Lord is risen to-day." (174)

C. AND M. 131. [7S.]

- K**RISTO 'kafufuka leo,
Wanadamu, Malaika,
Msifuni, kwa furaha,
Msifuni viumbe vyote,
Ukombozi umekwisha,
Nayo kazi ya upendo,
Vita vyote vimekwisha,
Yesu Kristo yu Mshindaji.
- 2 Na haikuwezekana
Kumfunga mwenye kaburi,
Mauti haina nguvu,
Kristo ameshinda vyote.
Ye yu hai Mfalme wetu,
Wapi nguvu za mauti ?
Amekufa, 'tuokoe,
Kaburi haina nguvu.

- 3 Tutakwenda kwake juu,
Tutamfuata mbinguni,
Tena kufufuka naye,
Tena washindaji naye.
Na tumsifu Mfalme mkuu,
Ufufuo na tusifu,
Asifiwe kote kote,
Astahili sifa zote.

70 "Welcome happy morning." (175)

H.C. 207. [IIS.]

- F**URAHINI leo, neno la daima
Kifo kimeshindwa, Uzima ni wetu.
Aliyeuawa, amekuwa hai
Viumbe vimsifu, Aliyeviumba.
Furahini leo neno la daima,
Kifo kimeshindwa, Uzima ni wetu, n.k.
- 2 Hata ulimwengu unashangilia,
Maana Bwana Yesu anakuja tena,
Hatakuja mpole, ila Mfalme mkuu,
Ameshinda giza, amelea mwanga, n.k.
- 3 Ee Mwokozi wetu, kwako ni Uzima,
Ulipotuona tukitangatanga
Ulimwacha Baba na fahari yako,
Ujinyenyekeze, mtu wa unyonge, n.k.
- 4 Wewe ni asili ya uzima wote
Hata kufa kwako hukukukataa.
Kifo chaonyesha, si dhaifu zako,
Ila nguvu zako ulipokishinda, n.k.
- 5 Basi ufungue watu wale wote
Walio watumwa wake yule mwovu ;
Walioanguka waokoke sasa,
Umeshinda dhambi, kifo na kaburi, n.k.

71 "Jesu Christ is risen to-day." (177)

H.C. 21. [7s.]

1 **Y**ESU 'kafufuka leo
Aleluya!
Tunashangilia sana
Aleluya!
Alikufa msalabani
Aleluya!
Hivyo tumekombolewa
Aleluya!

2 Sasa tumtukuze sana
Aleluya!
Mfalme wetu wa mbinguni
Aleluya!
Alistahimili kufa
Aleluya!
Awaponye wenye dhambi
Aleluya!

3 Na kwa maumivu yake,
Aleluya!
Ametuokoa sisi;
Aleluya!
Atawala faharini
Aleluya!
Malaika waimbapo
Aleluya!

72 "Jesus lives, Thy terrors now." (179)

H.C. 213. [7s. 8s.]

1 **Y**ESU hai! basi sasa
Hatutaogopa kifo,
Tunajua kwa hakika,
Hatuwezi shindwa nacho.
Aleluya!

2 Yesu hai! Na mauti
Ni mwanzo tu wa uzima;
Hatutahofu kupita
Mlango ule wa mbinguni.
Aleluya!

3 Yesu hai! Alikufa
Kwa ajili yetu sisi;
Nasi tumtukuze Yeye
Kwa miyo safi sana.
Aleluya!

4 Yesu hai! Tunajua
Hatuwezi tengwa naye
Nguvu zote za Shetani
Zimeharibika kweli.
Aleluya!

5 Yesu hai! Basi sasa
Asifiwe duniani,
Hatimae tutapanda
Tutawale naye huko.
Aleluya!

73 "Aleluya, Aleluya, Aleluya." (180)

H.C. 209. [P.M.]

1 **A**LELUYA! Aleluya! Aleluya!
Shindano, vita, vimekwisha,
Uzima umeanza leo,
Tuimbe sote kwa furaha,
Aleluya!

2 Mauti haiwezi tena,
Kristo ameshinda kabisa,
Tuimbe kwa sauti kuu,
Aleluya!

- 3 Zikiisha siku tatu, Yesu
Alifufuka atumilki,
Na asifiwe Bwana wetu,
Aleluya !
- 4 Aliivunja minyororo
Iliyofunga wanadamu ;
Aliyeshinda asifiwe,
Aleluya !
- 5 Ee Bwana kwa mateso yako
Na kufa kwako, tuokoe
Tuishi nawe na kuimba,
Aleluya !

BAADA YA UFUFUO

74 " Lord of the worlds above." (181)

H.C. 283. [6.6.6.6.8.8.]

- 1 **M**UNGU wa mbingu juu
Hekalu-duniani
Zapendeza sana
Kama pendo limo ;
Kwako mbinguni, moyo wangu
Ungependa kuona Wee.
- 2 Wabarikiwa wale
Waabuduo hapo,
Watafurahi sana
Wale wafikao.
Wanakusifu ; wapendao
Wa heri wakisali pako.

- 3 Hao ni wathabiti
Kushinda wanashinda,
Mpaka wafike wote
Unakokaa Wee ;
Ni heri siku, sisi sote
Tutakapofika kwa Mungu.
- 4 Mungu ni ngao yetu,
Hakosi kutulinda,
Anatukarimia
Na baraka nyingi ;
Yu heri yeye, Mungu wangu,
Anayekutumainia.

75 " O day of rest and gladness." (182)

H.C. 96 AND 519. [D. 75. AND 6S.]

1 **S**IKU ya shangwe leo,
Ya raha na ya nuru ;
Siku tupumzikapo
Tufurahie Wewe ;
Tangu zamani sana
Watakatifu wote
Walimwimbia leo
Baba, Mwana na Roho.

- 2 Mungu aliiumba
Nuru kwa siku hiyo ;
Yesu alifufuka
Toka kaburi leo ;
Na Roho alishuka
Kwa watu wako leo,
Kwa hiyo mara tatu
Imetabarukiwa.

- 3 Leo ni kimbilio
Tunaposumbuliwa,
Twaweza kustarehe,
Ili tuburudike ;
Na tukiona kiu,
Roho zikizimia
Ibada yake leo
Yatufariji sana.
- 4 Leo kwa watu wote
Mana yatoka juu ;
Hulisha wanadamu
Chakula cha kiroho ;
Neno la Yesu Kristo
Lahubiriwa leo,
Chemchemi ya uzima
Isiyoisha kamwe.
- 5 Basi na sisi pia
Tuburudike leo,
Tupate raha kweli,
Raha ya waamini ;
Na tutakapofika
Huko mbinguni juu,
Tutamwimbua Mungu
Baba, Mwana, na Roho.

KUPAA KWAKE

- 76 "The Head that once was crowned
with thorns." (183)

H.C. 105 AND 229. [C.M.]

- 1 **K**ICHWA kilichovikwa miiba
Chavikwa enzi sasa,
Na taji bora ya kifalme,
Kwani Yesu Mshindaji.

- 2 Cheo kikubwa astahili
Kupita vyote juu,
Yu Mfalme wa wafalme wote,
Na Nuru ya mbinguni.
- 3 Yu furaha ya wote chini
Na walio juu pia,
Atufunua pendo lake,
Alivyo tumfahamu.
- 4 Aibu yake msalabani
Imetuwia neema,
Na kwa ajili yake tu,
Twapata shangwe kweli.
- 5 Tukishirikiana naye
Mateso yake chini,
Tutatawala naye juu
Katika utukufu.
- 6 Msalaba ulileta kwake,
Aibu na mauti ;
Wawaletea watu wake,
Uzima wa milele.

- 77 "Lift up your heads, ye gates of brass." (184)

H.C. 113. [C.M.]

- 1 **E**NYI milango fungukeni,
Na pingu zikatike,
Apite Mfalme wa fahari
Mwenye msalaba wake.
- 2 Bendera yake inang'aa
Kuliko nyota zote,
Yawaongoza watu wake
Waendapo vitani.

- 3 Si vita vya dunia hii,
Ila ni vya kiroho ;
Shetani anatomaini,
Ya kuwa atashinda.
- 4 Majeshi ya Mungu Mkuu
Na Mashujaa wa Yesu,
Mwe tayari jipangeni
Kumpigania Kristo.
- 5 Ingawa m wachache sana,
Yesu mwenye uwezo,
Enendeni duniani kote,
Yeye pamoja nanyi.
- 6 Mwatekao lete kwake
Kutoka nchi zote,
Vikiisha vita jitoeni,
Miguuni pake Yesu.
- 7 Endeleeni bila hofu
Kwa Jina lake Yesu ;
Viumbe vyote duniani,
Vitasujudu pake.
- 8 Milango imefunguliwa,
Zimekatika pingu,
Tazama Yesu anapita,
Msalaba umeshinda.

78 "Where the high heavenly Temple
stands." (188)

H.C. AND 237. [L.M.]

- 1 **P**ALIPO Hekalu la Mungu
Lisilojengwa na mikono,
Kuhani mwenye utu wetu
Huwaombea wanadamu.

- 2 Aliyelipa dia yetu,
Aliye Mdhamini wa kweli
Mbinguni, anatuombea
Ni kazi yake ya daima.
- 3 Alipo sasa, atuona
Kwa macho yake ya upendo.
Kwa kuutwaa utu wetu
Dhaifu zetu azijua.
- 4 Aliyeteswa kama sisi,
Ajua maumivu yetu ;
Na juu hawezi kusahau
Machozi yake na huzuni.
- 5 Ameshiriki kila teso
Tunaliona sisi leo,
Misiba yetu aiona,
Atufariji kila mmoja.
- 6 Kitini kwake twathubutu
Kuleta haja zetu zote,
Kuomba msaada bila hofu
Wakati wa kutaabika.

HABARI ZA MBINGUNI

79 "In the sweet by-and-by." (192)

S.S. AND S. 964. [P.M.]

- 1 **I**KO nchi juu, ya baraka,
Kwa imani twaweza 'iona ;
Huko Baba anatumgojewa
Anaweke makao tayari.

Huko juu, Huko juu
Huko juu tuonane na Mungu ;
Huko juu, Huko juu,
Huko juu tuonane na Mungu.

- 2 Tutaimba na furaha hapo,
Nyimbo nzuri za mbinguni juu ;
Na mioyo si mizito tena
Ina furaha bora kwa Mungu, n.k.
- 3 Basi tumsifu Baba kwa moyo
Maana Yeye ni karimu kwetu ;
Pendo lake halina kiasi,
Siku zote tunabarikiwa, n.k.

80

“ There is a happy land.” (195)

H.C. 512. [P.M.]

- 1 **I**KO nchi ya shangwe
Huko mbinguni,
Hapo watakatifu
Wamesimama ;
Wanamwimbia Yesu
Mfalme na Mwokozi wao,
Wapaza sauti zao
Kumsifu Yeye.
- 2 Twende kwa nchi hiyo,
Twende upesi ;
Kwa nini wasiwasi ?
Msikawie ;
Tutafurahi kweli
Dhambi zikiondolewa,
Daima tutakaa
Na Yesu juu.

- 3 Katika nchi ile
Huzuni ? Siyo.
Na tutahifadhiwa
Na Baba yetu ;
Basi tujitahidi
Tuipate taji yetu
Na tutawale juu
Na Bwana Yesu.

81 “ O think of the home over there.” (198)

S.S. AND S. 942. [P.M.]

- 1 **F**IKIRI za nchi ya juu
Kwenye Mwanga wa Mungu mkuu,
Wako huko wateule wote
Nguo nyeupe wamevaa.
Huko juu, huko juu
Fikiri za nchi ya juu ;
Huko juu, huko juu
Fikiri za nchi ya juu.
- 2 Fikiri za rafiki juu
Ambao wametutangulia,
Na za nyimbo wanazoiimba
Mbele yake Mwenyiezi Mungu, n.k.
- 3 Mwokozi ni juu huko sasa
Na wapendwa waliofariki ;
Ningeacha huzuni za chini
Niende nikae pamoja, n.k.
- 4 Nitakwenda kwa nchi ile
Siku chache zikiisha pita ;
Wale waliotutangulia
Wangoja tukae pamoja, n.k.

82 "For ever with the Lord." (205)

H.C. 247. D.S.M. [A. AND M. 231]

- 1 "DAIMA kwake Bwana," amin na iwe hivyo,
Neno hilo lanifundisha 'tafufuka tena,
Nakaa mwilini hapa natanga toka kwako,
Lakini kila jioni, nakaribia kwetu.
- 2 Na ninaposafiri, kwa jicho la imani,
Naona nyumba ya Babangu, sio mbali nami ;
Roho, iionapo, yajaa shauku kubwa
Ya kufikia huko juu kwenye urithi wetu.
- 3 "Daima kwake Bwana," Ee Baba ukipenda,
Timiza ndani yangu sasa, neno hilo bora,
Siwezi kupotea ukinisaidia,
Nitasimama sihofu, ukinipigania.
- 4 Ijapo saa ya kufa nitwe fika kwako,
Uzima wako nitapata wakati wa kifo,
Nitakujua Wewe, unijuavyo mimi,
Nitakariri sikomi, "Daima kwake Bwana."

PENTEKOTE

83 "Come Holy Spirit, Heavenly Dove." (208)

H.C. 105 [C.M.] S.S. AND S. 188.

- 1 UTUSHUKIE Roho Mwema
Na nguvu za uzima,
Uwashe moto wa upendo
Katika mioyo yetu.
- 2 Ee Bwana wetu hatuwezi
Kuendelea hivi ;
Upendo wako mkubwa sana
Na wetu haba tu.

- 3 Njoo Roho, Hua toka mbingu
U Mtoa uzima,
Ulete pendo la Mwokozi,
Katika mioyo yetu.

84 "Spirit Divine attend our prayers." (210)

H.C. 255 AND 394. [C.M.]

- 1 ROHO ya Mungu sikiliza
Masala yetu humu,
Ushuke miongoni mwetu
Na nguvu za neema.
- 2 Ushuke uangazie
Misiba yetu chini ;
Utungoze siku zote
Kwa njia zenye haki.
- 3 Ushuke kama moto mkuu,
Uteketeze uovu
Unaokaã ndani yetu,
Tujitoe kwa Yesu.
- 4 Ushuke namna ya umande,
Utubariki sana,
Utuwezeshe tutumike
Na kumpendeza Yesu.
- 5 Njoo kama hua ya zamani,
Utuletee kwetu
Upendo, tufanane nao
Kanisa lako juu.
- 6 Roho ya Mungu sikiliza
Masala yetu humu ;
Ukae duniani mwote
Uite watu kwako.

85 "Our blest Redeemer, ere He breathed." (212)

H.C. 261. [8.6.8.4.]

- 1 **M**WOKOZI alipotuaga
Alituahidia
Kwamba ataleta Rubani
Akae nasi.
- 2 Akaja kutusaidia
Tuwe yatupasavyo ;
Akae moyoni mwa yule
Mnyenyekevu.
- 3 Tena sauti ya upole
Tunayoisikia
Ni yake, akivikomesha
Shaka na hofu.
- 4 Ee Roho umejaa neema,
Uhurumie sisi,
Ukae miongoni mwetu
Ututakase.
- 5 Uzuri na utakatifu
Si wetu ila wake,
Tushindapo ni Yeye tu
Moyoni mwetu.

86 "Come Holy Ghost, our souls inspire." (214)

H.C. 254. [L.M.]

- 1 **N**JOO Roho Mwema toka Mungu
Uwashe moto penye moyo,
Ni Wewe utuleteaye
Vipawa vyako saba bora.

2 Baraka yako toka juu
Yatufariji kwa upendo,
Uyafumbue macho yetu
Kwa maana hatuoni vema.

3 Utuchangamshe sisi sote
Na wingi wa neema yako,
Fukuza maadui wetu,
Ukiongoza tu salama.

4 Utufundishe tuwajue,
Baba, Mwana, Roho, Umoja
Ili tumbe tusikome,
Uimbo huu wa sifa zako :—

Sifa zote ziwe kwako
Baba, Mwana naye Roho.

87 "O Spirit of the living God." (216)

H.C. 53. [L.M.]

1 **E**WE Roho wa Mungu hai
Ushuke na neema tele
Juu yetu watu wapotevu
Po pote tukaapo chini.

2 Uwashe moto wa upendo
Katika miyo ya wote,
Tuende tubahiri pote
Neno la wokovu mkuu.

3 Fukuza giza, lete nuru
Ondoa machafuko yote,
Uwawezeshe wadhaifu,
Ushinde chuki na rehema.

- 4 Ewe Roho weka tayari
Wanadamu kumkuta Mungu ;
Uvute kwako mioyo yote
Ondoa ukaidi wake.
- 5 Batiza mataifa yote,
Uwaletee ukombozi ;
Usifu Jina lake Yesu
Mpaka wote wasujudu.

88 " Gracious Spirit dwell with me." (218)

A. AND M. 322.

- 1 **R**OHU Mwenye neema kuu,
Nifanane nawe tu ;
Watu wakuone wewe
Ukifanya kwangu kazi ;
Ningetaka, sina hofu,
Kutangaza zake Yesu.
- 2 Roho uliye wa kweli,
Ningesema kweli tu,
Na hekima ya kiroho
Itokee sana kwangu ;
Kwa matendo ya upendo
Nitamshuhudia Yesu.
- 3 Roho Mwema wa upole,
Nifanane nawe sana,
Mara nikijaribiwa
Nikukimbilie Wewe ;
Kwa maisha yangu mema,
Ningemshuhudia Mungu.
- 4 Roho ya uwezo wote,
Nipe uhodari wako,
Hivyo nitaweza shinda,

Peke yangu sina nguvu ;
Nakutumaini Wewe
Uliye imara sana.

- 5 Roho ya utakatifu,
Niwe hivyo, safi tu ;
Najitenga na uovu,
Nachagua vyote vyema ;
Ningemtumikia Yesu,
Maana alinipa Wewe.

89 " Come to our poor nature's night." (219)

H.C. 44. [7S. 5S.]

- 1 **U**JE tulettee nuru,
Mwanga bora wa mbinguni,
Maana tunakaa gizani,
Roho Mtakatifu.
- 2 Wenye dhambi 'tutakase,
Tu wagonjwa, utuponye,
Wapotevu, 'tuokoe,
Roho Mtakatifu.
- 3 Roho zetu ni maskini,
Tupe tokea hazina,
Shangwe, pendo na imani,
Roho Mtakatifu.
- 4 Tena utupe amani,
Utawale nia zetu ;
'Tufunulie za Kristo,
Roho Mtakatifu.
- 5 Ewe Mgeni Mwema sana,
Kaa milele micyoni,
Humo 'tuongoze vema,
Roho Mtakatifu.

6 Utuombee kwa Mungu
Na saüti ya 'pendeza,
Sisi wapungufu sana,
Roho Mtakatifu.

7 Utufundishe ya kuwa,
Mungu kweli Baba yetu,
Tulijue sana chini,
Roho Mtakatifu.

8 'Tutengenezee njia,
'Tuongoze tufikie
Akaapo Baba yetu,
Roho Mtakatifu.

UTATU

90 "Father of Heaven, whose love
profound." (222)

H.C. 263 [L.M.]

1 **B**ABA Mwenyiezi, pendo lako
Fidia imetupatia,
Twakusujudu wenye dhambi,
Utupe pendo na samaha.

2 Mwana wa Mungu, Neno lake,
Mfalme, Kuhani, na Nabii;
Twakusujudu wenye dhambi,
Utupe neema na wokovu.

3 Roho uliye wa milele,
Mtoa uzima na Mhuisha,
Twakusujudu wenye dhambi,
Utupe nguvu na uzima.

4 Utatu, Baba, Mwana, Roho,
Mungu wa siri, wa ajabu,
Utujalie wenye dhambi,
Samaha, neema, na uzima.

NENO LA MUNGU

91 "Holy Bible, Book Divine." (225)

H.C. 487. [7s.]

1 **C**HUO cha Mwenyiezi Mungu
Tunu bora, tena yangu;
Hali na asili yangu
Hayo yote waonyesha.

2 Wakemca nikitanga,
Watangaza za Mwokozi,
Waongoza, wahukumu,
Wafundishe tuokoke.

3 Wafariji huzunini,
Kwa mikono yake Roho,
Waonyesha tutaweza
Shinda Shetani na kifo.

4 Watwambia za furaha,
Za uzima wa milele;
Chuo cha Mwenyiezi Mungu
Tunu bora, wewe wangu.

92 "Lord, Thy word abideth." (231)

H.C. 267. [6s.]

1 **N**ENO lako Bwana,
Litakaa milele,
Laongoza, tena
Laleta furaha.

- 2 Wakikaribia
Maadui wetu,
Litatuhifadhi,
Litatuokoa.
- 3 Nani awezaye
Kueleza shangwe
Wapatayo wale
Waliaminio.
- 4 Siku za mashida
Giza nayo pote,
Latuangazia,
Laonyesha njia.
- 5 Neno la rehema,
Tukiwa wazima,
Neno la faraja
Saa yetu ya kufa.
- 6 Tungezifahamu
Zote zilizomo,
Tungezidi 'penda
Bwana wetu Yesu.

93

"Tell me the old, old story."

S.S. AND S. 1131.

- 1 **U**NIAMBIE zote, za mambo ya mbinguni,
Za upendo wa Yesu, za fahari yake,
Uniambie pole, kama kwake mwana mdogo
Maana mimi ni dhaifu, tena mwenye dhambi.
- Uniambie zote, uniambie zote,
Uniambie zote, za pendo la Yesu.

- 2 Uniambie pole, ili nifahamu
Ukombozi wa ajabu, wokovu kwa dhambi ;
Uniambie sana, nipate kuelewa
Mimi msahaulifu yafaa 'nikumbusha, n.k.
- 3 Nena kwa sauti ndogo tena kwa juhudi,
Kwa mimi mwenye dhambi, Yesu alikuja ;
Nena mara nyingi, ukitaka kwa kweli
Kuwa rafiki yangu na kunisaidia, n.k.
- 4 Nena habari hizo, unaponiona
Kuacha Mwokozi wangu, 'shike za dunia :
Na nitakapovutwa kwenye anasa zake,
Nena habari hizo, " Yesu yu Mwokozi." n.k.

WOKOVU NA SALAMA

94

"Simply trusting every day."

(237)

S.S. AND S. 836.

- 1 **N**IAMINI kila siku,
Niamini nikiteswa,
Ikiwa kidogo tu
Nimwamini Yesu tu.

Niamini siku zote
Niamini kila siku,
Litukialo lo lote,
Nimwamini Yesu tu.

- 2 Roho yake yaangaza,
Moyo wangu huu maskini,
Sitaweza kupotea,
Nikimtumikia Yesu, n.k.

3 Furahani nitaimba,
Huzunini nitaomba,
Hatarini nitamwita,
Nimwamini Yesu tu, n.k.

4 Niamini mpaka mwisho,
Siku zangu zote hapa,
Mpaka 'fika huko juu,
Nimwamini Yesu tu, n.k.

95 "What can wash away my stain?" (261)

s.s. AND S. 874. [P.M.]

I **N**ITATAKASWA na nini?
Ila damu yake Yesu
Sitaweza kuokoka
Bila damu yake Yesu.

Damu ina thamani,
Yaniosha dhambini,
Ni njia ya pekee,
Ndiyo damu yake Yesu.

2 Sioni kitu kingine,
Ila damu yake Yesu.
Sitasamehewa kamwe,
Bila damu yake Yesu, n.k.

3 Nitafidiwa na nini?
Ila damu yake Yesu.
Wema, sina nifanyeni?
Bila damu yake Yesu, n.k.

4 Sina taraja lingine,
Ila damu yake Yesu
Tena sina haki kweli,
Bila damu yake Yesu, n.k.

"Yield not to temptation."

(264)

s.s. AND S. 698. [P.M.]

I **U**SISHINDWE kamwe, Ujaribiwapo,
Kila ushindapo, Utaimarika,
Na kwa uhodari, Ushinde hasira,
Umkabili Yesu, Atakupa uwezo.

Omba msaada kwa Yesu,
Atakusimamisha,
Atakusaidia
Ukimumainia.

2 Epukana nao, Walio wabaya,
Jina lake Mungu, 'Litakase sana,
Saidia 'dhaifu, Moyo uwe mpole,
Umkabili Yesu, Atakupa uwezo, n.k.

3 Aliye Mshindaji, Atapewa taji;
Ijapo pengine Shetani ashinda,
Tusikate tamaa, Tumaini tu,
Umkabili Yesu, Atakupa uwezo, n.k.

"Have you been to Jesus for the
cleansing power?"

(267)

s.s. AND S. 379. [P.M.]

I **U**MEMWENDEA Yesu kwa kusafishwa?
Umeoshwa kwa damu ya Kondoo?
Unategemea sana neema?
Umeoshwa kwa damu ya Kondoo?

Umeoshwa? Umeoshwa?
Umeoshwa kwa damu ya Kondoo?
Nguo zako safi, tena ni nyeupe?
Umeoshwa kwa damu ya Kondoo?

- 2 Unafuatana na Mwokozi wako ?
Umeoshwa kwa damu ya Kondoo ?
Unautegemea msalaba huu ?
Umeoshwa kwa damu ya Kondoo ? n.k.
- 3 Yesu atakapokuja u tayari ?
Umeoshwa kwa damu ya Kondoo ?
Roho je tayari uingie juu ?
Umeoshwa kwa damu ya Kondoo ? n.k.
- 4 Tupa nguo zile zilizochafuka,
Umeoshwa kwa damu ya Kondoo ?
Iko chemchemi kwa walio wachafu,
Umeoshwa kwa damu ya Kondoo ? n.k.

98 "There is a road that leads to God." (270)

H.C. 494

- 1 I KO njia nayo nyembamba,
Iendayo mbinguni,
Walio wake Kristo kweli
Hupenda 'ifuata.
- 2 Yapita tu moja kwa moja
Duniani mwa dhambi ;
Tuifuate hatuhofu
Mpaka tufike juu.
- 3 Atawezaje mwana mdogo
Kupita peke yake,
Maana imo hatari nyingi,
Mitego kwa dhaifu.
- 4 Kwa njia pana wamo wengi,
Wakitembea humo ;
Wakristo wengi wakichoka,
Wafuatana nao.

- 5 Basi nisiteleze humo,
Wala kutangatanga ;
Mwokozi ataniongoza,
Kwa hiyo siogopi.
- 6 Nitaamini Neno lake,
"Atachunga kondoo,
Na atawaleta zizini,"
Kwa hiyo siogopi.
- 7 Nitathubutu endelea,
Akinichunga tu,
Macho mbinguni nitakaza
Mpaka kufika huko.

KUOMBA NA KUSALI

99 "Go when the morning shineth." (273)

H.C. 273. [D. 7s. 6s.] Tune Crüger.

- 1 ENDA kwa asubuhi,
Enda kwa adhuhuri,
Enda kwa alasiri,
Na kwa usiku tena.
Enda kwa usikivu,
Uache mashughuli,
Chumbani usujudu
Na kuomba kwa siri.
- 2 Wapendwa ukumbuke,
Nao wakupendao,
Ombea, wakiwapo,
Wanaokuchukia ;
Na kwa unyenyekevu,
Jiombee baraka,
Na hayo uyatake
Kwa Jina la Mwokozi.

3 Isipowezekana
Kusali peke yako,
Rafiki wakisonga
Na ungependa sali,
Neno lisilotamkwa,
Limo moyoni tu,
Litamfikia Mungu
Mwenye rehema kuu.

4 Baraka ya kusali,
Bora kuliko zote,
Yaleta furaha kuu,
Inayopita zote.
Na ukihuzunika,
Usisahau Baba,
Mujudie Mungu,
Yeye Mfariji Mkuu.

100 "Prayer is the soul's sincere desire." (275)

H.C. 318. [C.M.]

1 **K**USALI ni tamaa ya roho
Kutamkwa au siyo,
Ni hamu kubwa iwakayo
Katika mioyo yetu.

2 Pengine ni uguzi wetu,
Pengine ni kilio ;
Labda kukaza macho yetu
Kwa Mungu peke yake.

3 Kusali ni lugha nyepesi,
Wadogo wajua,
Impendezayo Mungu wetu
Kuliko lugha zote.

4 Kusali ndiko hewa nzuri,
Ni pumzi ya Wakristo,
Kwatutuliza mautini,
Kwatupitisha juu.

5 Kusali ni sauti yake
Aliye mwenye dhambi ;
Wakisikia malaika
Huimba sifa zao.

6 Watakatifu ni wamoja,
Wakati wa kusali ;
Ni ushirika bora sana
Na Baba na Mwokozi.

7 Si sisi tu tunaoomba,
Huomba Roho pia ;
Mwokozi naye huombea
Tulio wenye dhambi.

8 Ee Yesu uliye uzima
Na kweli, pia njia,
Onyesha jinsi ya kusali,
Wee ujuaye sana.

101 "I have a Saviour, He's pleading in
Glory." (279)

S.S. AND S. 350. [P.M.]

1 **N**INA Mwokozi, mbinguni huomba,
Mwokozi ni mpendwa, rafiki wa kweli;
Kwa moyo wa pendo, huniangalia,
Laiti angalikuwa wako pia.

Ninakuombea, ninakuombea,
Ninakuombea, ili awe wako.

- 2 Nina Baba pia, naye amenipa
Tumaini bora, la milele kweli ;
Ataniita niwe kwake mbinguni,
Laiti ungalikwitwa uje nami, n.k.
- 3 Nina mavazi, ni meupe sana,
Yesu anangoja mbinguni anipe ;
Nami nitavikwa mavazi hayo,
Laiti ungalivikwa nayo pia, n.k.
- 4 Nina amani, isiyopimika,
Ambayo wa chini hawawezi jua ;
Yatoka kwa Yesu, siyo kwa mwingine,
Laiti ungaliveza 'ipokea, n.k.
- 5 Mara kukubali Yesu Mwokozi
Waambie wote ulivyompokea ;
Na wewe uombe waletwe pamoja,
Wewe ulivutwa, je ! si wale pia, n.k.

IMANI

102 "My hope is built on nothing less." (288)

S.S. AND S. 902. [Six 8.]

- 1 **N**INACHOTAKA tumaini
Ni damu yake Yesu tu ;
Mwingine sitategemea,
Ila Yesu Mwokozi tu.

Ninasimama pa Yesu,
Yeye ni Mwamba, yu imara,
Pake siwezi kupotea.

- 2 Giza ikija nisione,
Ninategemea neema,
Na nikipepekwa sana,
Nguvu zake zitanishika, n.k.

- 3 Ameahidi 'niokoa,
Amana yangu damu yake ;
Rafiki wote wakitoka,
Yesu ni tumaini langu, n.k.
- 4 Siku atakaporejea,
Atanikaribisha juu,
Na haki yake nitavikwa,
Hivyo hukumu sitahofu, n.k.

103

"Jesus, lover of my soul." (297)

H.C. 299. [D. 7S.]

- 1 **Y**ESU Mpenda roho yangu,
Nakutegemea Wewe ;
Unifiche kwa tufani
Kifuani mwako Bwana.
Dhambi zangu zalemea,
Taabu ni kama dharuba,
Niongoze baharini,
Roho yangu ipokee.
- 2 Sina pa kukimbilia
Ila kwako Yesu Mwema ;
Sina nguvu, ni dhaifu,
Bwana unisaidie.
Tumaini langu lote
Nimekuwekea Wewe,
Sina wa kutegemea
Ila wewe Bwana wangu.
- 3 Wewe Kristo wanitosha,
Huniachilii kamwe ;
Uwaauni dhaifu
Na kuwaponya wagonjwa.
Jina lako takatifu,
Mimi mwovu tena mnyonge,
Dhambi zangu nyingi sana
Wewe ni Kweli na neema.

- 4 Neema nyingi iko kwako,
Kuondoa kila dhambi ;
Nipe maji ya uzima,
'Nitakase moyo wangu.
U asili ya uzima ;
Uhuishe roho yangu,
Kaa daima ndani yake
Iwe hai kwa milele.

104

" Jesus, I will trust Thee." (302)

H.C. 305. [IIS.]

- 1 **Y**ESU, roho yangu nitakukabidhi,
Mwenye dhambi nyingi utaniokoa ;
Mbinguni hakuna, wala hapa chini,
Anayefanana na Yesu Mwokozi.
- 2 Nitaliamini Jina lako Yesu,
Maana yake ndiyo, " Mwokozi wa watu "
Katika msalaba ulisulibiwa,
Kwako Wee aibu, kwetu ni wokovu.
- 3 Nitakuamini, nitatafakari,
Pendo lako kubwa, na rehema zako,
Watu wenye dhambi walikusongea,
Hata wa ukoma ulikaribisha.
- 4 Nitaliamini neno lako Yesu,
Sijakutazama, naamini tu ;
Roho wako Mwema anifundishapo,
Niwe Mwanafunzi anayesikia.
- 5 Nitakuamini pasipo mashaka,
Atakayekuja hutamtupa kamwe ;
Ni ahadi yako, damu ni amana,
Basi najiweka kwako salimini.

105

" Safe in the arms of Jesus." (303)

H.C. 301. [P.M.]

- 1 **M**IMI ni salimini
Nikaapo pa Yesu,
Upendo wake bora
Utanalinda kweli.
Nyimbo za malaika
Sasa nazisikia,
Nyimbo wanazoimba
Huko mbinguni juu.

Mimi ni salimini,
Nikaapo kwa Yesu,
Upendo wake bora,
Utanalinda kweli.

- 2 Mimi ni salimini,
Kwake sishughuliki,
Dunia haivuti,
Wala dhambi 'nidhuru.
Sihuzuniki bure,
Sina mashaka kwake,
Na taabu, machozi,
Hayatakuwa mengi, n.k.

- 3 Yesu ni kimbilio,
Yesu Mwokozi wangu
Hawezi kuniacha,
Basi nitaamini.
Nitasubiri hapo,
Nikingojea siku
Ambayo nitakwenda
Huko mbinguni juu, n.k.

106 "Blessed assurance, Jesus is mine." (312)

S.S. AND S. 873. [P.M.]

1 **H**AKIKA kweli Yesu ni wangu,
 Yeye limbuko la fahari yangu ;
 Mimi ni mrithi, amenunua
 Mwana wa Roho, safi kwa damu.

Hayo ni yangu,
 Hivyo naimba,
 Nasifu Yesu
 Bila kukoma ;
 Hayo ni yangu, n.k.

2 Nimejitoa kwake kabisa,
 Nina kwa hiyo kwake furaha
 Na kwa imani, iko kwa Mungu,
 Shangwe kamili, nayo ni yangu. n.k.

3 Nimejitoa, raha ni yangu,
 Katika Yesu nabarikiwa,
 Ninatazama kwake mbinguni,
 Nimezungukwa na pendo lake. n.k.

107 "I need Thee every hour." (316)

S.S. AND S. 577. [6s. 4s.]

1 **Y**ESU nakuhitaji
 Kwa kila saa,
 Sauti yako tu
 Huleta raha.

Yesu nakuhitaji,
 Nakutaka sana,
 Unibariki sasa
 Nakufikia.

2 Nakuhitaji sana,
 Kaã karibu,
 Shetani hataweza,
 Ukiwa hapo, n.k.

3 Yesu nakuhitaji,
 Siku za shangwe,
 Na za huzuni pia
 Ukae karibu, n.k.

4 Yesu nakuhitaji,
 Unifundishe,
 Ahadi zako kwangu,
 Uzitekeleze, n.k.

5 Nakuhitaji sana,
 Yesu U Mwema,
 Unifanyize mimi,
 Ili niwe wako, n.k.

108 "Peace, perfect peace, in this dark world of sin." (321)

H.C. 280. [10s.]

1 **A**MANI kweli, duniani pa dhambi,
 Damu ya Yesu huleta amani.

2 Amani kweli, tunaposhughulika,
 Kumtii Yesu ni amani kweli.

3 Amani kweli, huzuni pande zote,
 Kwake Yesu iko furaha bora.

4 Amani kweli, na wapendwa ni mbali,
 Ni salama Yesu akiwalinda.

5 Amani kweli, za mbele hatujui,
Yesu twamjua naye yu mbinguni.

6 Amani kweli, mauti ni karibu,
Hatuhofu, Yesu ameshinda.

7 Baada ya haya dunia itaisha,
Yesu atatuleta amanini.

109 "Thine forever, God of love." (322)

H.C. 224. [7s.]

1 "WAKO daima," Ee Mungu
Usikie toka juu,
Tungekuwa wako kweli
Hapa tena kwa milele.

2 "Wako daima," Ee Bwana
Utulinde duniani,
Wee Uzima, Kweli, Njia,
Tuongoze kwako juu.

3 "Wako daima," Wa heri,
Wanaokutegemea,
Ee Mwokozi na Rafiki,
Utulinde mpaka mwisho.

4 "Wako daima," Mwokozi
U Mchungaji wa kondoo,
Tu dhaifu peke yetu,
Tungekaa nawe pamoja.

5 "Wako daima," Rubani,
Hutimiza haja zetu,
Husamehe dhambi zetu,
Tuongoze kwake Baba

110 "The Saviour of the world." (330)

Tune Londonderry Air.

1 SIIJUI Yesu alivyokubali
SKupenda watu wenye dhambi nyingi,
Wala kwa nini aliwatafuta
Awarudishe wasitange tena.
Ila najua alivyojaliwa
Bin Mariamu, kwenye Bethlehemu,
Tena alitumika Nazareti,
Hivyo Mwokozi wetu alivyofika.

2 Siwezi jua maumivu yake
Alivyovumilia duniani,
Wala uchungu wake wa moyoni
Alipokaã sana msalabani;
Ila najua atoa majonzi,
Azua dhambi zetu na hofu,
Awafariji wanaolemewa,
Maana ndiye Mwokozi tena Mponyi.

3 Sijui atakavyoleta wote,
Wala jinsi atakavyomilkisha,
Wala jinsi atakavyoshibisha
Weusi, Weupe, wa hali zote.
Ila najua wote watamwona
Ambapo atakujaa faharini.
Adhama yake zitajulikana
Na watu wote watamkubali Mfalme.

4 Sijui atakavyoabudiwa
Wakati wa kukutanika naye,
Sijui jinsi itakavyokuwa kuu
Furaha itakayojaza moyo;
Ila najua kwenye mbingu zote
Mashangilio yatakuwa huko,
Na watu wote duniani pote
Witamkubali Yesu Mwokozi, Mfalme.

UPENDO

- 111 "There is no love like the love of
Jesus." (331)

S.S. AND S. 42. [P.M.]

I **H**AKUNA pendo lifananalo na lake Yesu Kristo,
Atawatafuta asikome, atawaleta wote.

Pendo kuu, la Yesu
Halipimiki kamwe,
Njoni wakosaji,
Kwenye pendo,
Yesu awaiteni.

- 2 Hakuna moyo ufananao na wake Yesu Kristo,
Na uchungu utusumbua, auona mbinguni, n.k.
- 3 Hakuna jicho lifananalo na lake Yesu Kristo,
Atuangalia tuendapo, ili tusipotee, n.k.
- 4 Hakuna sauti ifananayo na yake Yesu Kristo,
Hujaa upendo na upole, asemapo na sisi, n.k.
- 5 Tusikie sauti yake Yesu, wala kutanga tena,
Hata tutakapofika kwake, kwenye mbinguni juu, n.k.

- 112 "How sweet the name of Jesus
sounds." (336)

H.C. 318. [C.M.]

I **W**AAMINIO Bwana Yesu,
Hupenda Jina lake,
Huzuni, hofu na maradhi,
Lazifukuza zote.

2 Laponya aliyezimika,
Mashaka laondoa ;
Waliochoka lapumzisha,
Lalisha wenye njaa.

3 Hapo ndipo nitaijenga
Nyumba ya kimbilio ;
Kwake hazina imejaa,
Neema maridhawa.

4 Yesu ni Mchungu na Rafiki,
Nabii na Kuhani,
Yu Mfalme, Njia na Uzima,
Pokea sifa zangu.

5 Moyo wangu dhaifu sana,
Mawazo ni hafifu ;
Ila nitakapokuona,
Nitakusifu kweli.

6 Hata hapo nitatangaza,
Upendo wako pote ;
Na nitakapofika kufa
Litanifurahisha.

- 113 "One there is above all others." (339)

H.C. 478. [8s. 4s.]

I **Y**UKO mmoja juu ya wote
Apenda kweli ;
Pendo lapita la ndugu,
Apenda kweli ;
Tutaachwa na rafiki
Walio wageugeu,
Ila Huyu Mwaminifu
Apenda kweli.

- 2 Na kumjua ni uzima
Apenda kweli ;
Deni yetu kwake kubwa,
Apenda kweli ;
'Katukomboia kwa damu,
'Katafuta atuone,
'Katuletea zizini,
Apenda kweli.
- 3 Tumemwona Yu rafiki
Apenda kweli ;
Hupenda kutubariki,
Apenda kweli ;
Mioyo yamfurahia
Ikitupeleka kwake ;
Ya nini kutosadiki ?
Apenda kweli.
- 4 Kwa Jina limo samaha,
Apenda kweli ;
Maadui watashindwa,
Apenda kweli ;
Vyote bora atatupa,
Dhiki atazifukuza,
Atatuletea mbinguni,
Apenda kweli.

114 "Hark, my soul, it is the Lord." (340)

H.C. 319. [78.]

- 1 **S**IKILIZA roho yangu,
Yu Mwokozi, umsikie,
Huuliza kila siku,
"Ati wewe, wanipenda ?"

- 2 "Mimi nilikuokoa
Nikaganga majeraha ;
Nilikutafuta pote
Nikakuleta salama.
- 3 Je mama aweza acha
Mwana aliyemzaa ?
Naam, aweza kusahau,
Bali sisahau kamwe.
- 4 Sighairi nipendapo,
Pendo haliishi kamwe,
Haliwezi kupitika,
Li amini mpaka kufa.
- 5 Utaona enzi yangu,
Nikiisha leta wote ;
Utakaa kitini pangu.
Ati wewe, wanipenda ?"
- 6 Bwana ninahuzunika,
Kuwa pendo langu haba,
Nakupenda, naabudu,
Ningezidi kukupenda.

UTAKATIFU

115 "Search me, O God, my actions try." (349)

C. AND F. 22. [C.M.]

- 1 **N**IPELELEZE, nipimwe,
Na vyote dhihirisha ;
Ni fahamishe rohani
Nijione nilivyo.

- 2 Moyo wangu upeleleze,
Akili zangu pia,
Vilivyofichwa moyoni
Unionyeshe mimi.
- 3 Umulikie moyoni
Panapotoka chuki,
Dhamiri yangu uamshe,
Nizichukie dhambi.
- 4 Mawazo upeleleze,
Na makusudi pia ;
Yaharibuyo rohoni
Uyaondoe humo.
- 5 Na jicho upeleleze,
Uovu wangu wote,
Kwa neema yako niletwe
Nitubu mbele yako.
- 6 Hivyo nitakujua Wee
Upendo nitaona,
Pendo la Mwenyiezi Mungu,
Katika Yesu Kristo.

116

“Nearer my God to Thee.” (353)

S.S. AND S. 581. [6s. 4s.]

- 1 **N**IKARIBIE Wee
Ee Mungu wangu,
Kweli ndio msalaba
Univutao ;
Kwa hiyo nitaimba,
“Nikaribie Wewe,
Nikaribie Wee,
Ee Mungu wangu.”

- 2 Nisafiripo hapa,
Kama Yakobo,
Usiku nitalala,
Mto wangu jiwe ;
Katika ndoto zangu,
“Nikaribie Wewe,
Nikaribie Wee,
Ee Mungu wangu.”
- 3 Hapo nione njia
Mpaka mbinguni,
Hunikarimu sana
Rehema nyingi.
Malaika walaki,
“Nikaribie Wewe,
Nikaribie Wee,
Ee Mungu wangu.”
- 4 Tena ninapoamka
Nisifu Wewe,
Malalo ni Beteli,
“Nyumba ya Mungu.”
Katika shida zangu,
“Nikaribie Wewe,
Nikaribie Wee,
Ee Mungu wangu.”
- 5 Siku zangu za chini
Zinapoisha,
Nitapanda mbinguni,
Nifike kwako.
Hapo wimbo ni huu,
“Nikaribie Wewe,
Nikaribie Wee,
Ee Mungu wangu.”

“ I gave My life for Thee.” (358)

H.C. 349. [Six 6s.]

- 1 **N**ILIJITOA kwako
Na damu yangu pia,
Ili nikukomboe
Na usiangamie,
Nilijitoe kwako.
Wewe je? Nini kwangu?
- 2 Nilichukua shida
Siku zangu za chini,
Upate shangilia,
Siku zako za juu;
Umechukua nini
Unipendeze mimi?
- 3 Nyumba ya Baba juu
Yenye fahari kuu
Nilipenda kuacha,
Kukaa kwa ukiwa;
Hii kwa ajili yako,
Wewe je? Nini kwangu?
- 4 Wokovu na samaha
Nilivileta bure,
Nilikukarimia,
Kwani nilikupenda;
Vipawa gani vyema
Je, umeniletea?
- 5 Basi ujitolee
Katika kazi zangu,
Shirikiana nami
Mateso na furaha;
Nilijitoe kwako.
Nawe kwangu jitoc.

118 “ Oh, for a heart to praise my God.” (363)

H.C. 318. [C.M.]

- 1 **U**NIPE moyo nikusifu,
Moyo pasipo dhambi,
Ulioshwa na damu
Aliyotoa Yesu.
- 2 Moyo ulio na utii,
Hekalu la Mwokozi
Ambamo Yeye hutawala,
Mfalme wake pekee.
- 3 Moyo ulionyenyekea,
Amini, safi, kweli,
Unaoambatana naye
Ulio wake tu.
- 4 Moyo wenye mawazo mema,
Uliojaa upendo,
Mkamilifu, wenye haki,
Sawa na moyo wake.
- 5 Nipe Bwana, tabia yako,
Unijie upesi,
Na Jina lako la upendo
Moyoni 'liandike.

KUTUMIKA KWA MUNGU

119 “ Work for the night is coming.” (368)

S.S. AND S. 778. [7s.6s.5s.]

- 1 **J**ITAHIDINI sana,
Usiku ni karibu
Fanyeni alfajiri,

Tene adhuhuri ;
Fanyeni alasiri
Wala kukoma kamwe,
Jitahidini sana,
Usiku ni karibu.

2 Fanyeni kazi bora,
Maana siku chache,
Wala kukaä bure,
Hata saä moja,
Kazi za Yesu tele
Hazimalizwi hima ;
Jitahidini sana
Usiku ni karibu.

3 Jitahidini sana,
Usiku ni karibu,
Saa za mchana chache,
Kwa hiyo fanyeni.
Fanyeni mpaka giza
Limefukuza mwanga,
Jitahidini sana,
Usiku ni karibu.

120 " Take up thy cross, the Saviour said." (370)

H.C. 351. [L.M.]

1 **U**JITWIKE msalaba wako,
Atuagiza Bwana wetu,
Jinyime, kesha na kuacha
Tamaa za mwili na dunia.

2 Ujitwike msalaba wako,
Usihofu uzito wake,
Kwa nguvu utakazopewa,
Utauweza kuchukua.

3 Ujitwike msalaba wako,
Usikatae kwa kiburi,
Mwokozi alisulibiwa
Atuokoe na Shetani.

4 Ujitwike msalaba wako,
Ujipe moyo kupigana,
Kaburi, kufa, utashinda,
Mbinguni utakuongoza.

5 Ujitwike msalaba wako,
Usiuche hata kufa,
Kwa maana apataye taji
Ndiye achukuaye tu.

121

" Stand up, stand up for Jesus." (373)

S.S. AND S. 680. [D. 7S. 6S.]

1 **M**PIGANIE Yesu
Askari wa msalaba,
Inueni bendera
Hasara isipate ;
Yeye ataongoza
Jeshi lake vitani,
Adui watashindwa,
Yesu atatawala.

2 Mpiganie Yesu,
Aitapo endeni,
Mtoke kushindana
Na maadui wake ;
Majeshi yao mengi
Yasiyohesabika,
Ila uwezo wake
Hauwezi 'pimika.

- 3 Mpiganie Yesu
Kwa nguvu zake tu,
Msijitegemee
Uwezo wenu haba.
Mjivike silaha
Zilizo za kiroho,
Akutakapo Yesu
Mwe tayari hapo.
- 4 Mpiganie Yesu,
Bado kitambo tu,
Leo unapigana,
Kesho mwisho wa vita.
Na taji ya uzima
Hupewa ashindaye,
Atamilki na Yesu
Milele faharini.

122 "Lord, speak to me that I may speak." (374)

H.C. 344. [L.M.]

- 1 **N**ENA nami ili ninene
Ulivyowaambia kale,
Kama ulivyowatafuta,
Niwatafute wapotevu.
- 2 Ongoza Bwana niongoze
Wanaotanga duniani,
Nilishe, nishibishe Mana
Wenye njaa rohoni mwao.
- 3 Unipe nguvu nisimame
Nimeimarika kwa Yesu,
Nami nitawathubutisha,
Wanaotaka kuanguka.

- 4 Unifundishe nitangaze
Habari njema za wokovu,
Maneno yangu yafikie
Wanaofungwa na Shetani.
- 5 Unipe amani moyoni,
Niwafariji wa huzuni,
Niwape moyo waondoke
Wameburudika rohoni.
- 6 Unijaze na wema wako,
Nisiweze kuketi bure,
Niende nitangaze pote
Habari za upendo wako.
- 7 Unitume Bwana Yesu,
Upendavyo na upendapo
Hata nifike kwako juu
Nikae nawe furahani.

123 "To the work, to the work." (376)

G.B. 432. [P.M.]

- 1 **K**AZI tu ! kwa bidii Watumishi wa Mungu,
Tumifuata Yesu alipotembea,
Tukichoka tutaburudishwa na Yee,
Basi tufanye kazi ionekanayo ;

Kazi tu ! kwa bidii !
Tutumaini, tukaangalie
Hata kurudi kwa Mwokozi.
- 2 Kazi tu ! kwa bidii ! tulishe wenye njaa
Tuwalettee Yesu walio na kiu ;
Tukajivune katika msalaba tu
Tutatangaza pote, " Wokovu ni bure." n.k.

- 3 Kazi tu ! kwa bidii ! kazi iko kwa wote,
Na ufalme wa Shetani utaanguka
Jina la Mungu Yahuwa na lisifiwe,
Na Wajumbe wataimba, " Wokovu bure." n.k.
- 4 Kazi tu ! kwa bidii ! Kwa uwezo wa Mungu,
Yesu atatujazi mavazi na taji,
Waamini watakapokaa huko juu
Sisi sote tutaimba, " Wokovu bure." n.k.

124 " Take my life and let it be." (377)

S.S. AND S. 616. [7s.]

- 1 **T**WAA uzima wangu wote,
Uwe mtakatifu kwako ;
Na nafasi yangu yote
Nikusifu humo tu.
- 2 Twaa mikono na ifanye
Amri za upendo wako ;
Uitwae miguu pia,
Unapotaka iende.
- 3 Twaa sauti yangu pia,
Nimtukuze Mfalme wangu ;
Twaa midomo nitangaze
Neno lako takatifu.
- 4 Fedha na dhahabu twaa,
Sitaweza nyima senti ;
Twaa akili zangu pia,
Nijitahidie zako.
- 5 Twaa mapenzi yawe yako,
Nisitake nia zangu ;
Twaa moyo uwe hekalu
Humo Wee ukae tu.

- 6 Twaa pendo nalitolea
Nizipende zako tu,
Nafsi yangu uitwae
Niwe kweli wako tu.

SAFARI YA WAKRISTO DUNIANI NA
VITA VYAO

125 " Soldiers of Christ arise." (383)

H.C. 354. [S.M.]

- 1 **A**SKARI wake Kristo,
Silaha zivaeni.
Uwezo hutokea Mungu
Kwa njia ya Mwanawe.
- 2 Kwa nguvu zake Mungu
Sote tu mashujaa,
Tungali tunamtegemea,
Ni lazima tushinde.
- 3 Kwa uhodari wake,
Hatutahofu kitu ;
Silaha zetu za kiroho
Hatuna budi shinda.
- 4 Zidini jibidisha
Kukeshwa na kuomba,
Hivyo mtakavyokanyaga
Nguvu zote za giza.
- 5 Na vita vya dunia
Vikiisha kabisa,
Tutasimama pake Yesu,
Atatujazi taji.

126 "When we walk with the Lord." (385)

S.S. AND S. 642. [P.M.]

1 TUKIMFUATA Yesu
Alivyotuagiza,
Atatufurahisha njiani,
Tukishika mapenzi
Atakaa na sote,
Tulio wasikivu, watii.

Amini, utii,
Maana njia pekee
Ya kumpendeza Yesu,
Uamini, Utii.

2 Sitaona mashaka,
Sitasumbuka bure,
Maana Yeye ni karibu nami,
Sitaogopa kitu,
Wala lia machozi,
Niaminipo tena kutii, n.k.

3 Sitaweza 'lemewa,
Wala kusikitika,
Yuko karibu 'nisaidia,
Na huzuni, hasara,
Hugeuka furaha
Tuaminipo tena kutii, n.k.

4 Kamwe hatutajua
Pendo lilivyo kuu,
Hata tujitoe kwake Yesu ;
Kwani fadhili zake,
Shangwe anayotoa
Ni kwa waamini na watii, n.k.

5 Tutashiriki naye
Tukikaa mbele yake,
Tutafanya atakayo yote,
Atakapopeleka
Tutaenda upesi
Tutaamini tena kutii, n.k.

127 "Standing by a purpose true." (386)

S.S. AND S. 707.

1 TAZAMENI wahodari
Mungu wakimtii,
Heshimuni waamini,
Kundi la Danieli.

Thubutikeni nyie,
Simameni vema,
Nia zako zishikeni
Tena zitangaze.

2 Wapotea mashujaa
Wakihofu watu,
Bora kuiga Danieli,
Umtukuze Mungu, n.k.

3 Washupavu wa Shetani
Watashindwa mara,
Na wathubutuo 'iga
Danieli hodari, n.k.

4 Basi twende mbele tu,
Tutangaze Injili,
Tutafukuza Shetani
Mfano wa Danieli, n.k.

128

" Hold the fort."

(389)

S.S. AND S. 669. [P.M.]

1 NYIE wenzangu tazameni,
Yesu anaita,
Anatuletea msaada,
Kweli tutashinda.

Nyie pigeni moyo konde,
Yesu atuita ;
Mwashirieni ya kwamba,
" Twapigana tu."

2 Na Majeshi ya Shetani
Yanakuja naye,
Watu wengi wanakufa
Kando kando yetu, n.k.

3 Huko mbele ni bendera
Ya Mwokozi wetu ;
Yatulazimu kushinda
Akiwa karibu, n.k.

4 Vita ni vikali sana ;
Sisi tukichoka
Nguvu zake Bwana Yesu
Zitatuwezesha, n.k.

129

" Oft in danger, oft in woe."

(390)

H.C. 361. [7s.]

1 TWEENDE mbele tu Wakristo,
Tushindane na adui ;
Je tutaogopa nini ?
Nguvu za Yesu zatosha.

2 Tukiwamo hatarini
Si kitu, tuendelee ;
Tupigane, tusikome,
Tukiwezesha na Yesu.

3 Mkizimia rohoni
Zikumbukeni silaha ;
Mmepewa toka mbingu,
Lazima mshinde nazo.

4 Msihuzunike tena,
Wala kulia machozi ;
Itupeni mbali hofu,
Mtakavyo, mpewavyo.

5 Twende mbele tupigane,
Mwishoni tu washindaji ;
Adui ingawa wengi
Twende mbele nyie Wakristo.

130 " Why those fears ? Behold, 'tis Jesus." (400)

H.C. 364. [8s. 7s.] Tune Oriel.

1 WAOGOPANI ? Ni Yesu
Aliye Rubani wetu,
Tweka matanga tuende
Baharini mwa maisha ;
Tutafika
Kwenye nchi ya furaha.

2 Tumesikia zake tu,
Bandari tunakokwenda,
Hizo twasadiki sana
Na kuelekea hapo,
Naye Yesu,
Yuko nasi safarini.

3 Kwa nini tusiondoke
Bila kuhofu dharuba,
Humo tunayo amani
Kwani Yesu ni karibu ;
Na mawimbi
Husikia sauti yake.

4 Kweli iko mbele yetu,
Tutakapofika juu,
Shangwe yake kamilifu ;
Hapo watuchukia
Hawawezi
Kusumbua sisi tena.

131 "Who is on the Lord's side." (404)

S.S. AND S. 87. G.B. 501. [IIS.]

1 NANI wake Bwana, watumishi wake,
Watakaoleta watu kwake Yesu ?
Watakaocha vitu vya dunia ?
Watakaokwenda wamipigania ?

Nani wake Bwana, watumishi wake ?
Watakaoleta watu kwake Yesu ?
Kwa fidia yako, kwa neema kuu,
Sisi watu wake, Sisi wako Bwana.
